# Nipashe

Alhamisi Oktoba 6, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581090

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US




UKURASA 27

SUPA JACKPOT

TZS.1,037,361,877

KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.CO.TZ

PIGA *150*87#



**Idadi** watalii yaongezeka hadi 992,690

UKURASA 4



# PSSSF yalipa mafao bil. 60/- kila mwezi

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**RPC ANUSURIKA KIFO KWENYE AJALI YA GARI**

KAMANDA wa Polisi Mkoa wa Simiyu, Kamishna Msaidizi (ACP) Bladius Chatanda...

UKURASA WA 3

**AUAWA KWA KUCHOMWA KISU AKIPORWA SIMU**

MKAZI wa Mwananyamala, Manjunju mkoani Dar es Salaam, Billal Hoza (21)...

UKURASA WA 4

**SHAKA ATIA NENO UAMUZI RAIS WA SAMIA**

KATIBU wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM, Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu...

## Watu wawili washikiliwa tuhuma kunyonga mtoto miaka 3

UKURASA 2



UKURASA 2

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu (kulia), akipimwa joto la mwili na mtaalamu wa afya, alipofika mpaka wa Tanzania na Uganda, eneo la Murongo, wilayani Kyerwa, mkoani Kagera jana, wakati akikagua tahadhari zinazochukuliwa kukabiliana na tishio la ugonjwa wa ebola. **PICHA: MARY GEOFREY**

## Waziri Ummy atinga mpakani kuhamasisha tahadhari ebola

**MICHEZO** SIMBA YAFUNGUKA INACHOKITAKA CAF UK.32

**KABWELA** UK.7

## HABARI KITAIFA

# PSSSF yalipa mafao bil. 60/- kila mwezi

**Na Jenifer Gilla**

MFUKO wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), umesema kila mwezi huwalipa Sh. bilioni 60 wastaafu wa mfuko huo.

Meneja Uhusiano na Elimu kwa Umma wa Mfuko huo, James Mlowe, alisema fedha hizo hulipwa wastaafu 150,000 kwa mwezi.

Aidha, alisema Mfuko huo unalipa zaidi ya Sh. bilioni 120 kila mwezi mafao mengine ikiwamo ya uzazi, ukosefu wa ajira, mafao ya ugonjwa, ya kifo na wategemezi.

Mlowe alisema hayo jana alipotembelea ofisi za magazeti ya Nipashe na The Guardian zilizopo Mikocheni, jijini Dar es Salaam ikiwa ni ziara ya kufahamiana na kujenga uhusiano.

Akizungumzia jumla ya malipo yanayotolewa na Mfuko huo, alisema kila mwezi ni zaidi ya Sh. bilioni 180.

Meneja huyo alisema baada ya kuunganishwa kwa mifuko ya LAPF, PSPF, GEPF na PPF na kuwa mfuko mmoja wa PSSSF mwaka 2018, ulipitia changamoto mbalimbali ikiwamo kukosa pesa za uendeshaji kwa sababu hawakuwa na kipindi cha mpito cha kujijenga bali walianza utekelezaji moja kwa moja kwa kulipa mafao ya wastaafu.

"Tulipounganisha mifuko tulikuwa na deni la Sh. trilioni moja ya malipo ya mafao kwa wastaafu, kwa hiyo hiyo ilikuwa ni changamoto ya kwanza kwenye mfuko," alisema.

Aliitaja changamoto nyingine iliyowayumbisha katika kulipa madeni hayo ni kulazimika kulipa madeni ya wastaafu wa zamani yaliyotakiwa kulipwa na Hazina, ambayo fidia yake haikulipwa kwa wakati.

"Bahati mbaya serikali haikufanikiwa kulipa kwa wakati hiki kiasi ambacho mwanachama alitakiwa kulipwa, kitendo kilichosababisha deni hili kukua hadi kufikia Sh. trilioni 4.6. Hii ilisababisha PSPF ikayumba sana, sasa tulipoungana PSSSF ikaibeba hiyo shida," alifafanua.

Alisema anamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwa katika kipindi cha miezi mitatu ya mwanzo ya uongozi wake alitoa hatifungani ya Sh. trilioni 2.17 kwa ajili ya kulipia deni hilo na kuahidi baada ya miaka mitatu atamalizia kiasi kilichobaki.

"Tunashukuru jitihada za serikali katika kuiokoa PSSSF kwa sababu kiukweli tuliungana, lakini bila hiyo tayari tulikuwa tunarudi chini, kwa sababu unakuwa unalipa zaidi ya unachokipata," alisema.

Vilevile, Mlowe alisema hadi kufikia Februari, mwaka jana walifanikiwa kulipa asilimia kubwa ya wastaafu.

Wastaafu hao wanawalipa kutokana na vyanzo vyao vikubwa vya mapato ikiwamo michango ya wanachama ya kila mwezi wanayokusanya kwa waajiri na uwekezaji katika majengo ya kibiashara alioutaja unafikia ni Sh. trilioni 7.8.

Aidha, Mlowe alisema wamerahisisha huduma kwa wanachama kwa kufungua 'application' kwenye simu inayomwezesha mwanachama kupata huduma zote bila kwenda kwenye ofisi zao.

"Zamani ilikuwa mwajiri akitaka kuleta michango ya mwezi husika atalazimika kuja ofisini kwetu, ajaze fomu za kulipia, kisha aende benki akapange foleni, inachukua muda na watu sasa wana mambo mengi ya kufanya, ndio maana tumekuja na hizo application," alifafanua.

Alisema kuunganishwa kwa mifuko hiyo kumepunguza gharama za uendeshaji kutoka Sh. bilioni 128 kwa mwezi hadi Sh. bilioni 68 hali inayoongeza manufaa kwa wanachama.

Mfuko wa PSSSF una jumla ya wanachama 810,000.



Meneja Uhusiano wa PSSSF, James Mlowe (wa tatu kushoto), akikabidhi mwongozo wa mwanachama wa PSSSF kwa Mhariri Mtendaji wa gazeti la The Guardian, Wallece Mauggo (wa pili kulia) na Mhariri Mtendaji wa gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe (kulia), walipotembelea ofisi za Kampuni ya The Guardian Ltd, Mikocheni jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Ofisa Uhusiano Mwandamizi wa PSSSF, Abdul Njaidi (wa pili kushoto) na Meneja Uhusiano wa Wateja wa IPP Media, Nancy Mwanyika. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Waziri Ummy atinga mpakani kuhamasisha tahadhari ebola

**Na Waandishi Wetu**

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, ametembelea mpaka usio rasmi wa Kashenye jirani na Uganda, Missenyi mkoani Kagera na kuhamasisha wananchi kuzingatia tahadhari zote za tishio la ebola.

Akiwa katika eneo hilo jana, Waziri Ummy aliahidi hema na kuweka wataalamu wa afya katika maeneo ya mipaka isiyo rasmi yenye mwingiliano wa watu ili kuchukua tahadhari ya tishio la ugonjwa huo.

Waziri Ummy alisema mbali na kulipa eneo hilo kipaumbele kwa kuwapa elimu ya kutosha, lakini kuna umuhimu wa kuwa na kituo cha afya katika kata hiyo yenye zaidi ya wakazi 6,000.

"Nafikiri kuna haja ya serikali kuweka nguvu katika eneo hili ambalo mpaka wake siyo rasmi na uliwekwa na wakoloni, kuna mwingiliano mkubwa wa wananchi wa Uganda na Tanzania na Rais Yoweri Museveni ameahidi hatafunga mipaka, kadhalika na Rais Samia Suluhu Hassan naye ameshasema hatafungа mipaka ili shughuli za uchumi ziendelee," alisema Ummy.

Alisema maeneo ya mipaka isiyo rasmi inatakiwa kupewa msukumo mkubwa kwa sababu kuna mwingiliano ambao ni hatari kwa tishio la ugonjwa wa ebola.

Wananchi wa eneo hilo, walimshukuru Ummy kwa kuwa waziri wa kwanza kuwatembelea na kumuomba kuongeza nguvu ya uhamasishaji kwa sababu eneo hilo lilitumika pia kuingiza mgonjwa wa kwanza wa UKIMWI.

Mmoja wa wakazi hao, Anastazi Mathias, alisema mpaka huo ulianza miaka 58 iliyopita, hivyo serikali inatakiwa kuwapa elimu ili kuzuia ugonjwa huo usiingie nchini.

Kaimu Mkurugenzi wa Elimu ya Afya kwa Umma katika Wizara ya Afya, Dk. Amma Kasangala, aliwataka wananchi kuwahi kituo cha afya pindi wanapoona dalili za homa na uchovu wa mwili.

Pia aliwataka wakazi hao kunawa mikono mara kwa mara kwa sabuni na maji tiririka, kuepuka kushikana mikono na kugusa majimaji ya mwili yakiwamo matapishi.

#### MALIMA ACHOMBEZA

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Adam Malima, amewataka wakazi wa mkoa huo kuchukua tahadhari zote ili kujikinga na ugonjwa hatari wa Ebola.

Malima alitoa tahadhari hiyo jana jijini Mwanza katika kikao cha watalaam wa afya kutoka wizara ya afya, mkoa na wakuu wa taasisi za umma.

Alisema ugonjwa huo haujaingia nchini pamoja na mkoa wa Mwanza lakini lazima zichukuliwe tahadhari za kiafya ili kujikinga na janga hilo.

Aliwaomba viongozi wa dini kuendelea kuwahimiza wananchi kuchukua tahadhari ili kuepukana na ugonjwa huo ambao umeripotiwa nchini Uganda.

Naye Dk. Rutachonzibwa aliwaomba wananchi wanaposikia homa, maumivu ya misuli, kutapika na kuona vipele, kuharisha na kutokwa na damu wafike kituo chochote cha afya ili kuchunguzwa.

Pia alisema ili kuepukana na ugonjwa huo, wananchi wanatakiwa kutogusa vitu kama damu, matapishi, kamasi, mate, machozi, kinyesi na majimaji mengine yanayotoka mwilini mwa mtu mwenye Ebola.

***• Imeandikwa na Mary Geofrey na Pelusy Yohana, MWANZA.***

# RPC anusurika kifo ajali gari

**Na Mwandishi Wetu,** BARIADI

KAMANDA wa Polisi Mkoa wa Simiyu, Kamishna Msaidizi (ACP) Bladius Chatanda, amenusurika kifo baada ya gari lake binafsi kugongana uso kwa uso na gari la askari mwenzake.

Wakati Chatanda akinusurika, askari mwenzake, Timoth Philipo, amefariki dunia katika ajali hiyo iliyotokea Busega mkoani Simiyu.

Taarifa iliyotolewa jana na Kaimu Kamanda wa Polisi mkoani Simiyu, Shadrack Masija, ilisema ajali hiyo ilitokea Oktoba 2, mwaka huu, majira ya saa 2:15 usiku katika eneo la Nyakabidi.

Kamanda Masija alisema ajali hiyo ilihusisha magari mawili yenye namba za usajili T 462 BBD aina Toyota Harrier lililokuwa likiendeshwa na Chatanda na gari namba T 766 CCZ aina ya Toyota Mark II lililokuwa likiendeshwa na Philipo.

Alisema chanzo cha ajali hiyo kimetokana na gari lililokuwa likiendeshwa na Philipo aliyekuwa akitokea mjini Bariadi kwenda Lamadi kuhama njia ghafla upande wake wa kushoto wa barabara na kwenda upande wa kulia na kugongana uso kwa uso na gari la Kamanda Chatanda.

Kamanda Masija alisema gari la Kamanda Chatanda lilikuwa likitokea Lamadi kwenda Bariadi.

Aliongeza kuwa katika gari la Kamanda Chatanda alikuwapo msaidizi wake, Konstebo Emanuel ambaye alijeruhiwa na kupelekwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Simiyu kwa ajili ya matibabu.

Kamanda Masija alitoa pole kwa familia ya marehemu na kueleza kuwa Jeshi la Polisi litashirikiana na ndugu katika shughuli zote za mazishi ambayo yatafanyika Magu mkoani Mwanza.

# Washikiliwa tuhuma za mauaji ya mtoto

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

WATU wawili majina yamehifadhiwa kwa sababu za kiuchunguzi wanashikiliwa na polisi mkoani Kagera kwa tuhuma za kuhusika na mauaji ya kumnyonga shingo Aisha Issa (3) kwa kutumia kamba nyembamba ya nailoni.

Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Kagera, William Mwampaghale (pichani), alisema mauaji hayo yalitokea mtaa wa Matopeni Kata ya Kashai, Manispaa ya Bukoba.

Alisema mtuhumiwa wa kwanza alikamatwa siku ya tukio na kumtaja aliyeshirikiana naye ambaye pia alikamatwa Oktoba 3, mwaka huu.

"Tunawashikilia watuhumiwa wote wawili ambao wamekiri kuhusika na mauaji hayo, tutahakikisha wanafikishwa kwenye vyombo vya sheria, lakini tuwahakikishie wananchi kwamba maovu yote yanayofanyika katika mkoa huu ambayo ni ya jinai, jeshi la polisi tumejipanga kukabiliana nayo na kutamtafuta yeyote na popote alipo ambaye



anahusika na matukio haya hususani mauaji," alisema Mwampaghale.

Kutokana na tukio hilo, Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Albert Chalamila, alikwenda kuhani msiba katika familia iliyopoteza mtoto huyo na kusema kuwa jitihada zinafanyika kukomesha vitendo vya mauaji.

Alisema kuwa itafikia hatua vitendo hivyo vitakwisha na ndiyo maana vinafanyika vikao na watendaji wa vijiji, mitaa, kata na maofisa tarafa kuhakikisha amani ya mkoa inakuwapo.

"Nitoe pia elimu wazazi tujitahidi kuwalinda watoto wetu, hata kama anakwenda kucheza mahali tujue wanachezea wapi na yupo na kina nani, tusiwaachie tu watoto wakaenda wanaweza kutumbukia hata katika mitaro, sasa hivi mvua zimeanza kunyesha," alisema Chalamila.

Mtoto huyo ambaye tayari amezikwa katika makaburi ya Kishenge, yaliyoko katika Manispaa ya Bukoba, alitoweka nyumbani kwao Septemba 29, mwaka huu na baada ya msako, mwili wake ulikutwa katika nyumba ambayo haijaisha iliyoko katika mtaa wa Matopeni.




Katibu Mkuu wa Chama cha Democratic Party (DP) Abdul Mluya (wa pili kushoto), na Naibu Katibu Mkuu wa Chama hicho, Felix Makuwa, wakifungua pazia kuzindua ofisi ya makao makuu madogo ya DP, Soko la Rehema Nchimbi, jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Auawa kwa kuchomwa kisu akiporwa simu

**Na Romana Mallya**

MKAZI wa Mwananyamala, Manjunju mkoani Dar es Salaam, Billal Hoza (21), amefariki dunia baada ya kuvamiwa na kundi la vijana waliomchoma kisu sehemu mbalimbali za mwilini na kumpora simu.

Vijana hao wapatao watano walimvamia kijana huyo aliyekuwa amekaa nje ya nyumba yao na kumchoma kisu mgongoni, upande wa moyo.

Kamanda wa Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo lililotokea juzi saa 3:30 usiku, wakati Hiza na rafiki yake wakiwa wamekaa barazani nyumbani kwao, wakichezea simu.

"Wakati wanachezea simu walipita vijana kama wanne, kati yao mmoja akamfuata huyu kijana (Hoza) akampokonya simu, akaendelea kutembea na wenzake, ndipo Hoza akamfuata, akambana na kumtupa chini na mmoja wao akatoa kisu na kumchoma mgongoni, wakaendelea kutembea."

### MAMA MKUBWA ASIMULIA

Akisimulia kuhusu tukio hilo, mama mkubwa wa kijana huyo, Zabibu Maneno, alisema tukio hilo lilitokea juzi saa tatu usiku wakati Hoza na rafiki yake Abrahamu Michael, wakiwa wamekaa barazani nje ya nyumba yao.

Alisema ghafla lilifika kundi la vijana wapatao watano na kutaka simu.

"Hoza alikuwa ameshika simu mkononi anaichezea, hawa wahalifu walipofika wakawa wanataka wapewe simu, rafiki wa Hoza alifanikiwa kukimbia, wamemchoma Hoza na kitu chenye ncha kali karibu na moyo, wamempora simu na kuondoka," alisema.

### RAFIKI AELEZA

Shuhuda wa tukio hilo ambaye ni rafiki wa marehemu, Abrahamu Michael, alisema baada ya kundi hilo kuwavamia, alifanikiwa kukimbia kwenda kutafuta msaada kwa majirani.

"Nilipokwenda kwa majirani kuomba msaada sikupata ushirikiano, niliporudi nikamkuta rafiki yangu akiwa amelala chini anatokwa damu, nilipiga kelele kuomba msaada sikupata, watu walikuwa wanamshangaa tu.

"Niliamua kumbeba hadi hospitali ya Mwananyamala, nikaambiwa tayari amefariki dunia," alisema.

### HOSPITALI

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu wa Afya wa Hospitali ya Rufani ya Mwananyamala, Rajabu Kaseke, alithibitisha kupokelewa kwa mwili wa Hoza.

Alisema waliupokea ukiwa na jeraha na jana ulichukuliwa na polisi kupelekwa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), ili kuchunguza ni jeraha la aina gani.


Reliance Insurance Company (T) Limited

**RELIANCE INSURANCE COMPANY (TANZANIA) LIMITED**

## TAARIFA KWA UMMA

Tunapenda kuutaarifu umma kwa ujumla kwamba wakala wetu wa bima anayeitwa **KELVIN INSURANCE AGENCY amesimamishwa kufanya biashara ya bima kwa niaba ya kampuni yetu. Hivyo basi hatutahusika na hasara au dhima yoyote itakayojitokeza kutokana na miamala ya kibiashara itakayofanywa na KELVIN INSURANCE AGENCY.**

Mtu yeyote ambaye amepewa huduma ya bima na wakala **KELVIN INSURANCE AGENCY** anahimizwa afike mara moja katika ofisi ya **RELIANCE INSURANCE COMPANY (T) LIMITED** kwa ajili ya marekebisho ndani ya siku 14 kuanzia tarehe ya tangazo hili.

Kwa maelezo zaidi tafadhali wasiliana na **RELIANCE INSURANCE COMPANY (T) LIMITED** kwa kupitia anuani ifuatayo:-

**Mkurugenzi Mkuu,**
**Reliance Insurance Company (Tanzania) Limited,**
**Ghorofa ya 3 na 4, Jengo la Reliance,**
**Barabara ya umoja wa mataifa,**
**Upanga,**
**S.L.P 9826,**
**DAR ES SALAAM,**
**Simu: +255 222120088/89/90**



EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

BBN Limited TZA

## OMBI LA KUONESHA NIA KWA UTOAJI WA TAA ZA UMEME NA NGUZO ZA TAA.

## KUMB : ETJ-BB-PR-EI-GEN-EI-0001

BESIX Ballast Nedam Limited, MKANDARASI wa Uhandisi, Ugavi na Ujenzi wa Gati na Kituo cha Kupakia mafuta ghafi katika Ghuba ya Tanga kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), inakaribisha Kampuni zenye uzoefu kueleza nia yao kwa huduma zifuatazo:

**Uhandisi na Ugavi wa Taa za Umeme na Nguzo Za Taa**

Jamhuri ya Uganda, Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Uganda (UNOC), Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na/au Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), pamoja na makampuni mengine ya kimataifa ya mafuta yanashiriki katika utekelezaji wa Mradi wa EACOP.

Kama sehemu ya mradi wa EACOP, mafuta ghafi yatapakiwa kwenye meli kupitia kituo kilicho karibu na ufukwe wa Bahari ya Hindi. Kituo hiki kitakuwa na urefu wa kilomita 2 kutoka ufukweni kutoka eneo la Hifadhi ya Baharini lililopo kwenye peninsula ya Chongoleani mbele ya Bandari ya Tanga nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA WIGO WA VIFAA/HUDUMA:**
- Uhandisi, Ubinifu na Ugavi wa Taa za umeme na Nguzo za Taa

**KIWANGO CHA MAHITAJI:**

Kampuni zinazoonyesha nia yao zinaalikwa kuandika ombi lao kwa kuwasilisha vifuatavyo:
- Dhamana ya kazi ya miezi 24 na miaka 5 ya kasoro fiche (latent defects) baada ya kumalizika kwa muda wa dhamana ya kazi;
- Wasifu wa kampuni ulio na uthibitisho wa uwezo wa kutosha wa kifedha (Ripoti ya ukaguzi wa kifedha ya 2021-2022) na rasilimali za kutosha na zinazofaa kusimamia kandarasi husika.
- Orodha ya tajiriba / uzoefu iliyo na historia ya ugavi / rekodi ya uzoefu usiopungua miaka mitano (5) katika kutekeleza shughuli husika kulingana na viwango vya kimataifa vinavyojulikana katika biashara ya Mafuta na Gesi au soko linaloshabihiana,
- Ubunifu na uteuzi wa bidhaa unapaswa kufanywa kulingana na "Miongozo ya Kitaifa ya Uchafuzi wa mazingira kwa Mwanga kwa wanyamapori" (National Light Pollutions Guidelines for Wildlife)
- Bidhaa zilizochaguliwa zinapaswa kuzingatia viwango wa Mradi
- Rangi ya Nguzo za Taa ya HDG (HDG Coating) inapaswa kuwa angalau mikroni 85
- Taa zinapaswa kuendana na viwango vya Eneo Hatari la Zone 2
- Sera ya Ubora wa Kampuni na mipango ya Afya na Usalama eneo la kazi pamoja na vyeti y aubora vya ISO 9001:2015, ISO 14001:2015, OHSAS 18001 (ISO45001:2018) au vyeti sawa;
- Bidhaa zinapaswa kuzingatia Viwango vya IEC;
- Kuzingatia kanuni za petroli (Local Content) za 2017 na ufafanuzi wa kampuni ya ndani kwa Tanzania.
- Uthibitisho wa usajili/maombi kwa hifadhidata ya Watoa Huduma kwa Wasambazaji wa Ndani (LSSP) wakati wa kuwasilisha maombi, unapendekezwa sana.

Makampuni yanayovutiwa, yanayokidhi mahitaji ya chini kabisa na yana uwezo wa kutoa huduma zilizoorodheshwa hapo juu yanapaswa kuonyesha nia yao kwa kutuma barua pepe pamoja na hati zilizoorodheshwa hapo juu kwa: procurement@bbnjv.com . **(Ukubwa wa Barua Pepe na viambatanishi: MB 20 & Nyaraka zote lazima ziwasilishwe kwa lugha ya Kiingereza)** mnamo au kabla ya tarehe **20 Oktoba 2022 , Saa 12 jioni kwa saa za Tanzania.**

Makampuni yanayokidhi kwa kuridhisha mahitaji ya chini, yatatathminiwa na yakichaguliwa yataalikwa, kulingana na saini ya Makubaliano ya Kutofichua (NDA), ili kushiriki katika mchakato wa zabuni.

**Kumbuka :** Kampuni zilizohitimu awali pekee ndizo zitapokea mwaliko wa kuwasilisha zabuni yao ili kuendeleza mchakato wa Wito wa Zabuni.

217079302

# Idadi watalii yaongezeka hadi 992,690 nchini

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema takwimu za mwaka 2021 zinaonesha kuwa watalii wanaokuja nchini Tanzania wameongezeka kwa asilimia 48.6, kutoka watalii 620,867 mwaka 2020 na kufikia 922,692 mwaka 2021.

Alisema, mbali na kuongezeka kwa idadi ya watalii nchini, pia mapato yatokanayo kutoka sekta hiyo yameongezeka kwa asilimia 81.8 kutoka Dola za Marekani milioni 714.59 mwaka 2020 na kufikia Dola bilioni 1.3 mwaka 2021.

Aliyasema hayo jana alipomwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan, kwenye ufunguzi wa mkutano wa 65 wa Shirika la Utalii Duniani - Kamisheni ya Afrika unaofanyika jijini Arusha.

"Pia takwimu za mwaka 2022 zinaonesha kuwa Sekta ya Utalii inazidi kuimarika zaidi hususan baada ya uzinduzi wa Programu Maalumu iliyotekelezwa na Rais Samia ya The Royal Tour, iliyozinduliwa rasmi Aprili 2022 katika soko letu la utalii la kimkakati nchini Marekani."

Alisema mafanikio hayo ni matokeo ya mwongozo mzuri uliotolewa na Shirika la Utalii Duniani kwa nchi wanachama ikiwamo Tanzania katika kukabiliana na athari za UVIKO - 19. "Kwa msingi huo, ninatumia fursa hii kulishukuru Shirika la Utalii Duniani hususan, kwako Mheshimiwa Zurab Pololikashvili, Katibu Mkuu wa Shirika la Utalii Duniani kwa kuiongoza vyema sekta ya utalii katika kipindi chote cha janga hilo."

Hata hivyo, alisema lengo la serikali ni kuendelea kuongeza idadi ya watalii wanaoingia nchini hadi kufikia milioni tano na mapato ya Dola za Marekani bilioni sita ifikapo mwaka 2025. "Utajiri wa vivutio vya utalii tulivyonavyo umeifanya sekta ya utalii kuwa muhimili muhimu wa uchumi wa nchi yetu."

Kadhalika, Majaliwa alitoa rai kwa mashirika na taasisi za kimataifa kuendelea kuiamini Tanzania na kuichagua kama sehemu sahihi ya kufanyia matukio yenu mbalimbali ikiwamo mikutano adhimu kama huo.

Naye, Katibu Mkuu wa Shirika la Utalii Duniani, Zurab Pololikashvili, alisema baada ya mlipuko wa janga la UVIKO-19 nchi nyingi duniani ziliathirika kwa kiasi kikubwa katika sekta ya utalii, watahakikisha wanaendelea kuweka mikakati ya kurejesha katika hali yake ya kawaida.

"Wiki iliyopita tulisherehekea siku ya utalii duniani iliyokuwa na kaulimbiu ya Rethinking Tourism, ambayo tunaamini itasaidia kuirejesha sekta hiyo katika hali yake ya kawaida na kuendelea kusaidia kutoa mchango katika ukuaji wa uchumi na kuongeza idadi ya ajira."

Alisema, Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo zina vivutio bora vya kutembelea kwa ajili ya utalii na watu wengi duniani wameitambua kupitia filamu maarufu ya The Royal Tour. "Ninafurahi sana kuwa miongoni mwa watu walioshuhudia filamu hiyo ambayo imenimeweza kuona tamaduni na vivutio vilivyopo katika ardhi hii ya Uhuru na Umoja."

Awali, Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana alisema kuchaguliwa kwa Tanzania kuwa mwenyeji wa mkutano huo ni matokeo ya ushirikiano mzuri kati ya nchi yetu pamoja na jumuiya ya Kimataifa katika masuala mbalimbali yakiwamo ya utalii. Mkutano huo umehudhuriwa na washiriki kutoka nchi 33 wanachama wa Shirika la Utalii Duniani-Kamisheni ya Afrika.




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akikabidhi zawadi ya picha ya Mlima Kilimanjaro kwa Katibu Mkuu wa Shirika la Utalii Duniani, Zurab Pololikashvili, baada ya kufungua mkutano wa 65 wa Shirika la Utalii Duniani Kamisheni ya Afrika, jijini Arusha, jana. Kulia ni Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana. **PICHA: OWM**

# Walimu wataja vikwazo utendaji kazi

**Na Augusta Njoji,**

CHAMA cha Walimu Tanzania (CWT), kimetaja vikwazo vinne ambavyo vinawakabili walimu ikiwamo ukosefu wa nyumba na baadhi kuishi kwenye mazingira mabovu hali inayoathiri ufundishaji.

Vikwazo vingine ni kutokuwa na posho ya kufundishia na mishahara mizuri hali inayosababisha wawe na mikopo mingi inayowaumiza na kuathiri utendaji kazi wao.

Pia kimesema kutokuwapo na mafunzo kazini yanayoendana na mabadiliko ya mitaala kumechangia kuwa na baadhi ya walimu wanaofundisha teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) wakiwa hawawezi kuwasha kompyuta.

Kilio hicho walikitoa jana kwenye kongamano la Siku ya Walimu Duniani ambalo kimkoa lililofanyika katika Chuo cha Ualimu cha Bustani, wilayani hapo.

Akizungumza kwenye kongamano hilo, Mkuu wa Idara ya Elimu na Mafunzo wa CWT, Stella Kiyabo, alisema serikali inaajiri mwalimu lakini anapelekwa eneo hata nyumba ya kuishi hakuna.

"Tunaona serikali inajenga madarasa kweli tunapongeza dhamira yake lakini kasi hiyo iende sambamba na nyumba za walimu. Tumesikia itajenga mwaka huu wa fedha nyumba 809 ambazo bado ni ndogo. Tunaomba tupewe kipaumbele, kuna nyumba huko walimu wanaishi hazifai kukaliwa zina hali mbaya, hakuna maji wala umeme," alisema.

Alisema takwimu za Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) za mwaka 2020, zinaonyesha kuwa bado kuna mahitaji makubwa ya nyumba za walimu ambayo mahitaji ya shule za msingi za serikali ni 237,121, zilizopo ni 44,363, upungufu ni 192, 758 sawa na asilimia 81.3.

Pia alisema mahitaji ya shule za sekondari za serikali ni 81,973, zilizopo 14,274 na upungufu ni 67,699 sawa na asilimia 83.

Alishauri kufanyika mabadiliko kwenye mwongozo wa usajili wa shule kwa kuweka nyumba ya mwalimu kama kipengele muhimu kwa shule kusajiliwa.

Naye Mjumbe wa Kamati Tendaji Taifa ya CWT, Bakari Mtembo, aliwataka walimu kuondoa unyonge kwenye kupambania haki zao na kutokubali kurudi nyuma.

"Msifanye haya tunayodai ni ya viongozi hapana tupambane wote ili yafanyike yataleta tija kwenye ufundishaji wetu, maana mwaka 2012 tulipotaka kugoma tuliambiwa mtakosa sensa tukatulia huo ndo ukweli,"alisema.

Kuhusu posho, alisema CWT inaiomba serikali kurejesha posho ya kufundishia ili kufidia muda wa ziada ambao mwalimu anautumia kufanya maandalizi.

## Shaka atia neno uamuzi Rais Samia

**Na Mwandishi Wetu,** KILOSA

KATIBU wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM, Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, amevunja ukimya baada ya Rais Samia Suluhu Hassan, kufuta umiliki wa mashamba makubwa yenye ekari 23,016 katika wilaya za Mvomero na Kilosa mkoani Morogoro.

Rais Samia, baada ya kufuta umiliki huo ameagiza yagawanywe kwa wananchi kutokana na wawekezaji kushindwa kuyaendeleza.

Akizungumza wakati akizindua msimu wa kilimo kwa mkoa wa Morogoro juzi, Shaka alisema, ufutaji wa mashamba hayo haukufanywa kwa bahati mbaya au kwa kubahatisha bali ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2020-2025.

"Ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi imezungumza vizuri sana. ukisoma Ibara ya 74 tumezungumza vizuri namna ya kuhuisha na kuboresha matumizi bora ya ardhi. Pia, tumezungumza namna ya kufuta mashamba ambayo kwa muda mrefu kuna watu walijimilikisha na wakayatelekeza.

"Lakini, mashamba ambayo wajanja wajanja waliamua kuyachukua ili kukwamisha shughuli za maendeleo, bahati nzuri nimewahi kuwa Katibu wa CCM katika Mkoa wa Morogoro kwa kipindi cha miaka miwili.

"Nilipofika kwenye mkoa huu kwa kipindi cha miezi sita sikukaa ofisini, nilikuwa nakuja na kurudi Kilosa asubuhi na jioni. Kazi moja kubwa ambayo niilifanya kwa ustadi mkubwa ni kupokea malalamiko ya ardhi. Nadhani kwenye mkoa wa Morogoro, Kilosa ilikuwa inaongoza kwa malalamiko ya ardhi. Kesi kubwa za wilaya hii, wako watu wamejimilikisha mashamba na hayaendelezwi," alisema.

Aliongeza kuwa, wako wajanja wamechukua mashamba ya wenzao lakini hakuna kinachofanyika, lakini kesi kubwa ya Kilosa ilikuwa namna ambavyo hakukua na mpango bora wa matumizi ya ardhi.

"Kwa sababu sisi tulifanya kazi kubwa sana na tulifanya kazi ngumu kweli kweli, kwa maoni yangu viongozi mlioko kwenye mkoa huu mmeanza vizuri," alisema.

Shaka alisema Rais Samia, tangu ameingia madarakani ameweka mkazo katika kilimo ndiyo maana wote ni mashahidi kwa kuwa ameongeza bajeti ya kilimo kwa kiasi kikubwa kutoka Sh. bilioni 294 mwaka 2021/22 hadi Sh. bilioni 954 mwaka 2022/23.

"Hiyo haijapata kutokea tangu tumepata uhuru kwenye bajeti ya kilimo yenye fedha nyingi kama hii. Maana yake tunakwenda kutafsiri kwa vitendo kwamba kilimo ndio uti wa mgongo lakini kilimo ndiyo mkombozi kwa maendeleo ya nchi yetu."

HABARI KITAIFA

# Mtambo kuchenjua makinikia wasimikwa

**Na Mwandishi Wetu,** GEITA

KATIKA kutekeleza mpango wa kulinda mazingira na kuunga mkono juhudi za serikali kuifanya Tanzania kuwa nchi ya viwanda ifikapo mwaka 2025, Kampuni ya uchimbaji madini ya dhahabu ya Geita (GGML) imenunua na kusimika mtambo wenye thamani ya Sh. bilioni moja kwa ajili ya kuchenjua kaboni 'makinikia' inayotokana na uchimbaji wa madini hayo.

Hatua hiyo inaifanya Tanzania kuwa nchi ya kwanza na pekee katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati kuwa na mtambo huo kwa kuwa hapo awali kampuni hiyo ilikuwa inafuata huduma hiyo Afrika Kusini.

Hayo yalibainishwa juzi wakati ziara ya Waziri wa Madini, Dotto Biteko, alipotembelea kampuni hiyo mkoani hapa kwa lengo la kujua maendeleo ya GGML baada ya kuanza shughuli za uchimbaji wa chini ya ardhi katika migodi yake mitatu.

Makamu Rais wa AngloGold Ashanti, anayeshughulikia Miradi Endelevu kwa upande wa Ghana na Tanzania, Simon Shayo, alisema mradi huo utaongeza mapato kwa serikali na kampuni hiyo kwa ujumla.

"Mradi huu wa kuchenjua mabaki ya kaboni unatusaidia kuhakikisha hatuyatupi mabaki ya dhahabu na mabaki yenye asili ya hewa ukaa yanayoingia kwenye mazingira kwa sababu dunia nzima ipo kwenye mapambano ya kupunguza hewa ukaa," alisema.

Akizungumzia mradi huo, Dk. Biteko alisema, awali kaboni zilizokuwa zinazalishwa kwenye migodi iliyopo nchini zilikuwa zinasafirishwa kwenda nje ya nchi.

"Tulizuia watu wakadhani tunafanya kitu kibaya, sasa GGML wameweka mtambo mpya ambao umegharimu Sh. bilioni moja kwa ajili ya kuchenjua upya kaboni za dhahabu na kupata dhahabu safi badala ya kusafirishaile kaboni kupeleka nje ya nchi," alisema.

Aliongeza kuwa mbali na manufaa ya mapato ambayo nchi inapata, pia watu wengi wameajiriwa kwenye mtambo huo na kuondokana na umaskini.

"Lakini pili teknolojia ya kaboni hizi ambazo zinazalishwa kwenye migodi mingine zitakuwa zinafanyiwa 'processing' (kuchakatwa) hapa nchini hasa ikizingatiwa ile kaboni ina dhahabu.

"Mahali pengine unaweza kuona ile kaboni imetupwa kama uchafu, lakini kwa taarifa tuliyopewa itazalisha zaidi ya gramu 80,000. Ni dhahabu nyingi zaidi ya kilo 80 kwa kaboni hii na bado itaendelea kuzalishwa mara nyingi. Kwa hiyo, tutapata mapato mengi zaidi.

"Hakuna mgodi mwingine ambao umetengeneza mtambo wa kuchenjua hiyo kaboni Afrika Mashariki na Kati, hivyo teknolojia hii sisi tumekuwa walimu. Ninawapongeza GGML kwa ubunifu huu," alisema.

Mbunge wa Geita Mjini, Constantine Kanyasu (CCM), aliipongeza kampuni hiyo kwa hatua ilizochukua kuhakikisha inapanua wigo wa upatikanaji wa ajira kwa Watanzania.

"Mathalani, tukizungumzia 'local content', tulitaka iwe local of the local', ninauona ushawishi huo unafanikiwa kwa sababu sasa katika maeneo mengi ambayo nimekwenda nimeona ushiriki wa watu wa Geita kwenye shughuli mbalimbali za uchumi wa mgodi," alisema.



Mtambo wa kuchenjua kaboni 'makinikia' yanayotokana na shughuli za uchimbaji madini ya dhahabu wenye thamani ya Sh. bilioni moja, uliosimikwa na kampuni ya Geita Gold Mining Ltd (GGML). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Tanzania yang'ara kinyang'anyiro ITU

**Na Elizabeth Zaya**

TANZANIA imechaguliwa katika kinyang`anyiro cha ujumbe wa Baraza Tendaji la Shirika la Mawasiliano Duniani (ITU).

Ushindi huo umetokana na uchaguzi uliofanyika kwenye mkutano mkuu wa Shirika hilo ambao hufanyika kila baada ya miaka minne, na mwaka huu umepewa jina la ITU Plenipotentiary Conference 2022(ITU PP-22).

Tanzania imekuwa kinara katika wingi wa kura miongoni mwa nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika(SADC) zilizokuwa kwenye kinyang`anyiro cha nafasi hiyo na Afrika Kusini zinawakilisha ukanda wa SADC kwenye baraza hilo.

Katika uchaguzi huo, Tanzania ilipata kura 141 huku Afrika Kusini ikipata kura 122.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, alisema ushindi huo wa kura miongoni mwa nchi za SADC, unathibitisha namna ambavyo nchi za ukanda huo chini ya Jangwa la Sahara zilivyo na imani kwa mchango ambao Tanzania imekuwa ikitoa katika kukuza sekta ya mawasiliano.

Alisema, miongoni mwa nchi wanachama wa SADC ambazo Tanzania inahusika moja kwa moja kuziwezesha katika huduma za mawasiliano kupitia mkongo ni pamoja na Msumbiji, Malawi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na Burundi.

"Katika uchaguzi huo, Tanzania ilichaguliwa kuwa mjumbe wa Baraza la ITU kwa kura 141 kati ya 180 zilizopigwa, ikiwa ushindi muhimu na mkubwa ikizingatiwa kwamba Julai mwaka huu ilipata uanachama wa Baraza la Umoja wa Mawasiliano Afrika (ATU) kwa kipindi cha miaka minne ijayo inayoanzia 2023 baada ya wajumbe wa mkutano mkuu kuipitisha kwa kauli moja katika mkutano mkuu wa sita wa Umoja huo uliofanyika Algiers, Algeria," alisema Nape.

# Ahukumiwa kifungo madai kujifanya mdhamini daktari anayedaiwa kubaka

**Na Mwandishi Wetu**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imemtia hatiani na kumhukumu papo hapo Ferguson Mapunda kwa kosa la kuidanganya Mahakama kuwa ni mdhamini wa daktari wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Amana, Dar es Salaam, Dk. Joseph Mwaipola, anayetuhumiwa kubaka wakati si kweli.

Mapunda, alihukumiwa kwenda jela miezi sita au faini Sh 100,000 baada ya kufanya tukio hilo jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Yusto Roboroga, wakati shauri hilo la ubakaji lilipotakiwa kusikilizwa.

Dk. Mwaipola alishtakiwa kwa mashtaka matatu yakiwamo kumbaka mtoto wa miaka 17 ( jina linahifadhiwa).

Shauri lake lilikuja kwa ajili ya kusomewa maelezo ya awali lakini hakuwapo kwa madai kuwa anaumwa.

Wakili wa Serikali, Sylvia Mitanto, alidai mshtakiwa hayupo na upande wa mashtaka ulijipanga kumsomea maelezo ya awali.

Alipotakiwa mdhamini wa mshtakiwa kutoa taarifa, alisimama Mapunda ambaye ni mkwe wa mshtakiwa na kudai ni mmoja wa wadhamini watatu wa mshtakiwa.

Hakimu alimhoji maswali ambapo alijibu ni mdhamini na aliwasilisha barua kwa ajili ya kumdhamini.

Hakimu alipitia kumbukumbu za mahakama na kubaini jina lake halimo katika idadi ya wadhamini wawili waliomdhamini mshtakiwa.

Alihojiwa kwa nini ameidanganya mahakama kisha alikamatwa na kuwekwa mahabusu kwa hatua zingine za kisheria, baadaye alipanda kizimbani na kupewa adhabu ya kifungo cha miezi sita jela au faini Sh 100,000. Hadi mahakama inamalizika walikuwa wanatafuta fedha za kulipa faini.

Mwaipola katika shtaka la kwanza la ubakaji, anadaiwa alilitenda Februari, 2022 katika Hospitali ya Amana kwa kumbaka binti wa miaka 17.

Shtaka la pili, inadaiwa Mei 31, mwaka huu, katika nyumba ya kulala wageni ya Pazuri iliyoko Temeke, Dar es Salaam, mshitakiwa alimbaka binti huyo.

Wakili Sylvia, alidai shtaka la tatu ambalo ni kulawiti, mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo Februari, mwaka huu, katika Hospitali ya Amana ambapo alimlawiti binti huyo.

Mshtakiwa yuko nje kwa dhamana kwa masharti ya kuwa na wadhamini wawili wenye barua ya utambulisho pamoja na vitambulisho vya kura au vya kazi watakaotia saini dhamana ya Sh. milioni tano.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ongezeko la watalii nchini habari njema

**ONGEZEKO** la watalii nchini kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2021 kwa asilimia 48.6 ni za kutia moyo kutokana na sekta hiyo kuwa moja ya zinazochangia fedha za nje.

Watalii kwa mwaka 2020 walioingia nchini walikuwa 620,867 hadi kufikia 922,692 mwaka 2021.

Ongezeko hilo kwa mujibu wa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa limeongeza mapato yanayotakana na sekta ya utalii kwa asilimia 81.8 kutoka Dola za Marekani milioni 714.59 mwaka 2020 na kufikia Dola za Marekani bilioni 1.3 mwaka 2021.

Hiyo ni dalili nzuri ya matokeo ya uzinduzi wa programu maalumu iliyotekelezwa na Rais Samia Suluhu Hassan, Aprili mwaka huu.

Takwimu hizo zilitolewa na Waziri Mkuu kwenye ufunguzi wa Mkutano wa 65 wa Shirika la Utalii Duniani - Kamisheni ya Afrika unaofanyika jijini Arusha.

Hali ya utalii nchini ilianza kuyumba baada ya dunia kukumbwa na janga la UVIKO-19 ambapo nchi nyingi duniani zilifunga mipaka yake kwa kuogopa maambukizi ya ugonjwa huo.

Hata hivyo, kutokana na mwongozo mzuri uliotolewa na Shirika la Utalii Duniani kwa nchi wanachama ikiwamo Tanzania katika kukabiliana na athari za ugonjwa huo, dunia imeanza kufunguka na watu wameanza kusafiri bila kuwa na masharti magumu.

Mwongozo huo umesaidia kufungua fursa za uchumi kwa kuwa hata wafanyabiashara waliokuwa wakitegemea kusafiri ili kufanya shughuli zao walikwama kutokana na ugonjwa huo.

Waziri Mkuu amesema lengo la serikali ni kuendelea kuongeza idadi ya watalii wanaoingia nchini hadi kufikia watalii milioni tano na mapato ya Dola za Marekani bilioni sita ifikapo mwaka 2025.


Serikali pia imetoa rai kwa mashirika na taasisi za kimataifa kuendelea kuiamini Tanzania na kuichagua kama sehemu sahihi ya kufanyia matukio mbalimbali ikiwamo mikutano adhimu.

Katibu Mkuu wa Shirika la Utalii Duniani, Zurab Pololikashvili amesema kuwa baada ya mlipuko wa janga la UVIKO 19 nchi nyingi duniani ziliathirika kwa kiasi kikubwa katika sekta ya utalii, hivyo watahakikisha wataendelea kuweka mikakati ya kurejesha katika hali yake ya kawaida.

Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo zina vivutio bora vya kutembelea kwa ajili ya utalii na watu wengi duniani wameitambua kupitia filamu maarufu ya The Royal Tour. Yeye amekuwa miongoni mwa watu walioshuhudia filamu hiyo ambayo ameweza kuona tamaduni na vivutio vilivyoko Tanzania.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana alisema kuchaguliwa kwa Tanzania kuwa mwenyeji wa mkutano huo ni matokeo ya ushirikiano mzuri kati ya Tanzania na jumuiya ya kimataifa katika masuala mbalimbali yakiwamo ya utalii. Mkutano huo umehudhuriwa na washiriki kutoka nchi 33 wanachama wa Shirika la Utalii Duniani-Kamisheni ya Afrika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253 676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Tuwajibike kuhakikisha tunakabili shida ya afya akili ndani ya jamii

Na Yasmine Protace

**MAGONJWA** ya afya ya akili ni kati ya matatizo ya ubongo yanayomfanya mtu kuwa na hasira, fikra na matendo tofauti.

Afya ya akili inamfanya mtu kuwa na matendo tofauti na yale yanayotarajiwa na jamii, hata kusababisha kushindwa kukabiliana na changamoto za kimaisha.

Inaelezwa kuwa magonjwa hayo ya afya ya akili yanaweza kusababishwa na sababu za kibaiolojia au kisaikolojia.

Afya ya akili, kimsingi inajumuisha ustawi wetu wa kihemko, kisaikolojia na kijamii na inapomkumba mtu, huwa inaathiri jinsi tunavyofikiria kuhisi na kutenda.

Hivi karibuni Katibu Tawala wa Mkoa wa Dar es Salaam Rehema Madenge ametamka akirejea Shirika la Afya Duniani (WHO), kwamba katika kipindi cha muongo mmoja uliopita, kumekuwapo ongezeko la takribani asilimia 13 ya wagonjwa wa akili.

Rehema anasema, katika ufunguzi wa Maadhimisho ya Wiki ya Afya ya Akili Duniani yaliyofanyika mnamo Oktoba 3, mwaka huu katika viwanja vya Mnazi Mmoja Jijini Dar es Salaam, yenye kaulimbiu ya 'afya ya akili ni kipaumbele kwa wote.'

"Kwa mujibu wa takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO), katika kipindi cha muongo mmoja uliopita kumekuwa na ongezeko la takribani asilimia 13 la wagonjwa wa akili," anasema.

Anafafanua kwamba, inakadiriwa kuwa kuna wagonjwa milioni saba wenye magonjwa mbalimbali ya akili na matumizi ya dawa za kulevya nchini, huku miongoni mwao zaidi ya watu milioni1.5 wanaishi na ugonjwa wa sonona.

Sambamba na hilo, ameweka wazi kwamba kumekuwapo matukio mengi ya ukatili ambayo wanawake wanne kati ya 10 walio katika umri wa miaka 15 hadi 49 walifanyiwa ukatili wa kimwili, wakati takribani wanawake wawili kati ya kumi walifanyiwa ukatili wa kingono, hiyo hutokana na ongezeko la magonjwa ya akili.

**Sababu kubwa ya matatizo ya afya ya akili ni mabadiliko katika mfumo wa malezi ndani ya familia na jamii, msongo wa mawazo unaotokana na ugumu wa kushindwa kuhimili mahitaji ya kila siku, na matumizi ya vilevi hususani pombe, bangi na dawa nyingine za kulevya.**

Anaongeza kuwa sababu kubwa ya matatizo ya afya ya akili ni mabadiliko katika mfumo wa malezi ndani ya familia na jamii, msongo wa mawazo na matumizi ya vilevi kupita kiasi hususani pombe, bangi na dawa nyingine za kulevya.

"Sababu kubwa ya matatizo ya afya ya akili ni mabadiliko katika mfumo wa malezi ndani ya familia na jamii, msongo wa mawazo unaotokana na ugumu wa kushindwa kuhimili mahitaji ya kila siku, na matumizi ya vilevi hususani pombe, bangi na dawa nyingine za kulevya," anafafanua.

Pia, anatoa wito kwa wananchi kusaidia wahusika wa matatizo ya afya ya akili kupata matibabu, huku akisisitiza kuepuka unyanyapaa na kuwatenga wagonjwa hao ili kuwasaidia kurudi katika hali ya kawaida.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Rashid Mfaume amesema, mpaka sasa, huduma za afya ya akili zinaendelea kutolewa katika vituo vya kutolea huduma za afya vya umma na vya binafsi Jijini Dar es Salaam.

Msisitizo ni kwamba huduma hizo zinatolewa kwa kutumia wataalamu wabobezi katika utoaji huduma za afya ya akili, lakini katika vituo ambavyo havina wabobezi wa afya ya akili, watoa huduma wengine wamekuwa wakijengewa uwezo ili kuhakikisha kuwa wananchi wananufaika na huduma hiyo.

Hapa anafafanua pia Mkurugenzi Msaidizi wa magonjwa yasiyoambukiza Wizara ya Afya, Dk. James Kiologwe, anasema takwimu kutoka vituo vya kutoa huduma za afya ya mwaka 2019/20 nchini, zinaonyesha takribani wagonjwa 711,789 sawa na asilimia 10 tu ya wagojwa milioni saba, wamepatiwa huduma za afya ya akili na kukiri kuwa, idadi hiyo ndogo ya mahudhurio inachangiwa na uelewa mdogo wa jamii, kuhusiana na matatizo ya afya ya akili na unyanyapaa.

HABARI KITAIFA



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi (kushoto), akiwa na mteja wa benki hiyo tawi la Mlimani City, wakikata keki ya kusherehekea uzinduzi wa mwezi wa huduma kwa wateja, mkoani Dar es Salaam mapema wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Majaliwa aagiza mashirika yasiyo ya kiserikali kutumia benki za Tanzania

**Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, ameagiza mashirika yasiyo ya kiserikali nchini kufungua akaunti zao katika benki za ndani, akisisitiza kuwa kufanya hivyo ni kuonyesha uzalendo.

Majaliwa, alitoa agizo hilo juzi alipozungumza na wananchi na watumishi wa Benki ya NMB alipotembelea banda la benki hiyo katika kilele cha Jukwaa la Mwaka la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

Waziri Mkuu alitembelea NMB na kuzungumza na mashirika yasiyo ya kiserikali nchini ili kuwafungulia akaunti ndani ya benki hiyo ambayo ina matawi kila kona ya nchi.

Majaliwa alisema, mpango huo mbali na kuonyesha uzalendo pia utasaidia kuongeza mzunguko wa fedha ndani ya nchi, jambo litakalotafsiriwa kama kitendo cha kizalendo.

"Ninyi benki ndiyo mnapaswa kuwa wa kwanza kuzungumza na hawa watu, sina shaka na NMB kwamba fedha za mashirika haya zitakuwa salama kama zilivyo salama fedha zingine," alisema Majaliwa.

Waziri Mkuu, alirudia kauli hiyo akiwa ndani ya ukumbi na wakati akihutubia, alisisitiza mashirika yasiyo ya kiserikali kuwa utafika wakati watatulizana.

Majaliwa pia, aliziagiza taasisi kuelekeza nguvu zao vijijini badala ya kuendelea kulundikana mijini ambako kila kitu kinapatikana.

Meneja Mwandamizi wa Uhusiano katika Benki ya NMB, Dorah Monyo alisema utaratibu wa kuweka fedha kwa benki za ndani utakuwa na faida kubwa kwa wananchi kwa kuwa mzunguko wa fedha unabaki ndani.

Dorah alisema, kiasi cha fedha za mashirika hayo kama kitawekezwa katika benki za ndani ya nchi ni wazi kuwa kuna vitu vingine vitakuwa tofauti na sasa na maisha yataendelea vizuri kwa kuaminika kwa taasisi hizo.

"Lakini sisi NMB tumepunguza gharama za uendeshaji, hivyo hakuna tatizo kama fedha zao zitatunzwa kwenye benki za ndani. Ninadhani Waziri Mkuu yuko sahihi katika jambo hilo, tusubiri utekelezaji wake," alisema.

Dorah alimwahidi Waziri Mkuu kwamba, NMB itakuwa benki ya kwanza kuyasaidia mashirika hayo kuwa na akaunti ndani ya benki na uendeshaji wake ni wa gharama nafuu zaidi.

Mwenyekiti wa Mtandao wa Mashirika Yasiyokuwa ya Kiserikali, Dk. Lilian Badi alisema, ni wakati kwa taasisi binafsi kuwekeza fedha zao kwa benki za nyumbani ili kuchangia ukuaji wa uchumi na kwamba hakuna sababu za kuwekeza nje wakati ndani ya nchi kuna nafasi.

Dk. Badi aliomba serikali kuzipa nafasi taasisi zisizo za kiserikali ikiwamo kuwapa uhuru wa kufanya majukumu yao kuliko sasa ambapo wamebanwa, hasa kipengele cha usajili wa miaka 10, akiomba kifutwe kwa kuwa kinawakosesha nafasi ya kujadiliana na wadau kuhusu miradi mikubwa.

## Wamlalamikia mwenyekiti kwa DC kwa madai ya kuwapora mashamba

**Na Steven William,** IRINGA

BIBI kikongwe Veronica Chusi (84), amemlalamikia Mwenyekiti wa Kijiji cha Mgera Wilaya ya Iringa, Lucas Mgata, kwa madai ya kupora ardhi yake kwa njia ya kuazima kwa ajili ya kilimo lakini baadaye akaifanya mali yake.

Chusi alitoa malalamiko hayo juzi kwa Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Mohamed Moyo, kwenye mkutano wa kupokea malalamiko ya wananchi katika kata mbalimbali.

Alisema alianza kuitumia ardhi hiyo kabla mwenyekiti huyo hajazaliwa na sasa Mgata anasema amerithishwa na wazazi wake jambo ambalo si la kweli. Alisema tangu kiongozi huyo aingie madarakani, amekuwa na tabia ya kupora ardhi kutoka kwa wananchi.

"Ukilalamika mwenyekiti huyu anatishia kukuua na hii inatufanya wananchi wengi kuacha kufuatilia haki zetu. Tunaomba serikali itusaidie," alisema bibi huyo huku akizungumza kwa kihehe.

Kikongwe mwingine, Lusia Mbugano (90) alisema mwenyekiti huyo amekuwa akiwanyang'anya ardhi mara kwa mara na walikuwa wanakaa kimya kutokana na kutishiwa amani na kiongozi huyo.


Mbugano alisema mara ya kwanza aliwapora ardhi ambayo waliachiwa urithi na marehemu baba yao, Mzee Mwesimpya Nyaulingo mwaka 1937 lakini kiongozi huyo amekuwa akitumia njia mbalimbali ikiwamo kuwatisha anapotaka kupora ardhi.

Alisema hivi sasa familia yake haina hata eneo la kulima kutokana na kuporwa maeneo yao na mwenyekiti huyo, hivyo kuiomba serikali kusaidia kutatua mgogoro huo.

Mbugano alisema hivi karibuni mwenyekiti huyo alimpora tena ekari tatu ambazo alikuwa amebakiwa nazo, na sasa unakaribia muda wa kulima na hana eneo, hivyo kuiomba serikali kuharakisha kutatua tatizo hilo.

Naye Ayubu Mtweve, mkazi wa kijiji hicho alisema mwenyekiti huyo amempora ardhi yenye zaidi ya ekari mbili ambazo anamiliki kwa zaidi ya miaka 30 na kwamba kiongozi huyo amekuwa akihusishwa kwenye migogoro ya ardhi kwa kupora ardhi za wananchi kwa kutumia madaraka aliyo nayo.

## KABWELA



# Mabadiliko tabianchi kikwazo kwa maendeleo ya wanawake

**Na Mwandishi Wetu,** SAME

WATAFITI na wadau wametakiwa kujadili na kubuni nishati mbadala ya kutumia kwa ajili ya kupikia ili kupunguza matumizi makubwa ya kuni katika kipindi kigumu cha mabadiliko ya tabia nchi ambayo waathirika wakuu ni wanawake.

Wito huo ulitolewa jana na Mwenyekiti wa Bodi ya Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Gema Akilimali, wakati wa ufunguzi wa Tamasha la Kijinsia Kanda ya Kaskazini, mjini hapo lililoandaliwa na shirika hilo kwa kushirikiana na mashirika mengine yasiyo ya kiserikali, lililofunguliwa na Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu.

Alisema ni ukweli usiopingika kwamba mwanamke ndio mwathirika wa kwanza katika changamoto za mabadiliko ya tabia nchi, kwa kuwa kunapokuwa na ukame atahangaika kutafuta maji na kuandaa chakula.

"Nimefarijika zaidi kujua kwamba tamasha hili pamoja na mengineyo linalenga kujadili madhara ya mabadiliko ya tabia nchi, jambo ambalo ni muhimu kwa mustakabali wa nchi kwa kuwa ni ukweli kuwa mabadiliko ya tabia nchi yana athari kubwa kwenye usalama wa chakula," alisema.

"Mjadala huu unakuja wakati sahihi kwenye dunia inakabiliwa na changamoto nyingi za mabadiliko ya tabia nchi ambayo Tanzania ni sehemu ya dunia.

"Tunapojadili suala hili niwaase wajadiliane kubuni nishati mbadala ya kutumiwa kupikia ili kupunguza matumizi makubwa ya kuni, jambo linalopelekea maeneo mengi kuwa nusu jangwa kutokana na ukataji holela wa miti. Tutaweza kukabiliana na ukame unaotishia usalama wa chakula nchini, kila mtu ajitahidi kupanda miti," alisisitiza.

Akifungua tamasha hilo, Babu alisema serikali imeongeza idadi ya wanawake katika nafasi za uamuzi na uongozi huku akitolea mfano wa mawaziri kuongezeka kutoka asilimia 21.7 hadi 36.

Pia alisema serikali imeongeza fursa ya wanafunzi waliokatisha masomo kwasababu mbalimbali ikiwamo ujauzito kuendelea na masomo na kutoa fursa za kuwawezesha wanawake na makundi yaliyoko pembezoni kiuchumi, huku Rais akiwa kinara katika Jukwaa la Kidunia la Kujenga Kizazi chenye Usawa.

"Nimejulishwa kuwa tamasha la mwaka huu limebeba ujumbe wa 'Haki ya Uchumi: Raslimali Ziwanufaishe Wananchi Walioko Pembezoni kwa Maisha Endelevu'. Ni mada muhimu kwa wakati huu nchi yetu imeingia uchumi wa kati ambao unahitaji ushiriki wa wanawake na wanaume,"alisema.

Babu alisema pamoja na wanawake zaidi ya asilimia 50 ya wananchi bado hawajaweza kushiriki kikamilifu kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo ukatili wa kijinsia, mila na desturi potofu, elimu duni, kutokumiliki raslimali za uzalishaji na kuelemewa na mzigo wa kazi za kuhudumia jamii na familia.


Naye Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP, Lilian Liundi, alisema Tanzania kuna raslimali nyingi na kwa muda mrefu TGNP na wadau wake wamekuwa wakiendesha kampeni za kitaifa kwamba nchi sio maskini ila inatakiwa kuangalia namna raslimali zinatumika kwa usawa kwa maendeleo endelevu na jumuishi.

Alizitaja raslimali hizo ni ardhi, maji, maliasili, madini na watu na kwamba kwa muda mrefu kiwango kikubwa cha bajeti kinaelekezwa kwenye miundombinu, teknolojia ya mawasiliano, madini na viwanda.

"Sekta hizi ni za muhimu sana katika kuchochea ukuaji wa uchumi. Hata hivyo sekta ya kilimo ambayo inaajiri zaidi ya asilimia 58 ya Watanzania ambapo kati yao asilimia 80 ni wanawake ambao ni wakulima wadogo ndio wamekuwa wakilisha nchi hii. Ukuaji wa sekta hii umekuwa kidogo sana asilimia 5.2 na kilimo kimekuwa kikichangia zaidi ya asilimia 28.2 ya pato la taifa," alisema.

Aidha, alipongeza serikali kwa bajeti ya kilimo kwa mwaka 2022/23 iliyoongezeka maradufu kutoka Sh. 294,162,071,000 hadi 751,123,280,000 ongezeko la 155.34 kulinganisha na 2021/22.

"Bajeti hii imeainisha kuwa wanawake, vijana na makundi mengine yatakuwa kipaumbele katika fursa zinazoletwa na ongezeko hilo. Tamasha hili litatupa fursa ya kujadili fursa zilizoko na mpya zinazojitokeza katika sekta ya kilimo na namna wanawake na makundi ya pembezoni wanavyoweza kuzitumia kwa ajili ya ustawi wa maisha yao," alisema Liundi.




Mmoja wa wateja wa Benki ya Afrika, Celestine Mwesigwa (kulia), akipata ufafanuzi wa jambo kwa Ofisa wa Bima wa benki hiyo, Mary Samwel, alipotembelea tawi la Posta, jijini Dar es Salaam jana, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tendo la ndoa ladaiwa chanzo migogoro kifamilia

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

TABIA ya baadhi ya wanandoa kunyimana tendo la ndoa ni miongoni mwa sababu zinazochochea migogoro baina yao, msongo wa mawazo na kushamiri kwa ukatili dhidi ya watoto.

Mkuu wa Kituo cha Polisi cha Muze, Sumbawanga mkoani Rukwa, Valentine James, alibainisha hayo jana wakati akizungumza na mwandishi wa habari.

Alisema, katika dawati la jinsia lililoko katika kituo hicho, kuna migogoro mingi iliyoripotiwa na wanandoa ambayo alisema chanzo chake ni kunyimana tendo la ndoa na imekuwa ikisababisha hasira baina yao.

Mkuu huyo wa kituo alisema madhara zaidi yanakuwa kwa watoto wa wanandoa hao kwa kuwa wamekuwa wakifanyiwa vitendo vya ukatili vikiwamo vipigo kutoka kwa wazazi kutokana na hasira walizo nazo.

"Mwanandoa anapokuwa na hasira na akashindwa kumwadhibu mwenzi wake, anahamishia hasira zake kwa watoto, hivyo wamekuwa wakipigwa na kuumizwa, chanzo chake ni hasira za mzazi kutokana na mgogoro wa ndoa pamoja na msongo wa mawazo," alisema.

Changamoto nyingine, alisema ni baadhi ya wanaume kuwa na tabia ya kuchukua mazao ya chakula nyumbani na kwenda kuyauza kisha kwenda kufanya starehe na wanawake wengine hali inayosababisha kuibuka migogoro katika familia zao.

James, aliziomba tasisi za kidini na mashirika ya kijamii yanayojihusisha na kutoa ushauri kwa wanandoa kufika katika Kata hiyo ili kutoa ushauri kwa kuwa kesi hizo zinazohusu ugomvi unaosababishwa kunyimana tendo la ndoa zimekuwa zikiongezeka siku hadi siku.

Mtaalamu wa saikolojia katika Kituo cha Afya Mazwi, Shangwe Braya, alisema wako baadhi ya wazazi ambao wakikosana hasira zao zinaishia kwa watoto kwa kuwapiga.

# Wadhibiti ubora vyakula, vipodozi wafundwa

**Na Joseph Mwendapole**

MAOFISA afya na biashara wameshauriwa kuhakikisha wanadhibiti ubora na usalama wa chakula na vipodozi kwa uadilifu, uaminifu na weledi mkubwa ili kulinda afya za watumiaji.

Ushauri huo ulitolewa jana na Katibu Tawala wa Mkoa wa Dar es Salaam, Rehema Madenge, wakati akifungua mafunzo ya maofisa afya na biashara wa halmashauri zote za Dar es Salaam.

Mafunzo hayo yalihusu sheria, kanuni na miongozo inayohusika na utekelezaji wa majukumu ya ushirikiano baina ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Alisema bidhaa za vipodozi na chakula zinagusa maisha ya watu kwani watu wote wanajipodoa bila kujali ni wanawake au wanaume.

"Na watu wote tunakula chakula kwa hiyo chakula na vipodozi hivyo vinatakiwa viwe na viwango sahihi," alisema Madenge.

Aliwataka washiriki wa mafunzo hayo watambue kwamba azma ya serikali ni kuhakikisha inakuwa na mtandao mkubwa unaoshughulikia shughuli za udhibiti wa ubora na usalama wa chakula na vipodozi.

"Kwa kulitekeleza hili Serikali imeamua kuwatumia wakaguzi walio chini ya ofisi ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika shughuli za udhibiti wa bidhaa husika ili kulinda afya za watumiaji katika maeneo yao," alisema.

"Kazi hii mnatakiwa kuifanya kwa uadilifu, uaminifu na weledi mkubwa kwani tunawaona watu wanaotumia vipodozi ambavyo havina viwango na madhara yake kwa hiyo tuifanye kazi hii tukiwa na hofu kubwa vinginevyo tunaenda kuumiza watu wetu," aliongeza.

Aidha, alisema endapo watafanyakazi zao kwa uadilifu, weledi na uaminifu mkubwa watasaidia kuhakikisha shughuli za udhibiti zinafanyika kwa haraka na ufanisi zaidi.

Aliwataka washiriki wafahamu kuwa sheria, kanuni na mwongozo vimepitia mchakato wote unaotakiwa na vimepata baraka kutoka TAMISEMI na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara.

"Hivyo watumishi mna wajibu wa kuelewa na kutekeleza makubaliano yaliyoainishwa kwenye sheria, kanuni na miongozo husika ninaamini kuwa mafunzo haya ni njia muafaka ya kuleta tija zaidi katika juhudi za kuleta maendeleo katika udhibiti wa bidhaa za chakula na vipodozi katika mkoa wetu," alisema.

# Mabadiliko tabianchi yahusishwa na ukatili

**Na Christina Haule**

MABADILIKO ya tabianchi yametajwa kuwa ni moja ya sababu za kuendelea kwa vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa jamii licha ya kuwapo kwa makatazo na maelekezo mbalimbali yanayoendelea kutolewa na serikali na asasi za kiraia nchini.

Mratibu wa Mradi wa Kuleta Mabadiliko kwa Wanawake Vijijini (RWCC), Catherine Kasimbazi, alisema jana kuwa katika utafiti mbalimbali waliofanya kwenye mikoa inayotekeleza mradi huo, wamebaini kuwapo kwa changamoto ambazo pia bado zipo katika mikoa mingi ya Tanzania zinazoashiria ukatili wa kijinsia.

Miongoni mwa changamoto hizo, alisema ni mabadiliko ya tabianchi ambapo ukosefu wa mvua umeleta njaa inayosababisha kuwapo kwa biashara ya ngono kwa wanawake ili kupata fedha za kusaidia familia zao.

Aliitaja changamoto nyingine inayosababishwa na mabadiliko ya tabianchi kuwa ni ukatili wa kingono unaosababishwa na kuibuka kwa kasi masuala ya ndoa na mimba za utotoni kutokana na wazazi kuchukua hatua za kuwaozesha mabinti wakiwa katika umri mdogo ili wapate pesa za kujikimu.

Kasimbazi pia alisema, tatizo la ukosefu wa maji linasababisha kutokea kwa vitendo vya ukatili wa kingono kwa wanawake na watoto baada ya kutembea umbali mrefu kutafuta maji na pengine kufikia hatua ya kubakwa au kulawitiwa sambamba na kuwapo kwa migogoro ndani ya ndoa na pengine ndoa kuvunjika.

Pia alisema, bado tatizo la mfumo dume linaendelea kushika kasi kwa wanaume kujiona ndio wenye nguvu na uwezo katika uamuzi na uongozi kwa kutumia mali ikiwamo kuuza mazao na kutumia pesa kwa manufaa yao bila ya kuwashirikisha wanawake waliolima nao mashamba.

# Mifumo yaandaliwa kuzuia migogoro ardhi

**Na Romana Mallya**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Allan Kijazi, amesema mifumo inaandaliwa kuzuia migogoro ya ardhi hatua ambayo itaifanya wizara hiyo kuondokana na dhana kwamba ipo kwa ajili ya kutatua migogoro ya ardhi.

Dk. Kijazi aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari, kuhusu utatuzi wa migogoro ya ardhi unaofanywa na kamati maalum, ambayo kwa sasa iko jijini Dodoma.

Alipoulizwa kuhusu kuendelea kuwapo kwa migogoro ilhali kuna timu ya mawaziri wanane wa kisekta walizunguka nchi nzima, Dk. Kijazi alikiri migogoro ni mingi na iliyoshughulikiwa au kutolewa uamuzi na Baraza la Mawaziri ni ya vijiji 975 kati ya 16,000 vilivyoko.

"Hii ni sehemu ndogo ya migogoro ambayo imetolewa uamuzi, bado ipo ambayo ilikuwa haijafanyiwa kazi na mingine imeendelea kuibuka siku hadi siku.

"Suala la kushughulikia migogoro, siyo suala ambalo unaweza kulimaliza kwa siku moja, ndiyo maana tumeanzisha mkakati, pamoja na mawaziri wa kisekta, (wizara) tunaizungukia mikoa yote mikubwa kuitatua," alisema.

Dk. Kijazi alisema pamoja na hatua hiyo, hawawezi kuendelea kuwa serikali au wizara ya kutatua migogoro, ni lazima wajenge mifumo ya kuhakikisha haiwi mingi kama ilivyojitokeza.

Alisema wizara inaandaa mifumo ya kutafuta sababu za migogoro hiyo kuibuka, na kuweka mifumo ya kuizuia ili isiibuke, wakati wakiipunguza iliyopo.

Alisema kamati ya utatuzi wa migogoro iliyoko jijini Dodoma, ilipewa siku tano ya kuwasikiliza wananchi kuanzia Septemba 26, mwaka huu, lakini wizara imelazimika kutenga siku nyingine tatu zaidi baada ya watu kuendelea kujitokeza.

Alisema katika siku tatu zilizoongezwa, eneo la Kizota, Nkuhungu na Nala usikilizaji wa wananchi utakuwa Oktoba 17, mwaka huu, Mnadani na Miyuji siku itakayofuata na Oktoba 19, mwaka huu, wananchi wa Mtumba, Chahwa na Ibara nao watasikilizwa.

Alisema baada ya kamati hiyo kumaliza, itarejea Dar es Salaam kuwasikiliza wale ambao hawakufikiwa wakati wa awamu ya kwanza, ndipo mikoa mingine itafuata.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Exim, Jaffari Matundu (kulia), akiwaongoza maofisa waandamizi wa benki hiyo, kusafisha magari ya wateja waliofika kupata huduma kwenye tawi la makao makuu ya Exim, jijini Dar es Salaam jana, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja. Kushoto ni mmoja wa wateja wa benki hiyo kutoka Kampuni ya Vin Mart, Rashmit Lathigara. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wafanyakazi Exim waosha magari ya wateja

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Exim Tanzania, imeungana na watoa huduma duniani kote kusherehekea Wiki ya Huduma kwa Wateja huku ikiahidi kuendelea kuwa karibu zaidi na wateja wake kupitia huduma zenye ubunifu zaidi kwenye soko la huduma za kifedha.

Katika kuthibitisha kauli hiyo maofisa waandamizi wa benki hiyo, wakiongozwa na Ofisa Mtendaji Mkuu, Jaffari Matundu, jana walishuhudiwa wakiwaongoza wafanyakazi wengine kufanya matukio mbalimbali kwa ajili ya wateja ikiwamo kusafisha magari ya wateja waliofika kupata huduma kwenye tawi la makao makuu, jijini Dar es Salaam.

Akitoa salamu za heri kwa wateja na wafanyakazi wa benki hiyo, Matundu alisema pamoja na jitihada za benki hiyo kuvutia wateja wapya kupitia huduma mbalimbali za kisasa zinazoendana na mahitaji ya wateja hao, benki hiyo pia imekuwa ikiweka msisitizo mkubwa katika kuwahudumia wateja.

"Wiki ya Huduma kwa Wateja imetoa tena nafasi nzuri kwa benki kusherehekea jukumu muhimu ambalo tumekuwa tukilifanya kila siku, yaani kuwahudumia wateja wetu na kuonyesha umuhimu wa ushirikiano baina yetu kama uongozi, wafanyakazi pamoja na wateja wetu," alisema.

Ofisa Mkuu Idara ya Fedha, Shani Kinswaga, aliwapongeza wafanyakazi wote wa benki hiyo akisema utoaji bora wa huduma ni kiungo muhimu katika kuhakikisha wateja wanaridhika huku akiwataja wafanyakazi hao kama mashujaa muhimu ambao wamekuwa wakihakikisha wateja wanaridhika kupitia huduma bora wanazozitoa.

"Zaidi pia ningependa tuendelee kuzingatia na kujitolea katika kutoa huduma bora kwa wateja wetu ambao wameendelea kuwa waaminifu kwetu pia." alisema Kinswaga wakati akihimiza timu ya wafanyakazi hao kujisikia fahari kwa michango yao.

Katika maadhimisho hayo, mbali na uoshaji wa magari ya wateja, maofisa waandamizi wa benki hiyo waliwahudumia kifungua kinywa wateja mbalimbali waliofika kwenye baadhi ya matawi ya benki sambamba na kujadili pamoja maswala muhimu ikiwamo namna uboreshaji wa huduma za benki pamoja na kujadili fursa zinazopatikana kupitia ukuaji wa biashara.

Akisisitiza kuwa kila siku ni siku ya huduma kwa wateja katika benki hiyo, Mkuu wa Idara ya Huduma kwa Wateja, Frank Matoro, alisema benki imeendelea kujitolea kutoa kiwango cha huduma zenye ubora wa hali ya juu kwa wateja wake na wadau bila kujali hali zao au wapi walipo kote nchini.

"Kama sehemu ya hatua za kurejesha fadhila na uaminifu wa wateja wetu, wiki hii yote tumekuwa na shughuli kadhaa za kipekee na maalum kuonyesha namna tunavyowathamini wateja. Baadhi ya shughuli ni pamoja na kutembelea wateja kwa kushtukiza na kuwazawadia kama njia ya kuwashukuru kwa kuwa waaminifu kwetu," alisema.

Wakizungumzia mapokezi hayo pamoja huduma za benki hiyo, baadhi ya wateja, Hamisi Kozzy kutoka Kampuni ya Business Index, pamoja na Rashmit Lathigara kutoka kampuni ya Vin Mart, walipongeza benki hiyo kwa huduma za kisasa na zinazoendana na mahitaji yao.

"Kuridhika kwetu na huduma zinazotolewa na Benki ya Exim ndiko kunatufanya tuendelee kupata huduma zetu kupitia benki hii. Ni matumaini yetu kwamba ari hii haitapungua na tuko tayari kupokea mambo mazuri zaidi kutoka kwao," alisema Kozzy.

# Chuo uhasibu chatakiwa kuongeza ubunifu

**Na Mwandishi Wetu**, ARUSHA

CHUO cha Uhasibu Arusha (IAA) kimetakiwa kuongeza ubunifu katika utendaji kazi ili kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani yatakayokiwezesha kujiendesha kikamilifu.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Jenifa Omolo, alitoa maagizo hayo juzi wakati wa ziara yake katika chuo hicho. Omolo alitembelea miradi inayotekelezwa pamoja na kuzungumza na menejimenti ya chuo jijini hapa.

Omolo alisema, kuongeza ubunifu kutawezesha mapato ya ndani kuongezeka kwa kuwa changamoto zinapojitokeza zitatatuliwa kwa ushirikiano na kuibua mbinu mpya za kuongeza mapato.

"Kwenye kujiendesha lazima tuwe na timu ambayo inatengeneza ubunifu, ikiwa tumekupa chuo kwa miaka mitano unapotoka unatuachia nini, hakuna mtu mwingine atakuja kukutengenezea lakini ili mfanye vizuri lazima kuimarisha utawala bora," alisema Omolo.

Alisisitiza kuwa ili kufanikiwa katika kuongeza mapato, lazima chuo kijenge jina na kuongeza sifa kwa kuhakikisha kinazingatia ubora wa elimu inayotolewa ili kuvutia wanafunzi wengi zaidi na kuwa na wahitimu watakaoshindana katika soko la ajira kitaifa na kimataifa.

Omolo pia, aliitaka menejimenti ya chuo kuimarisha ushirikiano katika taasisi hiyo na kuhakikisha kuwa utekelezaji wa miradi mbalimbali chuoni hapo unafanyika kwa ushirikiano na kutafuta mbinu za kutatua changamoto zinapojitokeza mapema kwa pamoja.

Alisema ameridhishwa na miradi ya ujenzi inayotekelezwa chuoni hapo na kuwasisitiza kila mmoja kuwa na taarifa za miradi hiyo ili kuwa na uelewa wa pamoja na kuhakikisha kuwa Taasisi inaweza kuendelea na shughuli zake bila kukwama.

Omolo aliongeza kuwa Wizara ya Fedha na Mipango itaendelea kushirikiana na chuo hicho ili kufanikisha malengo na mipango ya muda mrefu kwa kukiwezesha kifedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya kuendeleza chuo.

Kaimu Mkuu wa Chuo hicho, Dk. Cairo Mwaitete, aliishukuru Wizara ya Fedha na Mipango kwa ushirikiano na kukiwezesha chuo katika kutimiza majukumu yake pamoja na kukipatia ruzuku ya Sh. bilioni tatu kwa ajili ya ujenzi wa jengo la utawala, Kampasi ya Babati na kutoa kibali cha kukopa Sh. bilioni nane, kwa ajili ya ujenzi wa hosteli.

Kuhusu mafanikio ya Chuo, Dk. Mwaitete alisema kuwa chuo kimeboresha uwezo wake wa kukusanya mapato yake ya ndani kutoka kiasi cha zaidi ya Sh. bilioni 6.4 kwa mwaka 2019/20 hadi kufikia Sh. bilioni 15.65 kwa mwaka wa fedha 2021/22.

"Chuo kimefanya jitihada za kujitangaza na kufanikisha kuongezeka kwa wanafunzi kwa miaka mitatu mfululizo kutoka wanafunzi 4,769 ambapo kufikia June, mwaka huu, chuo kilikuwa na wanafunzi 10,342 na matarajio kwa mwaka wa masomo 2022/23 ni kufikia zaidi ya wanafunzi 12,080", alisema.



Mkurugenzi Mtendaji wa Tigo Tanzania, Kamal Okba, akipokea simu na kuhudumia wateja katika kituo cha huduma kwa wateja cha kampuni hiyo, Morroco, Dar es Salaam jana, ikiwa ni mwendelezo wa wiki ya huduma kwa wateja 2022.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NIC yazindua mkataba huduma kwa mteja

**Na Frank Monyo**

SHIRIKA la Bima la Taifa (NIC) limezindua Mkataba wa Huduma kwa Mteja wakati wa Maadhimisho ya Kimataifa ya Wiki ya Huduma kwa Wateja kwa lengo la kutoa huduma bora na zenye viwango.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mkataba huo juzi jijini Dar es Salaam, , Msajili wa Hazina, Mgonya Benedicto, aliwataka watumishi wa NIC kufuata ahadi iliyowekwa kwenye mkataba huo na asiwapo yeyote wa kutenda kinyume kwa kuwa atachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria na miongozo ya utumishi wa umma.

Benedicto alisema NIC ni shirika linalofanya vizuri ikiwamo kupata faida mara nne mfululizo na kutoa gawio kwa serikali kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi.

Alisema madhumuni ya mkataba huo ni kuwafahamisha wadau juu ya upatikanaji wa viwango vya ubora wa huduma zitolewazo na NIC, kujenga utamaduni wa kuwafanya watumishi kuwa na mtazamo wa kuwajali na kuwahudumia wateja kwa viwango bora, kuongeza uwajibikaji wa watumishi katika kuwahudumia wateja kwa weledi.

"NIC imekuwa ikifanya vizuri sambamba na kupata faida mara nne mfululizo pamoja na kutoa gawio kwa serikali, mkataba huu utasaidia kuleta mafanikio zaidi katika huduma.

Mkataba huo unaweka wazi mfumo wa upokeaji wa maoni na malalamiko na kurudisha mrejesho kwa wateja baada ya kufanyiwa kazi." alisema.

Pia alisema watumishi wanatakiwa kufuata ahadi iliyowekwa kwenye mkataba huo na asiwepo mtumishi yeyote wa kutenda kinyume na mkataba huo kwani atachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria na miongozo ya utumishi wa umma na watakaofanya vizuri watapongezwa.

Alisema mkataba huo una lengo la kuboresha uhusiano baina ya shirika na wateja wake lakini pia ukikusudia kuongeza uelewa kuhusu aina na ubora wa huduma zinazotolewa, haki na wajibu wa mteja na jinsi anavyoweza kuwasiliana.

"Mkataba wa huduma kwa mteja ni makubaliano kati yenu watoa huduma na mteja wenu ikiwa ni ahadi ya kutoa huduma bora kwa mteja," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa NIC, Dk. Elirehema Doriye, alisema shirika hilo limekuwa likifanya mabadiliko kwenye kuwahudumia wateja ambapo wamekuwa wakiboresha huduma ili kuendana na ushindani ulioko sokoni jambo lililowavutia wateja kununua bidhaa zao za Bima na kuwafanya kuwa na ukuaji wa faida ya zaidi ya asilimia 100 katika miaka minne mfululizo.

"Moja ya misingi inayotuongoza NIC yetu ni kutambua kuwa siku zote "Mteja Kwanza" yaani "Customer first" hii inamaanisha kwamba mteja kwetu ni kipaumbele namba moja katika utoaji huduma," alisema Dk. Doriye.

Alisema katika kuadhimisha wiki ya mteja na kutambua umuhimu wa wateja, shirika limezindua Mkataba wa Huduma kwa Mteja "ikiwa ni ahadi yao kwa wateja kuwa tutawapatia huduma inayostahili kulingana na ahadi waliyoitoa.

Aliongeza kuwa katika wiki ya huduma kwa wateja wanakwenda kutoa mafunzo kwa wafanyakazi kwa kwenda kutoa huduma kwa wateja kwa viwango ambavyo vimeainishwa katika mkataba huo katika kujenga picha ya kile ambacho serikali inataka kwenda kasi ile ya kazi iendelee.

# Watumishi vishoka wa NSSF waonywa

**Na Joctan Ngelly**, GEITA

MENEJA wa Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) Mkoa wa Geita, Winniel Lussingu, amewaonya watu wanaojifanya wanyakazi wa taasisi hiyo na kupokea rushwa kwa wateja kwa madai ya kuwapatia huduma.

Ameonya kwamba, watu hao pindi watakapobainika, watachukuliwa hatua za kisheria ikiwamo kufikishwa mahakamani.

Lussingu alitoa onyo hilo jana wakati akizungumza na wajasiriamali kwenye ukumbi wa Nyerere ulioko Bombambili, mkoani hapa.

"NSSF ni taasisi ya umma, hivyo tunapinga vikali matendo yote ya rushwa na tunashirikana na serikali kwa karibu ili kuhakikisha huduma zetu zote zinatolewa kwa wakati zikiwa bora lakini bila gharama yoyote.

NSSF, tumekuwa tukihakikisha wanachama wetu wanapata huduma zetu bure, hivyo basi nitoe rai kama unakutana na mtu yeyote akakwambia utoe kiasi chochote ili kupata huduma NSSF, huyo ni kishoka si mtumishi wa NSSF," alisema.

Aidha, alisema kuna wateja wengi wameshalalamika kuhusu vishoka na wameshachukua hatua kwa sababu ndani ya NSSF kimeanzishwa kitengo cha usalama wa ndani ambacho kinashirikiana na vyombo vya dola ili kukomesha vishoka wanaojifanya watumishi wa NSSF.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Geita, Prof. Godius Kahyarara, alizitaka taasisi za serikali, ikiwamo NSSF kwasaidia wajasiriamali mkoani hapa ili kuimarisha sekta ya kilimo.

Naye Meneja wa Sekta Isiyo Rasmi, Rehema Chuma, aliwataka wajasiriliamari na wachimbaji wadogo wa madini kujiunga na NSSF ili kuhakikisha wanapokuwa kuwa wazee waendelee kusaidiwa.

Chuma alisema kila mjasiriamali akitaka kujiunga lazima tujuwe kazi yake au biashara yake kabla ya kujiunga na kianzio cha kuwa mwanachama ni Sh 20,000 kwa kila mwezi.

Pia alisema, mjasiriamali akitaka kuongeza zaidi ya Sh. 20,000 kwa mwezi ni vizuri kwa sababu kadri anapoweka fedha nyingi ndipo anapata mafao mengi.

# Wavuvi Nyumba ya Mungu waitwa kuanzisha ushirika

**Na Anjela Mhando,** MWANGA

WAVUVI kutoka vijiji 18 wanaotegemea kipato kutokana na kuendesha shughuli za uvuvi katika Bwawa la Nyumba ya Mungu, wameitwa kuanzisha vyama vya ushirika vya msingi vya wavuvi ili wanufaike na mitaji na dhana za uvuvi.

Mkuu wa Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, Abbas Kayanda, aliwaita wavuvi hao juzi kwa ajili ya kuunda vyama hivyo, wakati wa kikao cha ujirani mwema kilichowakutanisha wakuu wa wilaya tatu zinazozunguka bwawa hilo.

Bwawa hilo lililoko kati ya mikoa ya Kilimanjaro na Manyara, limetengeneza ajira za uvuvi kwa wananchi wa Wilaya ya Mwanga, Simanjiro na Moshi.

Alisema; "Serikali inaviwezesha vyama vya ushirika kwa kuvipatia elimu, dhana na vifaa bora vya uvuvi kama vile injini za boti, pamoja na kuviunganisha na taasisi za fedha ili kupata mikopo yenye riba na masharti nafuu, kwa lengo la kufanya shughuli zenu kwa tija.

Aliongeza: "Tutaendelea kuwa mstari wa mbele kuhamasisha wavuvi masuala mbalimbali ya kimaendeleo, hivyo na leo hii nichukue fursa hii kutoa rai kuwa ndani ya miezi mitatu, muwe mshajiunga na vyama vya ushirika au mjiunge na kuanzisha ushirika mpya kwa ajili ya manufaa yenu ya baadaye."

Kayanda, alisisitiza kuwa serikali kupitia mamlaka zake tofauti ina fursa nyingi ambazo inaweza kuzitoa kwa wanaushirika waliojiunga kwenye vikundi, ikiwamo mikopo kupitia halmashauri.

Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Dk. Suleiman Serera, alisema serikali italifunga bwawa hilo kwa muda miezi mitatu ili kutoa nafasi kwa samaki kuzaliana na kukua.

Alisema: "Serikali inao wajibu wa kuhakikisha Bwawa la Nyumba ya Mungu, linatumika kwa ajili ya matumizi yaliyokusudiwa wakati wote, hivyo kufungwa kwa bwawa hilo ni kutoa fursa ya samaki waweze kuzaliana na kuwa wakubwa ili waweze kukidhi mahitaji halisi ya walaji".

Katibu Tawala Msaidizi anayeshughulikia Uchumi na Uzalishaji katika Sekretarieti ya Mkoa wa Kilimanjaro, Vedasto Makota, alisema kujiunga na ushirika ni suala la msingi ambalo wavuvi kutoka maeneo hayo hawana budi kulizingatia.

Alisema: "Wakizingatia wazo la kujiunga au kuanzisha ushirika miongoni mwao, watanufaika na juhudi zinazofanywa na serikali ikiwamo kupata mikopo kwa ajili ya vifaa vya kufanyia shughuli zao kama vile boti za kuvulia samaki, vifaa vya usalama wawapo kazini na nyavu bora kwa ajili ya shughuli zao," alisema.

Aidha, alisema kuwa jumla ya wavuvi 194,000 nchini wamejiunga kwenye vyama mbalimbali vya ushirika kama ilivyoshauriwa na serikali na kwamba tayari wananufaika na fursa zinazohusiana na shughuli zao za uvuvi.

# TGS yatakiwa kuwaondoa makanjanja sekta ya miamba

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SERIKALI imeagiza Jumuiya ya Wanajiolojia nchini (TGS) kuondoa watu wasio na taaluma kwenye sekta hiyo ili kuleta heshima na nidhamu inayotakiwa.

Waziri wa Madini, Dk. Doto Biteko, alitoa agizo hilo wakati wa ufunguzi wa mkutano mkuu wa mwaka wa TGS.

Dk.Biteko alisema lazima taaluma hiyo iheshimike na watu wote kwa sababu ni muhimu kwa sekta ya madini. Katika mkutano huo, Biteko, alimwakilisha Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango.

Pamoja na mambo mengine, alisema serikali ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha usajili wa Bodi ya Wanajiolojia nchini.

Dk. Biteko alisema hakuna faida yoyote ya kuendelea kuwa na watu hao wanapotumia ujanja kwenye kazi zao za utafiti, badala ya kuweka uzalendo mbele.

Alisema chochote wanachokifanya kibaya kinapeleka taswira mbaya nje ya nchi, hivyo kama nchi hawezi kuendelea kuacha watu hao.

**Wizara ya Madini, inafuatilia taratibu za ukamilishaji wa mchakato wa kuundwa kwa bodi hiyo, ili sekta za nishati, madini, maji na zingine mnazohusiana nazo ziweze kusimamiwa kwa weledi kwa manufaa ya nchi.**

Dk. Biteko alisema: "Jiolojia ni sayansi ya dunia ambayo inagusa kila nyanja za maisha ya mwanadamu. Natambua mnajifunza kuhusu miamba, ambayo elimu hiyo inatoa fursa mbalimbali.

Aliongeza: "Mfano, tunaendesha kilimo kutokana na uwapo wa udongo ambao asili yake ni miamba, tunakunywa maji yatokayo ardhini kwenye mifumo ya miamba, tunatumia metali mbalimbali katika viwanda vyetu vya uzalishaji,metali hizi zinazotokana na madini yaliyomo kwenye miamba,

"Pamoja na hayo yote, baadhi ya vyanzo vya nishati vinavyotumika vinahusiana moja kwa moja na jiolojia; mfano, joto ardhi, mafuta na gesi asilia, makaa ya mawe na madini ya urani (uranium)."

Alisema ukiacha kilimo, rasilimali zilizoko kwenye miamba ikiwamo madini, vito, mafuta na gesi asilia ndizo zenye mchango mkubwa katika

Kuhusu uanzishwaji wa Bodi ya Usajili wa wanajiosayansi alisema serikali imeanza mchakato wa kutengeneza chombo hicho, ili kuondoa tatizo la uwapo wa watu wasio waadilifu na weledi kwenye sekta ya madini.

Alisema Wizara ya Madini, inafuatilia taratibu za ukamilishaji wa mchakato wa kuundwa kwa bodi hiyo, ili sekta za nishati, madini, maji na zingine mnazohusiana nazo ziweze kusimamiwa kwa weledi kwa manufaa ya nchi.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini, Msafiri Mbibo, alisema kada hiyo inahitaji nidhamu hasa katika eneo la utafiti na kuwa wao kama serikali wapo tayari kushirikiana na wadau wengine katika kutunza nidhamu.

Alisema nidhamu ni muhimu na ili taifa liweze kunufaika na kupiga hatua za maendeleo ni lazima wasimamie nidhamu.

Rais wa TGS, Prof. Abdulkarim Mruma, alisema Tanzania ina rasilimali nyingi na katika mkutano huo wataalamu hao watajadiliana mada mbalimbali kwa lengo la kujenga jumuiya hiyo.



Ofisa Mwezeshaji wa Shirika la Oikos East Africa, Rebeka Mguruta (kulia), akionyesha picha za nyayo na wanyama walao nyama, katika somo la kupunguza migogoro ya wanyama na wafugaji kwa wanafunzi wa Sekondari ya Lekule, Kata ya Gilai Lumbwa, wilayani Longido, mkoani Arusha hivi karibuni. Somo hilo, linaendelea kwenye shule sita za Kata ya Ketumbeine. Wa tatu kushoto ni Mwalimu wa Mazingira, George Kimaro. **PICHA: DANIEL SABUNI**

# Idadi wanaougua magonjwa ya akili mkoani Manyara yapungua

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

IDADI ya watu wanaougua magonjwa ya akili katika Mkoa wa Manyara, imeshuka, baada ya Hospitali ya Rufani ya Mkoa huo, kueleza kwamba kwa sasa inapokea wagonjwa wawili hadi watatu kwa mwaka.

Kwa mujibu wa Mtaalamu wa Afya ya Uzazi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara, Dk. Babu Meng'oriki, kiwango hicho ni kidogo kwa mkoa huo, ukilinganisha na miaka ya nyuma.

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), katika muongo mmoja uliopita, kumekuwa na ongezeko la watu kwa asilimia 13, kwamba watu bilioni moja wanaishi na tatizo hilo duniani.

"Lakini tukizungumzia tatizo hilo kwa mjamzito, hutokea baada ya saa 48 mpaka wiki mbili au wiki 12, baada ya kujifungua.

Alisema chanzo cha ugonjwa huo ni kichocheo kutoka ndani ya ujauzito na wengine kurithi tatizo hilo.

Alizitaja dalili kuwa ni kuongea vitu ambavyo havipo, mama kukataa kumnyonyesha mtoto na wakati mwingine kuvua nguo.

Pia aliyataja madhara ambayo anaweza kuyapata mtoto kuwa ni mama kumtupa mtoto, mtoto kukosa malezi ya mama, hasa joto la mama na mtoto kukosa maziwa ya mama, kwa kuwa wapo ndugu wanaomnyang'anya mtoto akipatwa na tatizo hilo.

# MEMKWA yawavutia walengwa kurudi shuleni

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

MPANGO wa Elimu ya Msingi kwa Walioikosa (MEMKWA), kutoa fursa kwa wanafunzi wanaogunduliwa kuwa na uwezo mkubwa wa akili kuvushwa darasa, unatajwa kuwavutia walengwa wengi wa mpango huo, kujiunga na madarasa yaliyotengwa na serikali.

Mkuu wa Divisheni ya Elimu ya Awali na Msingi wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Hussein Kitingi, alisema sera ya elimu inaruhusu mwalimu wa shule husika, endapo atamuona mwanafunzi wa MEMKWA ana uwezo huo, anaweza kumrusha na kumwandikisha darasa la tano, la sita au akamsajili moja kwa moja kufanya mtihani wa darasa la saba.

Kitingi, aliweka wazi suala hilo la kuvushwa ngazi kwa wanafunzi wa MEMKWA, alipokuwa akizungumza na wananchi wa kata za Weruweru na Mnadani, wakati wa maadhimisho ya wiki ya elimu ya watu wazima.

**Nitoe wito, niwakumbushe wazazi wao kwamba MEMKWA ni wa bure na watoto wanaokusudiwa ni kaunzia miaka 10 hadi miaka 13.**

"MEMKWA ni sawa na gari la mwisho, linabeba watu wote na hiyo ni fursa iliyotolewa na serikali. Kwa hiyo sasa hivi ninavyozungumza MEMKWA kwa takwimu hizo zilizotolewa hapa, maana yake ni kwamba bado tuna wanafunzi wengi wako mtaani.

"Nitoe wito, niwakumbushe wazazi wao kwamba MEMKWA ni wa bure na watoto wanaokusudiwa ni kaunzia miaka 10 hadi miaka 13.

"Sio lazima akiwa na umri huo akawa kwenye darasa la kwanza hadi la nne, lakini mwalimu wake, akimwona ana uwezo anaweza akamrusha akamwandikisha darasa la tano, la sita au akamsajili moja kwa moja kufanya mtihani wa darasa la saba, ilimradi tu awe hajawahi kufanya mtihani wa darasa la saba."

Kwa mujibu wa Kitingi, sababu kubwa za kuwapo watoto wengi mkoani Kilimanjaro, waliokosa elimu ya msingi ni baadhi ya wazazi kuacha familia na kwenda kutafuta maisha miji na mikoa mingine.

"Ukiangalia sababu za kiuchumi, Mkoa wa Kilimanjaro unaingia moja kwa moja. Kwa sababu ziko jamii, siyo kwa nia mbaya ila ni kwa sababu ya kutafuta maisha, bahati mbaya wazazi wao wamelazimika kuachana na familia na kwenda nje ya makazi yao ili kutafuta maisha."

Ofisa Elimu ya Watu Wazima wa Wilaya ya Hai, Immaculatha Mgaza, alisema wilaya hiyo ina vituo 12 vya kutolea elimu hiyo na hadi kufikia sasa wamesoma watu 734 wanaojihusisha na shughuli mbalimbali za kiuchumi.

Alisema: "Pia tuna vituo 15 vinavyotoa elimu ya msingi nje ya mfumo rasmi, yaani mpango wa elimu ya msingi kwa walioikosa. Aidha, kuhusu elimu nje ya mfumo rasmi tunayo sekondari ambayo tunafundisha kwa muda wa miaka miwili".




Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda (wa pili kushoto), akipewa maelezo ya kitaalamu kutoka kwa Ofisa Ugani wa Kampuni ya Maua Mazuri Tissue Culture Ltd ya mjini Moshi, kabla ya kufungua mafunzo ya uzalishaji wa zao la ndizi yaliyoratibiwa na Shirika la Tanzania Horticultural Association (TAHA), katika kata ya Mamsera, wilayani Rombo, mkoani Kilimanjaro juzi. **PICHA: JAMES LANKA**

# Wanafunzi 3,333 waliopata ujauzito warejeshwa shuleni

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

SERIKALI imesema hadi sasa wasichana 3,333 ambao walikatisha masomo kutokana na kupata ujauzito wakiwa shuleni wamerejeshwa na wanaendelea na masomo.

Mkurugenzi Msaidizi wa Mafunzo ya Ualimu kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Huruma Mageni, alitoa takwimu hiyo jana, wakati wa uzinduzi wa mwongozo wa utekelezaji wa Programu ya Elimu ya Sekondari, kwa njia mbadala.

Alisema wasichana hao wanaendelea na masomo, baada ya kusajiliwa kupitia mradi wa utoaji wa elimu kwa njia mbadala.

Mgeni alisema kuwa kupitia mpango huo, jumla ya vituo 131 vyenye walimu 803 vilivyoko kwenye mikoa 26 nchini, vimepokea wanafunzi hao ambao wanaendelea na masomo ya sekondari.

Alisema kuwa mradi huo ambao unatekelezwa na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, umekuja na mwongozo wa namna bora ya utoaji wa elimu kwa wasichana, nje ya mfumo usio rasmi.

"Mwongozo huu iwapo utafuatwa kwa ukamilifu, utasaidia kutatua kero mbalimbali zilizokuwapo katika uendeshaji wa programu ya elimu, kwa njia mbadala," alisema Mageni.

Awali, Mkurugenzi wa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, Dk. Michael Ng'umbi, alisema mwongozo huo umekuja kufufua matumaini mapya kwa mtoto wa kike, ambaye alikosa fursa ya elimu.

Alisema pamoja na mambo mengine, mwongozo huo umejumuisha kongani za elimu huria ili kumwezesha mtoto wa kike kupata elimu sawa sawa na yule ambaye yupo katika mfumo rasmi.

# Tanga yaporomoka viwango utoaji chanjo corona

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

MKOA wa Tanga unatajwa kufanya vibaya katika kampeni ya kitaifa ya utoaji wa chanjo ya UVIKO-19, baada ya kuporomoka kutoka mikoa 10 iliyokuwa na alama za juu na kushika mkia.

Jana, Mkuu wa Mkoa huo, Omary Mgumba, alieleza kushangazwa kwake na kushuka kwa hamasa ya chanjo hiyo, alipokuwa akifungua kikao kazi cha viongozi wa wilaya za Tanga waliokutana kufanya tathmini.

"Inaleta mshtuko kwa kweli, kwa kuwa awali ilikuwa ikishika nafasi za juu katika 10 bora kwa mikoa yote nchini, kwenye uchanjaji wa UVIKO-19.

"Kama ingekuwa hivi tangu hapo awali, serikali na viongozi tusingeshangaa. Tunashangaa kwa sababu tulikuwa kwenye nafasi za juu, lakini leo tumekuwa wa mwisho kwenye alama nyekundu."

Aidha, Mgumba, alieleza kuwa sababu za kushika nafasi hiyo mbaya ni kutokana na watendaji wanaotakiwa kuhamasisha, kushindwa kufanya kazi zao ipasavyo.

"Baada ya kufuatilia sababu imeonekana hakuna posho, hivyo watendaji wote wenye wajibu wa kusimamia jukumu hilo la kuhamasisha na kutekeleza mikakati tuliyokubaliana ya nyumba kwa nyumba, wao wamebaki majumbani na ofisini kwao," alifafanua.

Mgumba alisema katika sekta ya afya kuna tatizo la lishe kwa watoto, kutokana na kuwapo kwa kiwango kikubwa cha hali ya udumavu, ukondefu na viribatumbo.

Kutokana na jambo hilo, Mkuu huyo wa Mkoa, aliwaagiza viongozi wanaohusika na masuala ya lishe kutekeleza wajibu wao kupitia mkataba wa afya ya lishe kwa watoto, ili kupunguza na kuondoka kabisa hali hizo na kujenga watoto wenye afya ambao na Taifa bora kwa ujumla.

ama
ALHAMISI OKTOBA 6, 2022
AFYA NA MAZINGIRA



## Unajua mikataba lishe? Pata tathmini vita udumavu inavyowajibisha watendaji

Ukurasa 14



## MGOGORO WANAKIJIJI KATAVI VS TAWA

## Busara za RC Mrindoko kukutanisha wanaosuguana zatuliza moto, kila upande 'watapika nyongo' zake

Ukurasa 16

### KILA AJALI 20 HAWAKOSEKANI WALAU MMOJA...

# Kampeni usalama barabarani ikishirikisha walengwa, wahusika muhimu wanafunzi

**Na Halfani Chusi**

LINAPOTAMKWA suala la ajali barabarani, kuna marejeo ya kitakwimu, kwamba katika wastani wa kila watu 20, ni vigumu kumkosa mwanafunzi, hata kugeuka

Tatizo sugu lionaloshika utashi wa Taasisi ya Mpango wa Usalama Barabarani Tanzania (TARSI), iliyozindua kampeni kutoa elimu kwa wanafunzi walioko shuleni.

Hiyo inafanyika, ikizingatiwa asilimia kubwa ya safari za maisha yao wanatumia barabara, ikiwamo kwenda na kurudi shule, hata shughuli nyingine za kimaisha ikiwagusa moja kwa moja na hasa walioko mijini.

TARSI inafanya hayo kwa shule zilizopo wilayani Kinondoni, japo ndoto ni kuzifikia zote kitaifa. Hapo, Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Godwin Gondwe, akiwa mgeni rasmi kwenye hafla ya uzinduzi huo, ana maoni yake kwamba:"Kwa kushirikiana na jeshi la polisi, hatutomvumilia mtu yeyote atakayesababisha ajali kwa makusudi, hatua kali zitachukuliwa dhidi yake. Mwili wa binadamu hauna spea.

"Kwa hiyo, watumiaji wa barabara pamoja na madereva zingatieni sheria, ukiona taa nyekundu barabarani imewaka hata kama hakuna gari usivuke subiri mpaka taa ya kijani itakapo kuruhusu, kwa hiyo nipo tayari kishirikiana na taasisi hii kuhakikisha kila kitu kinakwenda sawa."



Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Godwin Gondwe (mwenye tai) akiongea na mwanafunzi aliyeshika bango kuzindua kampeni kuelimisha usalama barabarani. Kushoto kwake, ni Kamanda wa Polisi Usalama Barabarani Mkoa, Mrakibu Msaidizi wa Polisi, Notker Kilewa. **PICHA: MTANDAO.**

Mkuu huyo wa wilaya, anahimzia wito wake kwa watumiaji magari katika wilaya hiyo kufunga namba za magari ambazo wamepewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania TRA), ili iwe rahisi kumtambua mhalifu afanyaye kosa.

"Wakati naongea na wanafunzi, nimeambiwa kwamba wanaosababisha ajali barabarani wengi wao ni wamiliki wa magari binafsi na kuna wengine wanafunga namba za nchi za nje ili wasijulikane wakifanya kosa na wengine wanaweka namba zenye majina hata kama muda wake umeisha, hii haiko sawa!

'Nawapongeza sana wanafunzi wa wilaya hii kwa kuwa waelewa. Nimepita, nimeona mmechora michoro mizuri kama 'Zebra' na mnaeleza vizuri maana ya alama hizo. Hilo ni jambo zuri, kwa hiyo ndugu zangu wa TARSI tumekuja hapa kukuunga mkono kwa sababu tunatambua umuhimu wa jambo hili"

Mkurugenzi wa Taasisi hiyo, Maliki Barongo, ana ufafanuzi wa kilichomsukuma kuanzisha kampeni hiyo kwamba ni "kutoa elimu hiyo kwa kuwalenga zaidi wanafunzi, baada ya kubaini wengi wao wanauelewa mdogo juu juu ya sheria za barabarani

"Kama tunavyojua ajali nyingi zinasababishwa na binadamu, hivyo tumezindua programu hii ya kupita shuleni kuwapa wanafunzi elimu ya usalama barabarani, ili wajue namna ya kujiepusha na ajali na baada ya hapo tutaenda katika jamii yote."

Pia, anafafanua kuwa taasisi hiyo haitaishia Dar es Salaam, pekee akibainisha kuwa wamejipanga kufika mikoa mbalimbali, ili kuweza kutanua wigo katika kufikisha elimu hiyo.

Mbali na mipango hiyo, mkurugenzi huyo anaeleza kuelemea na ufinyu wa bajeti kwa kile anachodai, wafadhili ni wachache na anaomba wadau wengine waunge mkono jitihada hizo

"Tumepanga malengo mengi sana, lakini tuna shida ya wafadhili. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kuomba wadau wengine kujitokeza kutuunga mkono, ili tuifikishe elimu kwa mapana zaidi. Naamini kwa kufanya hivyo baada ya miaka kadhaa mbele, kila mwanafunzi atakuwa na elimu na tutafanikiwa kumaliza kabisa ajali za barabarani"

Ili kuonyesha uzito wa jambo hilo, Kamanda wa Polisi Usalama Barabarani Mkoa Kipolisi Kinondoni, Mrakibu Msaidizi Notker Kilewa, amehudhuria katika uzinduzi huo na kuipongeza taasisi hiyo kwa kuanzisha kampeni, naye akiahidi kuipa ushirikiano.

"Naipongeza sana taasisi hii na timu yake kwa kuwalenga watu wengine na wanafunzi. Mwanafunzi ni kijana pekee anayeshika elimu kwa wepesi na msambazaji mzuri wa ujumbe.

"Wameshaanza zoezi hilo katika eneo langu la Kinondoni, kwa hiyo sisi kama kikosi cha usalama barabarani tuaanhid kushirikana vema katika kulifanikisha jambo hili," anasema

Katika kufahamu umuhimu wa elimu hiyo nipashe alimtafuta mwannafunzi mmoja kutoka katika Shule ya Upili Mivumoni, ya Dar es Salaam, Buthaina Salum, anakiri kwamba ni mafunzo yaliyomuongeza uelewa w a kina kuhusu usalama barabarani.

AFYA

# Unajua mikataba lishe? Pata tathmini vita udumavu inavyowajibisha watendaji

## • Wiki moja ya mkataba uliozinduliwa nchini

**Na Waandishi Maalum**

SIKU sita zilizopita, serikali nchini kupitia Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), katika Kitengo cha Lishe, ilifanya tathmini ya utekelezaji wa Mkataba wa Lishe kwa Mwaka wa Fedha uliopita mjini Dodoma, katika hafla mgeni rasmi alikuwa Rais Samia Suluhu Hassan.

Ni tathimini iliyoambatana na kuingia mikataba na wasimamizi wa shughuli za lishe ngazi ya mikoa na wilaya nchini.

Kimsingi, ni hatua kuu tatu muhimu.

Kwanza ni maandalizi ya mikataba lishe, hatua ya pili ni kuingia mikataba hiyo baina ya serikali na wasimamizi wa masuala ya lishe katika ngazi husika na tatu ni hatua ya utekelezaji mikataba hiyo, hatua zinazohitaji sana tathmini na ufuatiliaji wa karibu wa utekelezaji wake, ili kubaini na kuchukua hatua stahiki kwa wakati muafaka.

Ni hatua inayotajwa kuwa muhimu sana kufikia malengo tarajiwa ya uanzishwaji wake. Miongoni mwa malengo hayo, ni kupunguza hali ya udumavu kutoka asilimia 32 hadi 24 ifikapo mwaka 2026.

Aidha, kuna suala kufanikisha milo mchanganyiko kwa kiwango kinachokubalika, kutoka asilimia 30.3 hadi asilimia 50 ifikapo mwaka huo. Hapo inaenda na kuongeza kutolewa fedha katika eneo la lishe kutoka asilimia 56 za mwaka wa fedha 2020/21 hadi asilimia 100.

Maeneo mengine katika mustakabali huo kwa mujibu wa Utafiti wa Kitaifa wa Hali ya Lishe nchini, 2018, ni haja ya kuongeza milo yenye viwango mchanganyiko vinavyokubalika kutoka asilimia 30 hadi asilimia 50 ifikapo 2026.

Pia, kuna suala la kupunguza idadi kubwa ya watoto wenye udumavu wakiwa katika umri chini ya miaka mitano, idadi yao ikiwa milioni tatu, kwa mujibu wa tathmini iliyofanyika na utekelezaji wake kuanza mwaka 2017/18.

Hata hivyo, inatajwa ni hatua inayohitaji sana tathimini na ufuatiliaji wa karibu katika utekelezaji, pia kusambaza taarifa kwa wananchi na taasisi mbalimbali, ili wazitumie kama funzo la kuboresha utekelezaji shughuli za lishe nchini, hasa kwa mikoa inayofanya vibaya katika masuala ya lishe.

### HATUA ILIYOFIKIWA

Hatua ya kwanza muhimu kwa taifa, ni kwamba kuna mikataba imeshaandaliwa na wananchi kupewa taarifa kuhusu umuhimu wa kufikia hatua ya maendeleo ya kielimu, kiafya na kiuchumi na kitaifa kwa ujumla.

Pili, inatajwa ni kutia saini mikataba hiyo, kati ya serikali, watekelezaji na wasimamizi wa masuala ya afya na tayari na imeshafanyika jijini Dodoma mnamo siku hiyo ya Ijumaa wiki iliyopita, mbele ya mkuu wa nchi.

Hatua ya tatu, ni kutekelezwa mikataba hiyo katika maeneo mbalimbali nchini inayotajwa kuwa muhimu sana, kwa sababu inatarajiwa kusaidia mamlaka husika na taifa zima kwa ujumla kujifunza na kubaini maeneo ambayo yalifanyika vizuri na ambako hakukuwapo ufanisi.

Hapo kunatajwa sura ya funzo na wakati huohuo, kuchukua hatua stahiki kwa yenye walakini.

### UKANDA WA FAIDA

Baadhi ya faida za kufanya tathmini na ufuatiliaji wa karibu wa utekelezaji mikataba ya lishe nchini ni katika kuboresha utekelezaji, hasa ambako hakufanyiki vizuri, ikibeba dhana "kujifunza kwa wengine wanaofanya vizuri sio mbaya".

Vilevile, mwisho taarifa za tathimini na ufuatiliaji wa utekelezaji wa mkataba wa lishe nchini kuna matarajio kwamba, zitasaidia nchi nyingine na jumuiya za kimataifa kujifunza mapungufu yaliyojitokeza, hivyo kuwekwa mpango mkakati utakaosaidia kubaini maeneo yanayohitaji maboresho katika mipango ndani ya maeneo yao.

Taarifa hizo zaelezwa zitaonyesha maeneo kulikofanyika vizuri hata kugeuka mfano wa kuigwa katika kuandaa na kutekeleza jukumu kama hilo kwingineko duniani.

Hivyo, taarifa kutoka takwimu za utekelezaji mikataba ya lishe, nazo ni vigezo vya kuisaidia Wizara za Elimu, Afya na TAMISEM, kujua maeneo yanayohitaji nguvu zaidi, ili zikatoe huduma inayoakisi mahitaji ya lishe ya wananchi wa eneo husika.

Ufuatiliaji nao unaorodheshewa faida nyingi zitokanazo na utekelezaji mikataba ya lishe nchini. Baadhi yake ni kusaidia kuongeza uwajibikaji miongoni mwa watendaji, pia mgawanyo sahihi wa rasilimali zinazohitajika katika kuendesha mikataba hiyo.

Suala la utekelezaji kikamilifu, linatajwa kutegemea utayari wa kisiasa na kijamii nchini. Hivyo, inarejewa kuwa muhimu, kila mwananchi ahamasike kushiriki na kutoa mchango wake katika utekelezaji mikataba hiyo ya lishe katika jamii yake, ili kupunguza udumavu na utapiamlo nchini.

- ***Imeandaliwa na Elifuraha Msese Katibu wa Afya wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga (Simu: 0625734800) na Pankras Luoga (Simu: 0757645746), Mhadhiri Msaidizi wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Tiba Muhimbili.***



Wakuu wa Mikoa wakitia saini mikataba ya Usimamiaji wa Shughuli za Lishe, katika ukumbi wa Halmashauri ya Jiji Dodoma.



Rais Samia Suluhu Hassan, akikagua mabanda yanayohusiana na sekta ya Afya na Lishe, kabla ya kushiriki utiaji saini jijini, Dodoma. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**



Rais Samia Suluhu Hassan, alipozungumza kwenye uzinduzi wa Mikataba ya Usimamiaji wa Shughuli za Lishe, wiki iliyopita jijini, Dodoma.

AFYA

# ...Vijana kuifikia lishe bora inapobaki kuwa janga kitaifa

Na Nimi Mweta

KATIKA suala la lishe, wasiwasi huwa unakuja katika sura mbili; moja kutokana na umasikini, halafu nyingine inatokana na kufaulu maisha

Wakati Rais Samia Suluhu Hassan anatoa rai kwa watafiti kuelekeza macho yao kwa changamoto za lishe zinazowakabili vijana (kwa maana ya wanaume) Ijumaa iliyopita, mtazamo wa watafiti wanawake, kila iitwapo 'leo' wanasisitiza kinamama ndio wanaofanya kazi zaidi majumbani, hata shambani.

Kijadi, wanaume ndiyo wanatakiwa kulisha familia, ila vijana siku hizi wanaishia kupata kazi za hapa na pale kando ya gereji, dukani, penye soko, magari, ili kupata 'chochote' ndani ya saa au hata siku.

Muda uliobaki unatumika kungoja kitokee kingine cha kufanya, ili kuwasaidia kwa ujira kidogo. Ni hali inayomuwezesha kijana kujipatia mahitaji kadhaa ya lazima.

Mojawapo ni lile alilozungumzia Rais Samia kama 'supu ya pweza,' kujenga nguvu ya mahitaji ya kinyumba. Moja ya vianzio vya hali kama hiyo ni ulegevu wa jumla kimaisha, unaosababisha udhaifu viungo kiasi fulani, ila kipato hafifu huzuia lishe linganifu.

Wakati huohuo, kile kidogo wanachokipata kinaweza kutumiwa isivyopasa kununua pombe kali za 'bei poa' pombe nyeupe zilizo katika chupa ndogo zinatajwa hukata kiu mapema zaidi.

Hapo kuna matokeo gani? Kama tumbo halikutangulizwa lishe inayofaa, madhara ya 'tija ya unyumba' hujitokeza. Kimsingi, jambo hilo linaanza kuleta wasiwasi katika ngazi za juu kiafya.

Haitakuwa rahisi kupata majawabu kwa suala hilo kirahisi, kwani tatizo la udhaifu wa mwili na hitilafu ya kinyumba haliangukii katika kipato pekee, bali hata matumizi mabaya ya fedha, vyakula na vinywaji visivyo na tija mwilini.

Ila isingekuwa rahisi kwa kongamano la kiutawala kuangalia kwa karibu tatizo la kisaikolojia, au hali ya akili kwa wakati hitajiwa, kupungua kujiamini mwanaume anapomtegemea mwanamke kumudu mahitaji ya nyumba.

Anaposhirikiana na mwanamke huyo kwa njia ya kuegemea huku akitumwa kazi za hapa na pale, inaweza isiwe tatizo, ila akitaka awe mwendesha nyumba halafu hana fedha, atakwama.

Anaposhindwa, ni hali inayoathiri kujiamini, kama vile anahitaji mazingira ambayo udhaifu



Mtoto akilishwa chakula. **PICHA: MTANDAO.**

wake hautangulizwi. Hivyo, hatari anayozungumzia rais kuhusu lishe ya vijana na usalama au uthabiti wa taifa, inahusiana kwa karibu na vijana kutokuwa na kipato cha kufaa kusimamia familia.

Ni hali ya lazima inayohitajiwa ili kijana ajisikie ndiye mume au baba nyumbani, hali ambayo inapoonyesha mapungufu anatafuta hifadhi katika raha za hapa na pale, za vyakula na vinywaji, zinaweza kuathiri afya hata zaidi.

**DIRA YA UZAZI**

Hali hiyo inatakiwa kuweza kupunguza kasi ya uzazi, kwani mwanamke anaweza kuwa na watoto kadhaa anapokuwa katika mazingira ya uhakika kifamilia. Wanaobahatisha tu na vijana wa mpito, au dhamira ya kujenga familia iliyofifia, hawaendelezi uzao hima.

Suala hapo ni kama kutakuwa na upungufu halisi wa uzazi katika rika iliyopo kutokana na kipato, lishe duni na kutojiamini, kunavyoathiri uwezo wa kuwa na unyumba thabiti kwa vijana wengi.

Upo uwezekano bayana kuwa uzazi unaweza kupungua, hali inayoonekana kwa wanawake wengi ambao bado ni vijana, ana mtoto mmoja (kwa tamaduni za pwani wanaita 'suna') kuondoa ombwe la tuhuma ya ugumba au ya kutokuolewa.

Mwanamke akiwa na mtoto ana heshima kamili ya mama, bila kuwa na 'kibarakashia' cha mke ambacho - nje ya suala la kumudu maisha, huuliziwa na watu wa rika kubwa.

Mtu anaweza kutofautisha kati ya uwezo wa kuunda familia na kuilinda, kwani hatua ya kwanza inafikiwa na vijana wengi, lakini si rahisi kwao kusimamia familia baada ya hapo.

Kukwama ndoa nyingi za vijana (au zaidi ni kukaa pamoja, kwani ndoa rasmi zina uwezo zaidi wa kudumu) kunaleta mazingira ya familia za mzazi mmoja, kwani watoto watalelewa na mama, ajitahidi kibiashara na misaada ya mahusiano ya hapa na pale. Kuolewa upya ni tatizo; unakuta mume hataki kuona watoto anaokuja nao.

Licha ya kwamba maelezo ya Rais Samia yalilenga upande mmoja wa afya ya kinyumba ya vijana wengi katika mazingira ya sasa, au kwa mujibu wa hisia za hapa na pale na taarifa halisi za kitiba, kuna upande mwingine wa suala hilo.

Tanzania kama zilivyo nchi nyingine iko katika wimbi la utandawazi na maendeleo kwa jumla. Ila, hisia za kijamii zimejikita katika jadi, hivyo kutazamia kijana akifikia umri labda angalau miaka 25 au zaidi kidogo, afikirie na aweze kuunda familia.

Hali hiyo si rahisi kwa sasa na familia za muda huo zinakuwa za majaribio zinazovunjika halafu kijana aunde familia nyingine baadae. Ni mchanganyiko halisi.

Kinachotokea sasa ni maendeleo au mabadiliko, kwani yako maeneo mengine ya mabadiliko ya uhusiano kijinsia, ambayo rais hakuyajadili, akielekeza hisia zake kwa suala la lishe duni na uhitaji hatarishi katika masuala ya unyumba.

Huo ni mwendelezo tu wa kuparanganyika. Kimsingi, uhusiano wa kijinsia unaendana na kukwama mfumo wa jadi ambako mwanamke alitegemea kuletewa mahitaji na mwanaume. Anatumika tu kwa kazi za nyumbani kama kukata majani, kukamua maziwa, kuchota maji, kutafuta kuni na kulima.

Usawa wa kijinsia kwa muda mrefu umezungumziwa kisheria, hasa kwa masuala ya elimu au kupata kazi, kuingia maeneo ya kipato ambayo yalisimamiwa na wanaume muda wote.

Uhuru wa wanawake kupata watoto wakiwa nyumbani, halafu kuwa na wasichana wa kazi ambao wanaanza kuwa na uhusiano na vijana mtaani mbele ya watoto, kimyakimya kumeondoa uhusiano kimapenzi katika mduara wa 'jando na unyago' na kuingiza katika mawasiliano ya kawaida.

Wazazi wanapofanya kazi na hasa inapokuwa ya nyumba ya mzazi mmoja kujifunza mapenzi si kazi kubwa. Ni mazingira ya mparaganyiko wa uchumi wa jadi ambao baba na mama wanafanya kazi, halafu watoto wanabaki na msichana anayeanza pia kujifunza mapenzi, hivyo nyumba wakati wa mchana ni eneo la mawasiliano.

Ikitokea wako mtaani na kuna mzazi mmoja, vigezo vya awali na woga havipo; wasichana hupata mimba za hapa na pale za vijana, pengine wakaanza kukaa pamoja wakakwama.

Vijana hushindania mapenzi na wanapata tabu nyingi katika anga hizo; urahisi wa maisha, chipsi na 'K-Vant' huwa kimbilio. Unaweza pia kuongeza vijana kutafuta pesa ya kujikimu ya kupewa kama wasichana tu.

MAZINGIRA

MGOGORO WANAKIJIJI KATAVI VS TAWA

# Busara za RC Mrindoko kukutanisha wanaosuguana zatuliza moto, kila upande 'watapika nyongo' zake

- Maswali ya kiualimu yamwibulia yaliyojificha
- Aamua: Serikali, wananchi wote mna makosa
- Tume ya siku 10; waliokamatwa wafutiwe kesi

**Na Neema Hussein, aliyekuwa**

**MLELE**

NI kijiji cha Kamsisi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mlele mkoani Katavi, yenye zaidi ya wananchi 400 ikikumbwa na mgogoro wa ardhi dhidi ya Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), sasa unadumu miaka kadhaa, upeo wa wastani wiki kadhaa mwezi sasa 'moto' unawaka'.

Utata huo unamuinua kitini Mkuu wa Mkoa wa Katavi Mwanamvua Mrindoko tarehe 20 mwezi uliopita, kwa safari hadi kijijini hapo, lengo ni kujua chanzo cha mgogoro na utatuzi wake.

Mrindoko akawakuta wanakijiji sehemu moja wamejikusanya, yeye anaonyesha shauku kujua hatima ya msuguano na TAWA baada ya mvutano na baadhi yao kukamatwa na polisi.

Mrindoko anaanza kusikiliza hoja moja baada ya nyingine kutoka pande zote mahali hapo penye msuguano, kudadisi mmiliki halali wa eneo linalogombaniwa kati ya TAWA na wananchi.

Mkazi, Amri Anthony, anawasilisha madai ya madhila yaliyomkuta tarehe 16 mwezi uliopita, kwamba alipelekwa Inyonga alikokaa mahabusu siku tatu bila ya maelezo yoyote. Hapo analalamika: "Mpaka leo (siku aliyofika RC) saa nne, ndiyo Ofisa Upelelezi akaniita kuchukua maelezo yangu, akasema wewe kesi yako utapata dhamana muda wowote.

"Nimedhalilishwa sana siku ya kwanza nilipopelekwa ndani, nilipigwa sana! Baada ya kupigwa sana saa saba usiku nikatolewa nje nilipitishwa hii hii barabara kwenda kule Tulieni, nikalazimishwa niende kuwachunguza wenzangu kaya moja hadi nyingine.

"Nilipigwa sana mimi wakati kesi yangu ilikuwa ni kuwalalamikia hawa TAWA wasikae kwangu muda ule. Hawa TAWA wakarudi kule wakachoma nyumba zangu, lakini chanzo cha ugomvi ni diwani na mwenyekiti."

"Hao ndio chanzo cha kuchonganisha, kwa sababu ule mgogoro walituuzia wenyewe hawa viongozi wetu," anasimulia Anthony, hoja iliyobeba hisia za Mkuu wa Mkoa Mrindoko akahoji "walifanyaje?"

Anthony akafafanua: "Walituuzia, kwa sababu mara ya kwanza walituuzia wenyewe, sisi wananchi tukafyeka tukakaa. Mwaka 2017 wakatuletea kiwanda cha nyama, ranchi tukaikataa mbele ya mkuu wa wilaya.

"Tulikuja kuikataa hapa hapa na mkuu wa mkoa mwaka juzi tarehe 5 mwezi wa 12 akaja kuidhinisha wananchi kule tukafanye kazi, ila baada ya kutoka habari za mkuu wa mkoa, yakaja mabadiliko kuwa wale watu walioko kule ni kupeleka jeshi ndiyo kutuletea TAWA.

"TAWA nao wanakuja kule kinguvu, hakuna mkutano wowote sio mkutano wa balozi wala mwenyekiti, bali tunaambiwa tutoke kule na kama tuna akili timamu tukabidhi eneo lile bila ya kulazimishwa.

"Mimi juzi nikawaambia nipeni fidia zangu, nikisema 'hata milioni tano mnipe, ndio tutaondoka hapa.' Ndio kisa cha kunibeba na kuanza kunipiga..."

Hoja kama hiyo inatolewa na mkazi Masala Mganga, anayeutaja kuwa' utata wa muda mrefu', akimueleza mkuu wa mkoa: "Tumeshitukia tu hiyo kampuni linakuja tunauliza kwamba vipi? Ikoje? Wanasema 'mwenyekiti wenu ndio anajua.'

"Tunaenda kwa mwenyekiti, ili kujua taratibu zikoje kuhusu TAWA na sisi wananchi, mwenyekiti anachukua hatua zingine na mpaka tulifikia kuwekwa ndani kwamba tumeenda kumvamia mwenyekiti.

"Tulienda kwa kujua kwamba mwenyekiti ndiyo mlezi wetu ambae anatuwakilisha masuala yote ya uongozi, tumesota mpaka ikafikia hatua watu wakawekwa ndani kwa kisingizio kuwa tumeiba maharage, kwa kweli mkuu wa mkoa kero yetu ni TAWA kuchukua mashamba yetu."



Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mwanamvua Mrindoko, akizungumza na wakazi wa Kamsisi, wilayani Mlele, Katavi. **PICHA ZOTE: NEEMA HUSSEIN.**

Mwanamama Prisca Jonas, mkazi wa Kamsisi anapewa nafasi naye anaeleza kwa hisia akitokwa na machozi kwamba hadi wakati huo mume wake hajulikani aliko.

"Baada ya kufika pale nyumbani nikaambiwa mume wangu anatafutwa na sikujua kwamba anatafutwa kwa misingi ipi, kwa kweli nikazidi kuumia na kufuatilia kuwa anatafutwa kwa kosa gani ila sikupata jibu," anasimulia.

"Muda wa saa nane usiku, nikasikia mlango unagongwa kwa muda mrefu sana pamoja na dirisha...wakaanza kusema sisi askari polisi, Joel toka! Nikatoka, nikafungua wakaniuliza 'mume wako yuko wapi' nikawaambia sijui, mimi nilitoka asubuhi nikaenda kanisani nimerudi sijamkuta.

"Mimi moyoni nikajua kwamba walikuwa wanamtafuta watakuwa wameshamkamata, wanataka nijue namtafuta kwa kosa gani," anaeleza. Mkuu wa Mkoa akahoji kwa ukali "mume wako anaitwa nani?" mama huyo akamtajia jina, akifafanua, watu hao walikuwa na bunduki na wamevaa mavazi meusi kuanzia kichwani, vigumu kuwatambua.

"Nilimbeba mwanangu mgongoni, wakaniambia 'simama hapa!'. Wakaingia ndani wakaanza 'kusachi' humo ndani huku wakisema 'mwambie mume wako atoke' nami nikasema 'sijui alipo'...Kwa kifupi ndugu Mkuu wa Mkoa kwa sasa hatuna amani!"

Mkazi anayejitambulisha kwa jina, Godfrey, anachangia kuwa: "Taasisi ya TAWA imekuja ikatukuta sisi tupo pale, lakini baada ya kuja hatujashirikishwa wala mkutano wowote hatujaitwa kuelezwa kuwa hapa tuna taasisi hii ambayo ina faida hii kwa wananchi. Haya malalamiko tulishayafikisha Ofisi ya Kijiji Kamsisi, lakini hatujapata msaada wowote.

"Tulibaki pale masika ilipoingia tukaanza kulima, tukaja kufyekewa mazao yetu. Tulikuja tena hadi kwa mwenyekiti wa kijiji ili tujue kinachoendelea katika mgogoro huu.

"Baada ya kufika pale, tulibambikiziwa kesi kwamba tumeenda kumvamia mwenyekiti, baadae tukawa ni watu wa kuwekwa ndani na mle hatukutoka bure, tumetoka kwa gharama.

"Bila shaka hata wewe Mkuu wa Mkoa kuna siku ulipokea simu kwamba huku Kamsisi kuna mazao yamefyekwa. Tumeendelea hivyo hivyo, mpaka ilifikia wizarani na 'stop oda' ikatoka kwamba hiyo taasisi isitishe kwanza shughuli zake na uchunguzi ufanyike."

Mkuu wa Mkoa akataka kuzijua wizara husika, akajibiwa TAMISEMI na hata alipohoji iwapo kuna barua zozote, akasema wanayo, baadhi wakisisitiza wametoka mahabusu siku hiyo.

### OFISA WA TAWA

Ofisa Ugavi wa TAWA Kanda Magharibi, Mayanzi Kidanha, anaeleza mkutanoni kwamba eneo hilo lina ukubwa wa ekari 131 na sasa wanaendelea kutekeleza miradi. Ni ufafanuzi ulioendana na maswali ya Mkuu wa Mkoa.

"Wakati tunaendelea na utekelezaji wa hili eneo katika utekelezaji wa jengo lile pale ambalo ni jengo la silaha, wenzetu wa Jeshi la Wananchi walifika siku ya Jumamosi wakatukuta kwenye hili eneo, tukawaonyesha eneo ambalo hiyo amali inatakiwa kujengwa.

"Wakawa wamebaki kwa ajili ya kuandaa kambi. Wakati wa maandalizi ya kambi, alitokea mwananchi mmoja pale ambaye ni wa kiume akawa anasema 'eneo hili hamuwezi kujenga kwa sababu mimi ninalimiliki, la sivyo hapa mimi nitamwaga damu za watu au nitawatilia sumu.' Kwa hiyo binafsi niliona yale maneno siyo mazuri.

"Walikuwepo wale askari wakaja kuniambia, mimi nilikua kwenye jengo lile la juu (anaonyesha), ikabidi nirudi pale, bahati nzuri nilimkuta palepale. Nikajaribu kumuuliza kwamba 'kuna changamoto gani hapa?' akasema, bwana mimi nimeshangaa nimeona watu wamekuja hapa kwenye eneo langu, mimi sina taarifa na wanasafisha kwa ajili ya kuseti kambi," anafafanua.

Anasema, wakati wanaripoti kwenye miradi hiyo kwa mkuu wa wilaya na mamlaka za polisi wilaya hiyo, wakapatiwa ofisa wa kuwahudumia na hata pale alipopata changamoto, akarejea kumfahamisha, zikiwemo kauli za vitisho walivyopatiwa na mwananchi huyo.

"Kwa sababu hatukuona kwamba tunaweza kuyachukulia kwa wepesi, baadae OCCID (Mkuu wa Upelelezi Polisi Wilaya) alishauri kwamba kama tuna gari tumfikishe kituo cha polisi...Mimi binafsi nilikuwepo pale, nikamuita nikamwambia aingie kwenye gari akakubali tukafika kituo cha polisi kwa ajili ya hatua zingine.

"Kwa hiyo, tunaendelea na huo ujenzi na DC (Mkuu wa Wilaya) na jeshi la polisi wamekuwa wakitusaidia kusukuma kazi ziende na mpaka hapa kikwazo kikubwa ni huu uvamizi," anafafanua Mayanzi.

### MKUU WA WILAYA

Mkuu wa Wilaya ya Mlele, Filberto Sanga, anaeleza historia fupi ya mgogoro, kwamba awali eneo ilikuwa misitu ya hifadhi na baadaye kukapangwa matumizi bora ya ardhi, wakalipima eneo hilo.

Anasema, ikaelekezwa itumike kufuga nyuki na mengineyo kuhusiana na hifadhi misitu na baadae wananchi wakaamua kuanza kugawa kwa maana kuwagawia watu, ili waanze kulima na kuanzisha makazi.

"Kwa sasa, eneo ambalo linaonekana lina mgogoro ni lile ambalo baada ya kuja watu wa TAWA kuanza kujenga, wananchi hoja yao wanasema kijiji kimewauzia watu wa TAWA lile eneo, kwa hiyo ndio hicho ambacho wanapigania.



Wakazi wa kijijini Kamsisi wilayani Mlele, wakiwa mkutanoni katika picha tofauti.

"Baada ya mimi kuhamia hapa mwaka jana, tulipata taarifa hiyo tulikwenda tukakutana na baadhi ya wananchi wale wanaoishi kwenye hilo eneo japo wananchi wengi hawakuja, anasimulia na kuendelea:

"Baada ya kukutana tukakubaliana vizuri tu kwamba jamani mko tayari kupewa eneo jingine ili hili eneo litumike kwa shughuli za serikali, wakasema wako tayari," anasimulia.

Sanga anaeleza kwamba, wananchi wakashitushwa kwa madai 'TAWA sio waaminifu', wakianza kuuza na inaonekana wengi wamejenga kuanzia mwezi wa Aprli hadi Juni.

"TAWA lile eneo baada ya kupewa, halmashauri (Mlele) iliwapa hati. Kwa hiyo, wana hatimiliki, ndio maana tulisimamia ujenzi katika lile eneo," anaeleza.

### RC KATAVI

Mkuu wa Mkoa Katavi, Mwanamvua Mrindoko, akaamua kutoa msimamo wake, akitamka: "Nirudie tena kusema pande zote mbili mlikosea, serikali ambayo ni ya halmashauri inayoshuka hadi kwenye vijiji pamoja na taasisi zake zote kuna mahali wamekosea. Pia, wananchi kuna mahali mmekosea, hilo tulishakubaliana.

"Sasa tumesema tutafute ufumbuzi wa jambo hili ili tuweze kulimaliza. Sasa kabla sijasema hatua za ufumbuzi, nianze kwa kusisitiza mambo yafuatayo, wananchi pamoja na taasisi za serikali, tuendelee kuheshimu amani, utulivu na usalama uliopo.

"Namaanisha kwamba kwa kuwa tunaelekea kutatua mgogoro huu, sitopenda kusikia kuna mwananchi amepigwa wala kuna askari amepigwa..."

Ni katika hatua hiyo akamuelekeza Kamanda wa Polisi Mkoa wa Katavi, pia wa wilaya Mlele na vituo vyote vya polisi, kuwaaachia wananchi iliowakamata.

"Suala lingine kwa upande wa wananchi niwaombe sana kusema kwamba, kesi hii tumeifuta, sio kwamba sasa tumehalalisha uhalifu... nasema tena asitokee mwananchi yeyote anakwenda kufanya makosa akatarajia tena mkuu wa mkoa atakuja asimame hapa aseme tena futa mafaili yote.

"Sitapenda kusikia kuna mtu kapigwa, sitapenda kusikia kuna mtu kachomewa nyumba, sijui kibanda sijui na mahindi. Naomba niwaeleze, askari wetu wanafanya kazi walizopewa kwa mujibu wa sheria.

"Suala la kwenda kumchomea mtu nyumba yake, suala la kwenda kumchomea mahindi ambayo ni chakula cha mtu fulani hilo sio agizo la serikali. Narudia tena, sio agizo la serikali na kama mtu atakwenda kufanya vitendo hivyo na tukabaini, hatutojali ana cheo gani iwe kwenye jeshi iwe kwenye nini!"

Mkuu wa Mkoa Mrindoko akajumuisha kwamba, tume ya siku 10 aliyounda kuanzia Septemba 26, itafanya kazi kuchunguza undani wa mgogoro ulivyo.

### NAIBU WAZIRI

Kabla ya ziara ya Mkuu wa Mkoa, mnamo Septemba 10 mwezi uliopita, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, akafika mkoani Katavi kutoa tamko la serikali kuhusu maeneo yaliyopandishwa hadhi kuwa mapori ya akiba, Juni 25 mwaka jana, ambayo ni: Luganzo Tongwe, Igombe, Wembere, Inyonga na Ugalla katika mikoa ya Katavi Kigoma na Tabora

Baada ya matangazo hayo, kuliibuka malalamiko kutoka kwa viongozi na wananchi wa maeneo hayo kuhusu mipaka, baadhi ya mamlaka za serikali za mitaa na vijiji, pia maeneo kuingizwa ndani ya mapori hayo.

Naibu Waziri Mary, akasema wizara yake iliunda kamati ya wataalamu kutoka Ofisi ya Rais Ikulu, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mamlaka ya Usimamizi wa TAWA, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Wizara ya Ardhi na Wilaya ya Tanganyika, ili kushughulikia suala hilo.

Anasema kamati husika ilikamilisha kazi yake na kuwasilisha taarifa, ikibaini mambo kadhaa; Mosi, kutoshirikishwa wadau katika mchakato wa kubadilisha hadhi hifadhi za misitu kuwa mapori ya akiba; pia, kuathirika mazao yatokanayo na misitu, ikijumuisha mbao na magogo.

Naibu Waziri anasema, serikali imeagiza mchakato wa uanzishwaji Pori la Akiba Luganzo Tongwe, uanze upya na ufanyike haraka kwa kuzishirikisha wizara za Maliasili na Utalii na Ardhi; serikali za mitaa kutoka mikoa ya Tabora, Katavi na Kigoma, TFS na TAWA.

Naibu Waziri Mary anasema, serikali imeelekeza tathimini ya kamati ya mawaziri wanane iliyoundwa, iendelee kuzunguka nchi nzima kutoa ufafanuzi.

Anafafanua, wao Wizara ya Maliasili na Utalii, wameziona changamoto zinazoendelea kuwepo pamoja na kuwa Rais ameachia vijiji hivyo 920, sasa ni jukumu la wizara yao kutambua changamoto na kuzitatua.



Sehemu ya mazingira yanayogombewa kati ya wananchi na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA).

AFYA

# Operesheni kumaliza shida vichwa vikubwa kwa watoto 500 kila mwaka

## • Waziri Ummy aanza na agizo la Rais lengo la 2023

**Na Mary Geofrey**

HADI sasa sehemu kubwa ya wananjamii, bado wanaamini kwamba tatizo la watoto kuzaliwa na vichwa vikubwa na mgongo wazi, mzizi uko katika ushirikina.

Tatizo hadi sasa linawagharimu wazazi na taifa, likitumia fedha nyingi kwa ajili ya matibabu, madaktari wanasema chanzo ni ukosefu wa virutubisho muhimu mwilini anavyotakiwa kuwa navyo mwanamke kabla ya ujauzito.

Katika kusaidia hilo, serikali inagawa bure vidonge vya 'folic acid' kwa wajawazito wanaohudhuria kliniki, ili kuwalinda watoto watakaozaliwa. Ni virutubisho vitokanavyo na matunda, mboga za majani, mayai na milo yenye protini.

Takwimu za Wizara ya Afya, zinaonyesha kuwa katika kila watoto 1,000 wanaozaliwa nchini, watatu wana tatizo la mgongo wazi na kichwa kikubwa.

Hivyo, kwa mwaka kuna takribani watoto milioni mbili wanaozaliwa nchini na matatizo hayo, ikiangukia wastani watoto 6,000 kila mwaka wanazaliwa na matatizo hayo

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, anaeleza takwimu hizo na mikakati ya serikali ya kusaidia kundi hilo lenye watoto 500 wenye matatizo, kuanzia mwakani.



Watoto wenye vichwa vikubwa katika mandhari tofauti. **PICHA ZOTE: MTANDAO,**

**SERIKALI NA MATIBABU**

"Kwa hiyo Rais Samia Suluhu Hassan, ameielekeza Wizara ya Afya kuanzia mwakani tutagharamia watoto 500. Nitoe wito kwa wazazi na walezi wasiwafiche watoto wenye vichwa vikubwa na mgongo wazi.

"Badala yake wawapeleke kwenye vituo vya afya na hospitali ili wafanyiwe upasuaji ili na wao waendelee na maisha yao ya kila siku," anafafanua Waziri Ummy, akitaja.

Aidha, anaeleza kwamba zaidi watoto wanaozaliwa na kichwa kikubwa na mgongo wazi ni tatizo kubwa nchini na takwimu zinaonyesha katika nchi tano barani Afrika Tanzania ipo nafasi ya tatu kwa idadi kubwa ya watoto wanaozaliwa na matatizo hayo, ikitanguliwa na nchi za Algeria na Ethiopia.

"Na tatizo hili watalaamu wameeleza tunaweza kulizuia kwa sababu vichwa vikubwa na mgongo wazi unatokana na ukosefu wa madini ya 'folic acid' yanayopatikana katika vyakula tunavyokula.

"Baadhi ya vyakula hivyo ni njegere, maharage, karoti, machungwa, mboga za majani pamoja na maboga. Kwa hiyo tunaweza kupata 'folic acid' katika vyakula tunavyokula," anasisitiza Waziri Ummy.

Wito kwa kinamama wenye umri wa kujifungua, kuanzia miaka 15 hadi miaka 49 na hasa wanaopanga kupata watoto, wahakikisha miezi sita kabla ya ujauzito wawe wanakula vyakula vinavyowapatia 'folic acid'.

"Nitoe wito kwa wajawazito kuhudhuria kliniki mapema, kwa sababu kuna tatizo la wajawazito wengi kuchelewa kwenda kliniki wakiwa na ujauzito," anafafanua.

Waziri anahimza virutubisho hivyo vinatolewa bure na zinakuwa katika mfumo kidonge, ambacho mhusika atakula kimoja kwa siku, miezi sita kabla ya kupata ujauzito.

"Kuna baadhi ya taasisi walikuwa wanataka tuzitoe kwa wanafunzi, lakini tukaona ni vema vidonge hivyo vikatolewa kwa wale wanaopanga kubeba ujauzito," anaeleza Waziri, akihimza kwamba serikali itaendelea kuwekeza katika huduma za afya ya uzazi, hususani kabla ya ujauzito, wakati wa kujifungua na baada ya kujifungua.

"Lakini niwatake waganga wakuu wa mikoa na wilaya kuhakikisha 'folic acid' zinapatikana katika vituo vyote vya kutoa huduma, kuanzia zahanati, vituo vya afya na kwenye hospitali," anasema.

**OFISA LISHE**

Ofisa Lishe wa Taasisi ya Tiba ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu (MOI), Germana Gasper, anasema watoto wanaofanyiwa upasuaji wa kuwaondolea uvimbe wa vichwa vikubwa, wanategemea lishe bora ili wapone majeraha, badala ya kutegemea dawa pekee.

Germana anasema, tiba lishe inahitajika zaidi kwa wagonjwa wanaotibiwa hospitalini na inapokosekana, inasababisha utapiamlo kwa watoto hao wenye kichwa vikubwa.

Anatoa tafsiri, mtoto anapozaliwa na kichwa kikubwa, anakuwa hajapata lishe ya kutosha na ndiyo sababu akifikishwa hospitalini, wanaanza kumpa matibabu ya lishe.



Mtaalamu huyo anadems, wapo watoto wanaopewa tiba lishe na kukaa sawa, ila enye matatizo makubwa hupatiwa dawa za kuwasaidia, hivyo ili kiwa salama dhidi ya matatizo hayo ,wanapaswa kupata mlo kamili unaozingatia makundi ya vyakula.

**VYAKULA VIRUTUBISHI**

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, katika taarifa yake anataja mkakati wa kiserikali ulioko mbioni, kutengeneza mashine nchini za kuongeza virutubishi katika unga zitakazotumiwa na wasindikaji wadogo na wakati.

Kwa mujibu wa Jenista, ni mkakati unaoandaliwa kupitia Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO), Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), pia, Tume ya Sayansi na Teknolojia nchini (COSTECH), pamoja na wadau wengine.

Meneja Mradi wa Programu za Uongezaji Virutubishi katika vyakula kutoka taasisi ya kimataifa ya Global Alliance for Improved Nutrition (GAIN), Archard Ngemela, anaeleza umuhimu wa virutubishi lishe katika vyakula. Anaendelea kufafanua.

"Hayo yote ikiwamo utapiamlo yanatokana na upungufu wa virutubishi mbalimbali. Hivyo, ni muhimu kula vyakula vyenye virutubishi, yakiwamo mafuta ya kula, unga, mahindi na vingine."

Ngemela anasistiza kwamba, chakula cha binadamu ndicho kinachobeba virutubishi mwilini kuupatia nguvu, kuusaidia kukua, hata kupambana na maradhi.

AFYA

# Ni vita mpakani Kagera kudhibiti ebola inayotikisa Afrika Mashariki

## • Maabara, wataalamu na simu maalum
## • Elimu kila kona mtaani, WHO yajiunga

**Na Waandishi Wetu**



Mandhari ya shughuli za mji wa mpakani Mutukula, wilayani Misenyi, mkoa wa Kagera.

EBOLA ni nini? Ni virusi hatari vyenye dalili zinazojumuisha homa ya ghafla, udhaifu mkubwa, maumivu ya misuli na koo, kutapika, kuhara, homa kali na kutokwa damu ndani na nje, dalili zikijitokeza kati ya siku mbili hadi wiki tatu.

Kuna wakati inaweza kuhusishwa na magonjwa mengine kama vile malaria na taifodi na maziko ya aliyeathiriwa, yanatajwa kuwa hatari kwa waombolezaji wanaowasiliana moja kwa moja na mwili.

Mnamo Septemba 20 mwaka huu, mgonjwa wa kwanza aligundulika kuambukizwa virusi vya ebola nchini Uganda na kutangazwa na Wizara ya Afya nchini humo.

Ni hali inayoifanya mara moja mpaka kati ya Tanzania na Uganda kugeuka eneo la tishio kwa 'salamu' za mlipuko kusikika wilayani Mubende katikati ya nchi hiyo. Siku kadhaa ilisikika watu watano walipata ugonjwa huo jijini Kampala na maeneo jirani. Maambukizi yakaendelea.

Mkoa wa Kagera ukawekwa katika uangalizi maalum kwa wanaoingia kutoka Uganda. Wataalamu wanatahadharisha, kuna uwezekano wa kusambaa haraka, hasa kwa mguso wa mwathirika na jasho lake.

Picha iliyojengeka mwishoni mwa mwezi uliopita, ilisukuma hatua za ukaguzi mipakani, kwa tahadhari ya kuenea nchini, kwani ndani ya Uganda, homa hiyo imeshaenea kwa kasi kuliko ilivyozoeleka kusikika nchini DRC, penye mzizi wake.

Mkurugenzi Msaidizi Kitengo cha Elimu ya Afya kwa Umma, Dk. Amma Kasangala, anasema serikali haitofunga mpaka kwa sababu kuna shughuli zinaendelea za uzalishaji kwa wananchi, badala yake watajikita kutoa elimu ya kujikinga na virusi hivyo.

Ni ugonjwa unaoenea kati ya binadamu mmoja hadi mwingine kwa kugusana moja kwa moja na maji ya mwili na mazingira machafu. Mazishi yanaweza kuwa hatari hasa ikiwa waombolezaji wanawasiliana moja kwa moja na mwili.

Septemba 20 mwaka huu, mgonjwa wa kwanza aligundulika kuwa na maambukizi ya virusi vya Ebola nchini Uganda na kutangazwa na Wizara ya Afya nchini humo. Hadi mwishoni mwa wiki iliyopita, kulipatikana wagonjwa 54 na kati yao, 25 walishafariki.

Nchini Kenya, pia kuna mgonjwa anayetibiwa na vipimo vyake vinaendelea kuchunguzwa.

Tanzania na Uganda ni nchi jirani ambazo zimepakana kwa karibu na wilaya ya Misenyi mkoani Kagera kwa umbali wa kilometa zaidi ya 200 kupitia mpaka wa Mutukula.

Katika kukabiliana na hatari ya kuenea kwa ugonjwa huo nchini, serikali imeanza kuchukua hatua za kudhibiti watu wanaoingia na kutoka nchini kwa kuwapima kama wana viashiria vya tishio la ugonjwa wa ebola katika mipaka.

Serikali imewekeza nguvu zaidi mkoani Kagera, panapotajwa kuwapo zaidi ya mipaka isiyo rasmi sana inayotumiwa na wakazi kuingia na kutoka nchini.

Mipaka rasmi inatajawa iko saba ambayo tayari serikali imeweka mikakati madhubuti ya kuzuia kuingia kwa ugonjwa huo mchini na tayari timu ya wataalamu chini ya Wizara ya Afya, wameweka kambi mkoani humo kuhakikisha inawekwa mipango sahihi ya kuudhibiti ugonjwa huo.

**MAABARA &UDHIBITI**

Hatua ya kwanza inayochukuliwa na serikali kufunga maabara tembezi kupima virusi vya ebola katika Kituo cha Afya Kabyaire, wilayani Misenyi mkoani Kagera, na hadi sasa imeshatenga hospitali 12 za kuhudumia matibabu ya ebola na yametengwa maeneo maalum, kuweka wagonjwa wa ebola katika vituo vyote vya afya mkoani humo.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Dk. Issessanda Kaniki, anasema serikali imeweka maabara hiyo tembezi ya kupima virusi vya ebola, kutoa elimu kwa jamii na , baadhi ya wadau wa afya, walishauri mipaka inayoingia jirani ya Uganda ifungwe kusiwapo mwingiliano, ila haikuamuliwa hivyo.

Kaimu Mkurugenzi wa Maabara Kuu ya Taifa, Menadi Beyanga, anasema mtambo wa kupima ebola umegharimu zaidi ya milioni 600 hospitalini Kabyaire, pia wamefunga mashine nyingine za kupima magonjwa mbalimbali, ili mgonjwa atakapofikishwa kituoni apate huduma za vipimo vingine na matibabu.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Misenyi, Dk. Daniel Chochole, anasema wameanza kuchukua vipimo vya wanaoingia na kutoka, katika Halmashauri ya Wilaya Misenyi iliyopakana na Uganda, ili kudhibiti kuenea.

Kadhalika, anasema kuna gari la kubebea wagonjwa, ikibainika mwenye dalili, awahishwe katika hospitali iliyoandaliwa kuwahudumia wagonjwa wa aina hiyo.

**MAFUNZO YA WATUMISHI**

Mkurugenzi wa Huduma za Kinga wa Wizara ya Afya, Dk. Beatrice Mutayoba, ameshafungua mafunzo ya siku saba kwa wataalamu wa afya katika halamshauri nane mkoani Kagera, kwa ajili ya kuwajengea uelewa namna ya kujikinga, kubaini na kutibu wagonjwa tajwa.

Anawataka wataalamu hao kuimarisha ufuatiliaj, pia utoaji taarifa kwenye maeneo yenye viashiria vya mlipuko wake. Ni mafunzo yanayotajwa yatawasaidia kutoa elimu kwenye vituo vya afya, ngazi ya jamii wakiwamo watendaji, viongozi kata na vijiji na madereva wa bodaboda na kuziingiza kwenye mfumo.

"Bodaboda ni wasafirishaji wa abiria, wanamtoa sehemu moja kwenda nyingine, hivyo ni kundi muhimu ambalo litasaidia kufichua taarifa za watu watakaohisiwa kuwa na Ebola, hata nchini Uganda ndio walisaidia kuwafichukua," anasema Dk. Beatrice.

Lingine analolitaja, ni kugawa simu maalum watumishi wa Afya 90 ngazi ya jamii, ili zitumike kutoa taarifa za viashiria vya ugonjwa huo na kuingiza taarifa hizo kwenye mfumo maalum wa Wizara ya Afya zihifadhiwe.

**WHO YAJITOSA**

Mtaalamu wa Maabara wa Shirika la Afya (WHO), nchini, Mura Ngoi, anasemaWizara ya Afya imeshakutana na wadau muhimu wa afya pamoja na WHO, kuangalia namna ya kuimarisha utayari kwenye maeneo hatarishi ya kuingia kwa ugonjwa huo.

Anasema, wameshainisha mikoa inayohitaji mahitaji muhimu ya msaada, nguvu kazi na vitendea kazi kwa ajili ya kukinga, kudhibiti kuingia na kuenea ugonjwa huo.

Ngoi anasema, WHO kwa kushirikiana na serikali na kwa uzoefu wao, limejipanga kusaidia kifedha na vitendea kazi katika kudhibiti viashiria vya ugonjwa huo nchini.

**HALI YA CHANJO**

Inatajwa wasiwasi uliopo ni ebola aina ya Sudan, haina chanjo iliyoidhinishwa, tofauti na aina ya kawaida ya Zaire. Hiyo inamaanisha kuwa, hakujawepo na chanjo ya wafanyakazi wa afya, walioshughulikia mikasa iliyothibitishwa.

Ugonjwa wa Ebola- Zaire ulisababisha mlipuko mkubwa zaidi kuwahi kutokea Afrika Magharibi kuanzia Desemba 2013 hadi 2016, zaidi ya watu 11,000 walifariki.

Pia, kuna mikasa 28,000 katika nchi za Guinea, Liberia na Sierra Leone, miaka miwili baadaye, wanasayansi walifanya utafiti na kupata chanjo yake na WHO ilipata kibali chake kutumiwa.

Kwa sasa, Rais wa Uganda Yoweri Museveni, anadems wanajaribu kuchunguza kama chanjo ya Zaire inafaa kutumiwa.

• ***Nimi Mweta na Mary Geoffrey, Bukoba.***




Mashine ya kupima ebola. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

# Wadau Kivule Dar waorodhesha kero na balaa kuzunguka watoto, dada zao

**Na Yasmine Protace**

UNAPOTAJA eneo la Kitunda Kivule, jijini Dar es Salaam, ni eneo lenye sifa kwamba ni nje ya mji, umbali wa kilomita 10 kutoka iliko barabara kuu kati wa Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere na Gongolamboto, eneo la Ukonga Banana.

Zamani palikuwa ukanda uliokuwa na shida ya usafiri, lakini sasa imebadilika ghafla, kuna huduma nyingi za usafiri na hasa daladala, zikiwamo zinazofika mjini, pia zinazoishia Banana, hali kadhalika Kitunda hadi Buza.

Ni eneo linalopata maendeleo kwa kasi, utitiri wa wakazi, biashara na shughuli asilia za ulimaji bustani na kufuga kuku wa mayai, ikiwa na hisa kulisha Dar es Salaam.

**KUTOKA KATA**

Lakini kama ilivyo misemo ya asili 'kizuri hakikosi kasoro', nako hapo kunakabiliwa na habari zisizo njema kwa ustawi wa mwili, hadi saikolojia ya mtoto, kama anavyofafanua Ofisa Mtendaji wa Kata ya Kivule, Ulinduka Mtemi, kwenye mkutano ofisini kwake akilalamika matukio ya ukatili katika kata hiyo, kuwa zao la kukosekana malezi bora kwa watoto.

Anafafanua: "Watoto wanaishi Kama hawana wazazi au walezi,wamejuwa hawapati malezi bora na kujikuta wakihusika katika masuala ya vitendo vya kubakwa,"

Mtemi, anaunganisha kilio chake na haja ya kuongezwa elimu inayotolewa kwa wazazi na walezi, akiwataka kuwa na upendo kwa watoto wao, hata wanapofanyiwa ukatili waweze kuwaeleza uhalisia kuwa 'wamefanyiwa ukatili.'



Baadhi ya washiriki wa kikundi Cha kituo cha taarifa na Maarifa Kivule,wakiwa katika picha ya pamoja walijadili Jambo katika mkutano wa mrejesho wa kuibua changamoto kutoka katika maeneo wanayotoka

Anasema, baadhi ya wazazi wanapokosa ukaribu na watoto, kumechangia sana watoto wanapofanyiwa ukatili, huwa wanakosa pa kuyasemea hata kuchangia ongezeko matukio hayo ya ukatili.

Rai ya Ofisa Mtendaji Kata huyo, ni kila mzazi atumie nafasi yake kuelimisha watoto, ili wajue wanayotakiwa kuyafanya, hata kuisaidia jamii kutoa taarifa pale wanapofanyiwa ukatili.

Anaongeza kuwa, elimu inapaswa itolewe na wazazi kuwasaidia watoto, pale wanapofanyiwa ukatili, hatua ya kuchukua. Ni hoja inayochangiwa na askari polisi (jina tunalo) katika kikao hicho, anayewahimiza wazazi kuwa karibu na watoto wao.



Mwenyekiti wa Kituo cha Taarifa na Maarifa Kivule, Zahara Omary, akielezea jambo. **PICHA ZOTE: YASMINE PROTACE.**

"Watoto wanafanyiwa ukatili mkubwa na hawawaambii wazazi wao na kusababisha kuendelea kuwapo kwa masuala ya ukatili," anasisitiza, akitoa mfano mkasa wa Kivule kwamba kuna kesi iliyojitokeza hapo Kivule, mtoto wa darasa la nne aliyekuwa akifanyiwa ukatili wa kunajisiwa mtu wa miaka 40.

Anasema, mtoto huyo akaieleza polisi namna amekuwa akitoroka shule na kwenda kupika kwa mtu huyo na anapomaliza kupika wanakula na kisha anamnajisi.

"Baada ya kupata taarifa tulimkamata mtu huyo na alipohojiwa alikiri," anasema askari huyo kwa hisia za kuhisi ukakasi, akiwataka wazazi mkutanoni hapo kuwa makini na watoto wao wajenge urafiki na upendo kutoka kwingine.

Mwalimu wa shule ya msingi inayopatikana Kivule, anachangia hoja mkutanoni akisema kuna ukatili unaoendelea kwa wanafunzi, naye anawarudishia wazazi wajibu wa kujikita katika elimu kwa watoto wao wajitambue na kuwalea kwa usahihi na nidhamu.

Analalamika kwamba, watoto wengi wanajilea wenyewe, hali inayotokana na wazazi kutokaa nyumbani muda mrefu wakiwa katika mazingira ya majukumu yao kimaisha, hata kukaribisha ukatili dhidi yao, akitoa mfano: "Baadhi ya wazazi wanawakimbia watoto wao kutokana na kudaiwa vikoba wanaamua kuyakimbia makazi na kuwaachia nyumba watoto."

Mwalimu huyo anatoa mfano wa uhalisia mwingine katika mazingira ya Kitunda Kivule, kwamba kuna wazazi wanaouwatuma asubuhi sana watoto wao kwenda kumwagilia mboga bustanini, huko wanakutana na wanaume 'wabaya' wanaowawafanyia ukatili.

Hali kadhalika, anatumia mfano kwamba kuna watoto wanaofanyiwa ukatili kwa sababu ya wazazi wao wanatumia muda mrefu kwenye biashara, hata wanashindwa kukaa karibu nao muda mrefu.

Pia, anawataja wavulana wanaokabiliwa na madhila ya kulawitiwa hasa katika ngazi ya kidato cha kwanza, moja ya wakala wakuu kwa watoto wote ni simu za mkononi wanazozitumia, ikiwamo kuangalia mambo yasiyofaa.

**KITUO CHA TAARIFA**

Mwenyekiti wa kituo cha Taarifa na Maarifa, Zahara Omary, anasema kikundi chao kilikutana na kuibua changamoto katika maeneo wanayotoka, ili umma ufahamu kinachoendelea na hatua za kukabili, kuziondoa kero zinazofika katika maisha ya kijamii ya kawaida.

Anasema, katika suala la ukatili, anagundua pengo la kukosa elimu ya malezi lina madhara makubwa kwa umma, akitilia mkazo maeneo ya haki za watoto na kijinsia.

Zahara anasema, katika Kituo cha Afya Cha Kivule, wamegundua changamoto ya kukosekana gari la kubeba wagonjwa, akiomba serikali kufikiria haja ya kusaidia.

Anasema, katika baadhi ya shule za Kivule kuna uhaba wa matundu ya vyoo vya kutosha, hali inayowafanya watoto wa kike kupata changamoto na hasa zinazohusiana na kujisitiri wakati wa hedhi, huku shule nyinginezo zikipatikana umbali mrefu.


---

## CHEMSHABONGO NA -00 10 00-

Na Felix Magezi
felixmagezi@gmail.com


Dondoo: Kulia
1. Msemaji
6. kiambaza
9. moyo wa wema
11.hutumiwa na nyuki kuhifadhi asali 12.binadamu
13.ago 16.furahia 19.Muscat ni mji mkuu 20.alikuwa Rais Marekani 21.Ugwe

Chini:
1. hueneza Malaria
2. ubinadamu
3. ondoa maganda ya ndizi
4. kiongozi 5. kitengo maalum cha matangazo ya redio
7. jina la zamani la Tabora
8. Jiji kubwa India
9. mwamuzi wa kesi kortini
10.makazi ya watu wengi
14.jimbo kubwa Marekani
15. jina la kiarabu msichana "Zawadi ya Allah"
17.kabichi kwa kihindi




Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

| | |
|---|---|
| AFRIKA | AGA |
| SHAKA | MLEI |
| AGIZA | DAKA |
| ISRAELI | KIMA |
| KIWANDA | ZAA |
| SAMBAZWA | AMKA |
| ZAIDI | UZAO |
| MAKOSA | OKA |
| KAIDI | KAMA |
| AMAZONI | |
| KANYWA | |
| ADAA | |
| MAZAO | |
| BAADA | |











# TANESCO yatoa tuzo kampuni, taasisi vinara ulipaji bili

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO) Mkoa wa Mbeya limetoa tuzo kwa kampuni na taasisi mbalimbali za umma mkoani humo ambazo zinalipia huduma ya nishati hiyo kwa wakati.

Motisha hiyo ni sehemu ya maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja.

Taasisi zilizokabidhiwa tuzo hizo ni Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya, Kiwanda cha Saruji cha Mbeya, Kiwanda cha Pepsi, Kiwanda cha TBL na baadhi ya hoteli zilizoko jijini hapo.

Meneja wa TANESCO Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Mathias Solongo, alisema shirika hilo limewagawa wateja wake katika makundi mawili ambayo ni wanaolipa ankara kwa wakati na wale ambao nguvu huwa zinatumika kuwadai.

Alisema wateja waliopatiwa tuzo huwa wanalipa ankara zao pale zinapotoka na hawajawahi kuwafuatilia kwa ajili ya kuwadai, hivyo kuwapatia tuzo hizo ni sehemu ya kutambua mchango wao.

**Kwa sasa hospitali hiyo inazidi kupanua huduma zake kwa kujenga miundombinu mipya, kununua vifaa tiba vya kisasa pamoja na kuanzisha viwanda ambavyo vinahitaji umeme wa uhakika.**

Alisema mbali na kuwatembelea wateja hao na kuwagawia tuzo, lakini wamepanga watawatembelea wateja wa kawaida na wale ambao ni wasumbufu katika kulipa ankara ili kuwapa elimu ya umuhimu wa kulipia huduma kwa wakati.

"Tutafanya shughuli mbalimbali ndani ya wiki hii, tutatoa huduma za papo kwa papo kwa wateja wetu na wengine wanaweza wakaomba siku hiyohiyo wakabahatika tukawapelekea huduma siku hiyo hiyo, lakini pia tuna mpango wa kuwatafuta wazee wasiojiweza ili tuwahudumie bure," alisema Mhandisi Solongo.

Alisema watahakikisha wanaitumia wiki ya mteja kuimarisha huduma na uhusiano kati yao na wateja wanaowahudumia bila kujali aina ya mteja.

Baadhi ya wateja waliopatiwa tuzo hizo waliupongeza uongozi wa TANESCO kwa kuendelea kuboresha huduma wakidai kuwa kwa sasa huduma zinazotolewa na shirika hilo ni bora kuliko ilivyokuwa miaka ya nyuma.

Mkurugenzi wa Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya, Dk. Godlove Mbwanji, alisema kwa sasa wanapata huduma bora kuliko ilivyokuwa miaka ya nyuma, akaliomba shirika hilo kuendelea kuboresha huduma hiyo kutokana na ongezeko la matumizi.

Alisema kwa sasa hospitali hiyo inazidi kupanua huduma zake kwa kujenga miundombinu mipya, kununua vifaa tiba vya kisasa pamoja na kuanzisha viwanda ambavyo vinahitaji umeme wa uhakika.

Meneja wa Kiwanda cha Saruji Mbeya, Pamphili Mumwi, alisema kwa sasa kiwanda hicho kinafanya kazi saa 24 kutokana na kuwa na umeme wa uhakika na kwamba hata uhusiano wao na TANESCO umeimarika.

Alisema inapotokea hitilafu yoyote ya umeme maofisa wa shirika hilo huwa wanafika mapema na kuitatua hali ambayo inafanya uzalishaji ndani ya kiwanda hicho kuendelea.




Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (katikati), akikabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 50 kwa viongozi wa kikundi cha umoja wa wakatisha tiketi za mabasi Uyole, jijini Mbeya juzi, ambazo ni mkopo uliotolewa na Taasisi ya Tulia Trust.
**PICHA: NEBART MSOKWA**

## Waiomba serikali kudhibiti upandaji bei ya vyakula

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BAADHI ya wananchi mkoani Mbeya wamesema kuendelea kupanda kwa bei ya vyakula kunasababisha hali ya maisha kuendelea kuwa ngumu, hivyo wameiomba serikali kuangalia namna ya kudhibiti bei hizo.

Waliyasema hayo jana walipozungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti kuhusu hali ya maisha.

Walisema bei ya mafuta imeanza kuleta matumaini lakini bei ya vyakula inazidi kupanda.

Mmoja wa wananchi hao, Elius Simwanza, alisema kwa sasa bei ya mahindi imefikia Sh. 16,000 kwa debe moja huku bei ya mchele ikipaa mpaka Sh. 53,000.

Alisema bei ya mafuta ya kupikia ilikuwa imeshuka mpaka Sh. 5,000 kwa lita lakini kwa sasa yameanza kupanda tena hali ambayo inazidi kuleta ugumu wa maisha.

"Tunashukuru serikali imeweka ruzuku kwenye pembejeo za kilimo hasa mbolea na kwenye mafuta, sasa kinachokera sasa hivi ni bei ya vyakula ipo juu mno, tunaomba serikali itusaidie kudhibiti bei hii," alisema Simwanza.

Alisema kitendo cha mazao hayo kuendelea kupanda kinasababisha baadhi ya wafanyabiashara kuyaficha mazao hayo ili wauze baadaye kwa bei ya juu jambo ambalo alisema linaweza likawaumiza wananchi.

Wilhelmina Mpepo alisema hali ya hewa ya msimu uliopita ndiyo iliyosababisha kupungua kwa mavuno na kufanya machache yaliyopatikana kuuzwa kwa bei ya juu.

Alisema miaka ya nyuma bei ya mchele iliwahi kupanda kwa kiwango kikubwa hali iliyosababisha serikali kuagiza bidhaa hiyo nchini Vietnam kwa ajili ya kudhibiti makali ya bei.

**Bei ya mafuta ya kupikia ilikuwa imeshuka mpaka Sh. 5,000 kwa lita lakini kwa sasa yameanza kupanda tena hali ambayo inazidi kuleta ugumu wa maisha.**

# Waomba hamasa matumizi mbolea asili kwenye kilimo

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

BAADHI ya wananchi wilayani Rungwe katika Mkoa wa Mbeya, wameiomba serikali kuhamasisha matumizi ya mbolea za asili kwenye kilimo ili kutunza mazingira.

Wamesema mbolea za viwandani zina athari kiafya ikiwamo kusababisha magonjwa kana kansa na kupunguza nguvu za kiume, kwamba mbolea za asili hazina madhara yoyote kulingana na elimu ambayo wamekuwa wakipatiwa.

Walitoa ombi hilo juzi wakati maofisa wa Wakala wa Usimamizi wa Misitu nchini (TFS) walipotembelea maeneo mbalimbali yanayozunguka Hifadhi ya Mlima Rungwe kwa ajili ya kutoa elimu ya utunzaji wa mazingira.

Mmoja wa wananchi hao, Nyarusi Mwakalema, alisema mbolea za viwandani zinaharibu mazingira kwa kuongeza tindikali kwenye udongo pamoja na kuua baadhi ya wadudu ambao ni muhimu kwenye udongo kwa ajili ya kurutubisha udongo.

Alisema baadhi ya mbolea hizo zinaharibu viini lishe kwenye mazao hali ambayo inasababisha udumavu kwa watoto, hivyo akaomba wahamasishwe zaidi kutumia mbolea za asili.

"Kwa sasa magonjwa kama kisukari, presha yamekuwa yakiongezeka kwa kasi sana lakini baadhi ya wataalamu wanasema ni kwa sababu ya matumizi ya hizi mbolea zenye kemikali, sasa kwa nini tusihamasishwe zaidi kutumia mbolea za asili?" Alihoji Mwakalema.

Naye Green Mwantonono alisema kwa sasa suala la utunzaji wa mazingira limeshuka kutokana na wananchi kutoshirikishwa vizuri, huku akieleza kuwa hata Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) wenyewe hawafanyi kazi kama ilivyokuwa mwanzo.

Alisema miaka ya nyuma maofisa wa TFS walikuwa wanaweka vizuri mipaka baina yao na wananchi kwa kutengeneza barabara za kuzuia moto kuingia maeneo ya hifadhi, lakini kwa sasa jambo hilo halifanyiki.

Alisema wakati wa kuweka mipaka hiyo walikuwa wanashirikishwa na kwamba utaratibu huo ulikuwa unawafanya na wao kuwa sehemu ya wahifadhi kutokana na kushirikishwa kwenye shughuli hizo.

Mhifadhi Mkuu wa Mazingira Asilia ya Mlima Rungwe, Grace Mwile, alisema Hifadhi ya Mlima Rungwe inapakana na vijiji 39 ambavyo baadhi vipo katika Mkoa wa Mbeya na vingine vipo katika Wilaya ya Makete mkoani Njombe.

Alisema wananchi wa Kijiji cha Ilundo wamekuwa wakishirikiana kwa kiwango kikubwa kutunza mazingira hasa kukabiliana na matukio ya moto ambayo yamekuwa yakitokea mara kwa mara.





# Watoto wenye mahitaji maalum kupata huduma kila kata

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma inapanga kuwafikia watoto wote wenye mahitaji maalum bila kumwacha hata mmoja nyuma kwa kuanzisha kituo cha huduma maalum kila kata.

Hadi sasa watoto wenye mahitaji maalum zaidi ya 829, tayari wameshasajiliwa kwa ajili ya kupatiwa mahitaji yao ya msingi ikiwamo kuandikishwa shule.

Ofisa Elimu Maalum wa Jiji la Dodoma, Issa Kambi, alibainisha hayo alipokuwa akifungua mafunzo kwa wazazi wanaoishi na watoto wenye mahitaji maalum yaliyoratibiwa na Taasisi ya Special Olympics Tanzania.

Kambi, alisema wanataka kuwaandikisha watoto wote ili wapate mahitaji yao yote ya msingi kama ambavyo wengine wanapatiwa.

"Tayari tumeshawasajili watoto 829 na tunaendelea kuwafikia wengine pia tutahakikisha kuwa huduma hizi za mahitaji maalum tunazisogeza kwa kila kata kuwa na kituo chenye wataalamu wenye weledi wa masuala haya," alisema.

**Mafunzo tutakayo fundisha ni pamoja na afya ya kinywa na meno, macho na utimamu wa mwili, lakini tutakuwa na upimaji wa afya na michezo siku ya mwisho kwa watoto hawa wenye mahitaji maalum.**

Pia alisema ili kutoa huduma bora kwa watoto hao, jiji limepanga kuanza kujenga mabweni kwa ajili ya watoto wenye mahitaji maalum.

"Sasa hivi tupo kwenye hatua za mwanzo za uandishi wa maandiko na pia tunaendelea kuweka miundombinu kwenye maeneo ambayo bado hayana kwa ajili watoto wenye mahitaji maalum, tutahakikisha kuwa hakuna mtoto hata mmoja ambaye anaachwa nyuma," alisema Kambi.

Kadhalika, aliwataka wazazi wenye tabia ya kuficha watoto wenye ulemavu kuacha mara moja na badala yake wawatoe na kuwapeleka shule kwa kuwa serikali inaendelea kuboresha miundombinu yao.

"Rai yangu kwa wazazi wote wenye tabia ya kuficha watoto kuacha mara moja kwani watoto hawa kama watapelekwa shule na kufundishwa mambo mbalimbali wanaweza kuwa wazalishaji wazuri katika familia badala ya kuendelea kuwa tegemezi," alisema.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Special Olympics Tanzania, Charles Rays, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwafundisha wazazi masuala ya afya kwa watoto wao.

"Mafunzo tutakayo fundisha ni pamoja na afya ya kinywa na meno, macho na utimamu wa mwili, lakini tutakuwa na upimaji wa afya na michezo siku ya mwisho kwa watoto hawa wenye mahitaji maalum," alisema.

Mjumbe wa Bodi ya Special Olympics, Muharam Mchume, alisema wanaishukuru Halmashauri ya Jiji la Dodoma kwa kuwapa ushirikiano kufanikisha utoaji wa mafunzo kwa wazazi.

Alisema lengo lao ni kuhakikisha kuwa watoto wote wenye mahitaji maalum wanapata haki zao za msingi ikiwamo kusoma badala ya kuendelea kufichwa ndani na wazazi kwa kuwapatia mafunzo ambayo yatasaidia kulinda afya za watoto wao.

Mtaalamu wa Afya ya Kinywa na Meno, Dk. Sophia Mwidri, alisema wanafundisha wazazi namna bora ya kuwasaidia watoto wao kupiga mswaki pamoja na aina ya vyakula ambavyo hawapaswi kuvitumia ili kulinda meno yao.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akipokea tuzo kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan, kwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Dk. Dorothy Gwajima, iliyotolewa na Jukwaa la Mwaka la Mashirika yasiyo ya Kiserikali, lililofanyika jijini Dodoma juzi. Wa pili kulia ni Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la mashirika yasiyo ya kiserikali (NaCoNGO), Dk. Lilian Badi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wadau elimu wafanya tathmini utekelezaji

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WADAU wa Elimu Jumuishi wamejifungia kufanya tathmini ya utekelezaji wa mkakati wa taifa wa elimu hiyo na kutoa maoni kwenye maboresho ya sera na mitaala yanayoendelea nchini ili mahitaji ya kundi hilo yajumuishwe.

Akifungua kikao kazi cha wadau hao jana jijini hapo, Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Francis Michael, alisema lengo la kikao hicho ni kupata uelewa kuhusu mkakati huo wa mwaka 2021/22-2025/26 na kufanya tathmini ya utekelezaji wake kwa mwaka mmoja.

"Kikao hiki pia kutafanyika mawasilisho ya serikali na wadau kuhusu utekelezaji wa mkakati huu na kufanya tathmini kwa mwaka wa kwanza, kugawa kazi za kufanya mwaka wa pili wa mkakati 2022/23 kwa kuangalia mikoa na wilaya ambazo hazina wadau wa Elimu Jumuishi ikiwamo mikoa ya Kigoma, Songwe, Katavi na Rukwa," alisema.

Pia alisema kufanya majadiliano kuhusu miongozo ya ziara ya nyumbani, shule ya nyumbani na wa uanishwaji na usimamizi wa shule maalum na jumuishi na kutoa maoni ya kuboresha sera, mitaala kuhusu elimu hiyo ngazi zote za elimu.

Alisema vikwazo vitakavyobainika kwenye tathmini hiyo wadau watajadili namna ya kuboresha utoaji elimu hiyo.

"Wadau wa elimu jumuishi hakikisheni upatikanaji wa elimu bora kwa wote unazingatia ujumuishi kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum," alisema.

Aliwaomba wadau wa maendeleo waendelee kuona umuhimu wa kuchangia juhudi za serikali kuwapatia huduma stahiki wanafunzi wenye mahitaji maalum ili kushiriki kikamilifu katika kujifunza na kutimiza ndoto zao.

# Kesi kanisa la Anglikana kusikilizwa Oktoba 13

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KESI ya Kanisa la Aglikana Tanzania dhidi ya aliyekuwa Katibu Mkuu wake, Dk. Mecka Ogunde, imepangwa kuanza kusikilizwa Oktoba 13, mwaka huu, baada ya jana Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) kutoa uamuzi mdogo na kukubali maombi ya upande wa mlalamikaji kuleta shauri la msingi.

Uamuzi huo ulitolewa juzi na Msuluhishi Mwandamizi (CMA) Dodoma, Jerome Kato, baada ya kupitia maombi ya upande wa mlalamikaji kuhusu kuleta shauri hilo la msingi.

Akizungumza na waandishi wa habari, wakili wa mlalamikaji, Felician Daniel, alisema wanaishukuru CMA, kwa kukubali maombi yao ya kuleta shauri lao la msingi na kulipangia tarehe ya kusikilizwa.

"Kwa mujibu wa sheria tulipaswa kufungua shauri hili ndani ya siku 30, lakini sisi tulichelewa hivyo tuliwasilisha maelezo yetu na kueleza kwanini tulichelewa, hivyo leo CMA, imetoa uamuzi mdogo wa kuruhusu kuleta shauri letu ambalo ni kufukuzwa kazi kwa aliyekuwa Katibu Mkuu Kanisa Aglikana Tanzania bila kufutwa sheria," alisema Daniel.

Kadhalika, alisema baada ya uamuzi huo wanakwenda kujipanga kwa ajili ya kuanza kwa shauri hilo ambalo limepangwa kusikilizwa Oktoba 13, mwaka huu.

"Leo tumepatiwa uamuzi huu na Msulushi Mwandamizi CMA, mheshimiwa Kato na kukubali kuwa tarehe hiyo shauri hili kuanza kusikilizwa, upande wa mlalakiwa leo hawajafika hivyo tunafuatilia samansi kwa ajili ya kuwapelekea kuja kwa ajili ya kuanza rasmi kwa shauri hili," alisisitiza Wakili Daniel.

Dk. Ogende alifungua shauri CMA, kulishtaki Baraza la Wadhamini wa Kanisa Aglikana Tanzania baada ya kufukuzwa kazi bila kufuata sheria na kumnyima stahiki zake.

Julai 27, mwaka huu, akizungumza na waandishi wa habari wakili wa mlalamikaji Willison Ogunde, alisema shauri walilofungua ni CMA/DOM/84/2022 na mteja wake ambaye alikuwa Katibu Mkuu wa Kanisa Aglikana Tanzania analalamikia ajira yake kusitishwa bila kufuatwa sheria.

Kutokana na shauri hilo upande wa mlalamikiwa walileta hati kinzani, mapingamizi ambayo upande wa mlalamikaji waliomba muda kwenda kuyapitia ili kuja kutolea majibu.

Agosti 10, mwaka huu, pande zote zilitoa maelezo yao mbele ya Msuluhishi Mwandamizi (CMA), Mkoa wa Dodoma, Rodney Matalis, ambaye alitoa uamuzi wake Agosti 26, mwaka huu kwa kuyatupilia mbali mapingamizi hayo.

Mgororo huo ulianza baada ya Baraza la Wadhamini wa Kanisa hilo kumwondoa madarakani kwa madai ya kuwa nje ya ofisi kwa muda mrefu mapema mwezi Juni, mwaka huu.

Hata hivyo, kwa mujibu wa Dk. Ogunde, alilazimika kufungua kesi kulishtaki baraza hilo baada ya kushindwa kufikia makubaliano na uongozi wa kanisa kuhusu stahiki zake.



# Viongozi wa dini waomba ushirikiano kupambana vitendo vya udhalilishaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

VIONGOZI wa dini wameiomba jamii kuwaunga mkono na kushirikiana nao katika jitihada wanazofanya za kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia.

Wakizungumza jana katika mkutano wa kutathmini juhudi za kupambana na vitendo hivyo uliofanyika mjini hapo, walisema wanatumia mahubiri ya dini wakiwa katika nyumba za ibada kupinga vitendo hivyo, lakini licha ya juhudi hizo bado watoto na wanawake wanaendelea kudhalilishwa.

Akizungumza katika mkutano huo, Shekhe Masoud Makame Haji, kutoka Kisiwa cha Tumbatu Kaskazini Unguja, alisema wana utaratibu wa kutumia hotuba za Ijumaa, mawaidha, ziara za madrasa, lakini jitihada hizo zinahitaji kuungwa mkono na jamii.

Amina Yusuf Ramadhani, mwanaharakati wa kupinga vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia, ameviomba vyombo vya sheria kuwa makini katika ufuatiliaji wa kesi hizo kwa sababu kumeibuka wimbi la kubambikiziana kesi za udhalilishaji.

"Pia kuna tatizo la kulipiziana visasi na kuzifanya kesi hizo kuwa kama biashara jambo ambalo linaongeza ugumu katika mapambano hayo," alisema.

Alitaka jamii kurudisha malezi ya zamani ya kuwa 'mtoto wa mwenzio ni wako' na pia kutowaacha huru kupitiliza watoto kwasababu athari atakayoipata mtoto akidhalilishwa hailipiki kwa adhabu yoyote atakayopewa mtuhumiwa.

Akifungua mkutano huo, Mkurugenzi wa Idara ya Wazee na Ustawi wa Jamii, Abdallah Saleh Omar, alisema lengo la mkutano huo ni kubaini mafanikio na changamoto zilizojitokeza katika kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia.

Abdallah alipongeza juhudi za viongozi hao wa dini katika kupambana na vitendo vya udhalilishaji na kufikisha ujumbe katika jamii.

Jumla ya wilaya nane za Unguja ikiwamo wilaya ndogo Tumbatu zimewasilisha taarifa za utekelezaji kwa kipindi cha Julai-Septemba na kuwasilisha mpango kazi wa utekelezaji kwa kipindi kinachofuata cha Oktoba - Desemba ambao unasimamiwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto kwa ushirikiano wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA).

**Pia kuna tatizo la kulipiziana visasi na kuzifanya kesi hizo kuwa kama biashara jambo ambalo linaongeza ugumu katika mapambano hayo.**

# CHADEMA yasema iko tayari kumsaidia Mwinyi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Salum Mwalimu, amesema kuwa viongozi wa vyama vya siasa wapo tayari kumsaidia Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kuijenga Zanzibar mpya isiyokuwa na utumwa wa kihistoria ya ubaguzi na uhasama.

Aliyasema hayo juzi wakati akizungumza katika mkutano wa wadau wa demokrasia kujadili masuala mahsusi ya Zanzibar yanayohusu demokrasia ya vyama vingi vya siasa uliofanyika mjini hapo ambao ulifunguliwa na Rais Mwinyi.

Alisema changamoto kubwa ni kutengeneza kizazi kipya na imara ambacho kilizaliwa baada ya mapinduzi ya mwaka 1964 kitakachoenzi yale yote yalioasisiwa na viongozi waliotangulia na kuwa tayari kuitengeneza Zanzibar mpya.

**Lazima kila mmoja awe mzalendo wa nchi ili kuwa na mustakabali mzuri kwa wananchi katika kujenga umoja na mshikamano na kulinda amani ya nchi iliyoko.**

"Lazima kuitengeneza Zanzibar mpya isiyokuwa na utumwa wa kihistoria unaotugawa, unaoendeleza ubaguzi, chuki na jamii ya kuhasimiana na kila wakati tunarudi katika miafaka ya maridhiano," alisema.

Alisema wapo tayari kumsaidia Rais kutimiza dhamira yake katika kuijenga Zanzibar moja yenye ustawi na isiyo jirudia katika changamoto za kisiasa.

Alisema muono wake kuwa katika kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 itakwenda kuzaa Zanzibar mpya isiyokuwa tena na mifarakano ya kisiasa chini ya uongozi wa Dk. Mwinyi.

Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha ACT-Wazalendo, Ismail Jussa Ladhu, alisema kujitahidi kueleza historia ya Zanzibar katika misimamo ya ukweli na sio misingi ya kuendeleza mgawanyiko, chuki na uhasama.

Alisema hatua hiyo itasaidia kuepusha mambo na kujenga umoja wa Wazanzibari.

Alisema kuna hatua zilifanyika katika mariadhiano ya kisiasa, lakini mafanikio yaliyopatikana yalisita mwaka 2015 na Zanzibar inahitaji tume makini ya kusimamia muafaka wa kimaridhiano na mengine mengi ambayo yanalalamikiwa.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha ADC, Hamad Rashid Muhammed, alisema lazima kila chama kiheshimu ajenda za kitaifa na kuacha kupandikiza chuki za kisiasa.

Aidha, viongozi hao walisema lazima kila mmoja awe mzalendo wa nchi ili kuwa na mustakabali mzuri kwa wananchi katika kujenga umoja na mshikamano na kulinda amani ya nchi iliyoko.




Mkurugenzi wa Bodi ya Korosho Tanzania, Francis Alfred (kulia), akizungumza mjini Zanzibar jana, baada ya kuzindua usafirishaji wa kontena la kwanza lenye korosho zilizobanguliwa na Kampuni ya Word Holding Tanzania, kwenda Marekani. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# ZATU yaunga mkono mageuzi ya elimu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA cha Walimu Zanzibar (ZATU), kimesema kinaunga mkono jitihada za serikali katika kusimamia mageuzi ya elimu.

Hayo yalisemwa jana na Katibu Mkuu wa chama hicho, Haji Juma Omar, akizungumza na waandishi wa habari, ofisini kwao Mwanakwerekwe kuhusu Siku ya Walimu Duniani ambayo hufanyika kila mwaka Oktoba 5 na kwa Zanzibar itafanyika Oktoba 6, mwaka huu, kituo cha Mafunzo ya Amali huko Mkokotoni Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Hata hivyo, alisema mwalimu ni nyenzo muhimu katika maendeleo ya elimu na bila ya kuimarisha mifumo inayosimamia taaluma, haki na maslahi ya walimu ni vigumu kufikia lengo la serikali la kutoa fursa ya elimu bora kwa wote.

Alisema katika kufanya mageuzi hayo ZATU inaamini kuwa utekelezaji wa uanzishwaji wa Tume ya Utumishi ya Walimu utapewa kipaumbele kama ilivyoelekezwa katika mipango ya serikali ikiwamo Sera ya Elimu ya 2006 na Mpango wa Maendeleo ya Elimu Zanzibar (ZEDP II).

"Kwa mfano katika ZEDP II, mpango wa elimu ukurasa wa 56 umeweka wazi kuwa ili kuinua sifa na hadhi ya ualimu na ubora wa elimu, kunahitajika kuanzishwa kwa Tume ya Utumishi ya Walimu," alisema Omar.

Aidha, alisema ni matumaini yao kuwa jambo hilo litafanyiwa kazi kwa haraka kutokana na umuhimu wake.

Alisema siku ya walimu hufanyika kwa lengo la kuimarisha hadhi ya mwalimu kulingana na mapendekezo ya Shirika la Kazi Duniani (ILO) na Shirika la Elimu ya Sayansi na Utamaduni (UNESCO).





# Maelfu ya wananchi Shy wanufaika mradi wa maji

**Na Marco Maduhu**, SHINYANGA

WANANCHI 3,800 wa Kijiji cha Mwandutu wilayani Shinyanga, wameondokana na shida ya kutumia maji machafu ambayo yanahatarisha afya zao baada ya mradi wa majisafi na salama kutoka Ziwa Victoria kukamilika na kuanza kutoa huduma.

**Mradi huo utanufaisha wananchi 3,800, umegharimu Sh. milioni 305.**

Walisema kabla ya mradi huo walikuwa wakitumia maji ya kwenye visima na mabwawa ambayo sio salama kiafya na wakati mwingine walichangia na mifugo.

Walibainisha hayo juzi wakati wa ziara ya Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, kijijini humo kuona utekelezaji wa mradi huo.

Mmoja wa wananchi hao, Rahel Rutonja, alisema mradi wa majisafi na salama ni mkombozi kwa afya zao na kwamba kwa sasa wataondokana na matumizi ya maji machafu ambayo walikuwa wakitumia hapo awali.

"Kabla ya mradi huu tulikuwa tukitumia maji ya kwenye visima na mabwawa na wakati mwingine unakuta mifugo imeshavuruga maji hayo na kuacha vinyesi vyao, lakini kutokana na shida ya maji inabidi kuyachota tu na kwenda kutumia hivyo hivyo," alisema Rutonja.

Mwenyekiti wa kijiji hicho, Mwandutu Mashaka, alisema mradi huo utanufaisha wananchi 3,800.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, alipongeza Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira (RUWASA), kwa kutekeleza mradi huo kwa kasi kama alivyotoa maagizo yake ambao umeanza kuhudumia wananchi.

Aliwataka wananchi kuvuta maji hayo majumbani mwao na kumtua mwanamke ndoo kichwani.

Aidha, aliwatahadharisha wananchi hao wasitumie vishoka wakati wa kuvuta maji hayo kwa kuwa kufanya hivyo wataharibu miundombinu ya mradi huo pamoja na kutapeliwa pesa zao.

Kaimu Meneja wa RUWASA, wilayani Shinyanga, Andrew Mogella, alisema mradi huo umegharimu Sh. milioni 305.



Mhandisi Mwandamizi wa Mgodi wa Bucreef, Erick Yohana (wa pili kulia), akizungumza na waandishi wa habari katika ofisi za mgodi huo, Kijiji cha Lwamgasa, Mkoa wa Geita jana, kuhusu ushiriki wa wachimbaji wadogo na wakubwa katika maonyesho ya teknolojia ya sekta ya madini yanayoendelea mkoani humo: **PICHA: JOCTAN NGELLY**

# Mbunge aonya wanaoozesha wanafunzi

**Na Shaban Njia**, KAHAMA

MBUNGE wa Jimbo la Ushetu, Emmanuel Cherehani, amewaonya wazazi na walezi katika Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga wanaowaozesha wanafunzi wa kike wanaohitimu kidato cha nne kwa tamaa ya kujipatia ng'ombe na fedha.

Cherehani alitoa onyo hilo jana kwenye mahafali ya 23 ya Shule ya Sekondari ya Mweli iliyoko Kata ya Ushetu na kwamba serikali itachukua hatua kali za kisheria kwa mzazi au mlezi atakayebainika kujihusisha katika kuozesha mwanafunzi kinyume cha sheria.

Alisema wanafunzi wa kike wanapohitimu elimu ya kidato cha nne hususani vijijini huozeshwa kwa lazima na wazazi wao na kuwakatisha ndoto zao za kufikia malengo yao ya kielimu waliojiwekea kutokana na kujiingiza kwenye ndoa wakiwa wadogo.

"Ipo haja kwa viongozi wa vijiji na kata kuhakiki ndoa zinazofungwa katika maeneo yao katika msimu huu ili kujiridhisha waolewaji kama sio wanafunzi, katika uongozi wangu sitakubali kuona mwanafunzi anakatishwa masomo kwa kuozeshwa kwa tamaa za baadhi ya wazazi wasiokuwa waadilifu," alisema Cherehani.

Alisema, serikali imekuwa ikiboresha miundombinu katika sekta ya elimu kuhakikisha mtoto wa kike anasoma na kutimiza ndoto zake na kuwataka wazazi kujiepusha na vitendo hivyo vya jinai na watakaobainika watawajibika kisheria ikiwa ni pamoja na kufikishwa mahakamani.

Kwa upande wake, Ester Sango, mwanafunzi wa kidato cha nne katika shule hiyo, aliomba serikali kuwachukulia hatua wazazi na walezi watakaobainika kuwaozesha watoto wao waliofaulu kuendelea na masomo kwa tamaa za kutaka mali ili kuondoa ndoa za utotoni.

Alisema wazazi wao wanapokea mahari watoto wao wakiwa shuleni na wanapohitimu kabla ya matokeo kutangazwa wanalazimishwa kuolewa na mwanaume ambaye hajamchagua na kuonya kitendo hicho sio cha kiungwana.

# Serikali yaagiza wachimbaji wadogo watambuliwe

**Na Alpionce Kabilondo**, GEITA

NAIBU Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini, Msafiri Mbibo, ameziagiza taasisi za madini zilizo chini ya wizara yake zinawasaidia wachimbaji wadogo wa dhahabu ili watambulike katika shughuli zao.

Alitoa kauli hiyo hivi karibuni wakati akifungua mafunzo kwa machimbaji wadogo wa madini ya dhahabu mkoani Geita wanaoshiriki kwenye maonesho ya kimataifa ya teknolojia na uwekezaji sekta ya madini yanayoendelea mjini Geita.

Msafiri alisema sekta ya madini ni muhimu katika taifa lolote duniani na kuongeza kuwa kuna manufaa makubwa kwenye madini.

"Watanzania hatuna budi kujipanga na kunufaika zaidi na rasilimali na wachimbaji wadogo hawawezi kuwa wadogo, lazima wawe wakubwa kwani hata wakubwa kwa sasa siku za nyuma walikuwa wadogo," alisema.

Aliwataka wachimbaji kupeleka taarifa kwenye taasisi za umma ili waweze kuaminika na kupata mikopo benki na kwamba bila kufanya hivyo ni vigumu kuaminiwa na kukopesheka.

Aidha, alisema serikali itaendelea kuimarisha taasisi yake ya utafiti wa madini GST ili iweze kuwasaidia wachimbaji wadogo waweze kuondokana na uchimbaji madini kwa kubahatisha.

Pia alisema umefika wakati sasa wachimbaji hao kuyageuza mafunzo hayo wanayopata kuwa chachu kwao kwa kujua sheria mbalimbali zinazowaongoza na namna ya matumizi ya kemikali za uchenjuaji na uchakataji madini.

Mkuu wa Wilaya ya Geita, Wilison Shimo, akimkaribisha Katibu Mkuu, alisema kuwa Ofisi ya Tume ya Madini Mkoa wa Geita inakabiliwa na uhaba wa watumishi pamoja na usafiri wa magari hali ambayo imekuwa ikisababisha maofisa wake kushindwa kufika kwenye maeneo ya uzalishaji wa madini.

Kaimu Ofisa Madini Mkoa wa Geita, Martine Shija, alisema wachimbaji wadogo wanalipa zaidi ya Sh. bilioni 40 kwa mwaka kama kodi ya serikali.

Mwenyekiti wa Chama cha Wachimbaji Mkoa wa Geita, Gerema Kadeo, alisema mkoa huo una wachimbaji wadogo zaidi ya 25,000 na leseni 1,000 za uchimbaji.

# OPEC+ kupunguza uzalishaji mafuta

**VIENNA, Austria**

NCHI zinazoongoza katika uzalishaji mafuta zikiongozwa na Saudi Arabia na Russia zinazojulikana kama OPEC+, zinatarajiwa kukutana mjini Vienna, huku ripoti zikidokeza kuwa zinatafakari kupunguza uzalishaji mafuta kwa mapipa milioni mbili kila siku katika jitihada za kuongeza bei inayoshuka.

Ikiwa hatua hiyo itatekelezwa basi itakuwa punguzo kubwa la kwanza tangu, mpango mkubwa wa kupunguza uzalishaji uliowekwa mwanzoni mwa janga la COVID-19.

Bei ya mafuta ilipanda baada ya Russia kuivamia Ukraine mapema mwaka huu na kusababisha mfumuko wa bei kuongezeka katika kiwango ambacho hakijashuhudiwa kwa miongo mingi ulimwenguni.

Lakini katika miezi ya hivi karibuni, bei ya mafuta imeanza kushuka kufuatia wasiwasi kwamba mahitaji yamepungua pamoja na kudorora kwa uchumi wa ulimwengu.

Nchi nyingi ambazo zinanunua mafuta, zimekuwa zikishinikiza kundi hilo la OPEC+ kuongeza uzalishaji ili kupunguza bei ambayo imepanda, lakini miito hiyo imepuuzwa pakubwa.

**DW**

**Bei ya mafuta ilipanda baada ya Russia kuivamia Ukraine mapema mwaka huu na kusababisha mfumuko wa bei kuongezeka katika kiwango ambacho hakijashuhudiwa kwa miongo mingi ulimwenguni.**

# Russia yaonya upelekaji silaha Ukraine, yadai mapigano kamili na ulaya yananukia

**WASHINGTON, Marekani**

RUSSIA imeonya kwamba uamuzi wa Marekani wa kutuma msaada zaidi wa kijeshi nchini Ukraine, unaongeza hatari kuwepo mapigano ya moja kwa moja na nchi za Magharibi.

Balozi wa Russia nchini Marekani, Anatoly Antonov, alisema ni tishio la moja kwa moja kwa nchi yake na kwamba Marekani ni mshiriki wa mzozo huo.

Hapo awali, Marekani ilitangaza msaada mwingine wa kijeshi wa dola milioni 25 kwenda Ukraine.

Msaada wa silaha za kisasa kutoka Marekani zimesifiwa kwa kuisaidia Ukraine kuongeza kasi ya mashambulizi dhidi ya maeneo yanayokaliwa na majeshi ya Urusi. Wanajeshi wa Ukraine wamepata maendeleo makubwa kaskazini-mashariki na kusini mwa nchi hiyo katika wiki za hivi karibuni.

Vifaa vilivyotolewa hivi karibuni vya Marekani pamoja na mifumo mingine minne ya roketi yenye usahihi wa hali ya juu ya Himars vimeisaidia Ukraine.

Mpaka sasa Marekani imetoa msaada karibu wa dola bilioni 17 wa kijeshi kwa Ukraine tangu Rais wa Russia, Vladimir Putin kuamuru kuivamia Ukraine Februali 24 mwaka huu.

Antonov alionya kwamba uamuzi wa Marekani kuendelea kusaidia utawala wa Ukraine kwa silaha nzito unalihakikishia taifa hilo kuwa mshiriki wa mzozo huo.

" Silaha hizo zitasababisha umwagaji damu wa muda mrefu na majeruhi wapya" alisema Antonov.

"Tunatoa wito kwa Marekani kuacha vitendo vyake vya uchochezi ambavyo vinaweza kusababisha athari mbaya zaidi," aliongeza kusema balozi huyo wa Russia.

Russia imeapa kujilinda kwa njia zote zinazopatikana bila kukataa matumizi ya silaha zake za nyuklia.

Hata hivyo, nchi hiyo inasonga mbele na majaribio yake ya kunyakua mikoa minne ya Ukraine ya Donetsk na Luhansk upande wa mashariki, Kherson na Zaporizhzhia upande wa kusini.

Onyo la Antonov linakuja muda mfupi baada ya Rais wa Marekani Joe Biden, na Makamu wa Rais Kamala Harris kujadili ushirikiano zaidi wa kijeshi na Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky.

Ikulu ya White House ilisisitiza kwamba Marekani haitatambua kamwe hatua ya Russia inayodaiwa kunyakua eneo la Ukraine.

**NDEGE ZA IRAN ZATUMIKA**

Vituo vya redio na machapisho kadhaa ya mtandao wa telegram vinaripoti kutokea kwa milipuko katika mji wa Kyiv na Tserkva.

Waandishi wa chaneli zingine za telegraph walieleza kwamba mashambulizi hayo yalifanywa kwa kutumia ndege zisizo na rubani kutoka Iran zilizopewa jina la Geran.

Kulingana na Video zinazoonekana kwenye mitandao ya kijamii hakuna kinachoonekana (usiku), lakini unaweza kusikia, kulingana na wanablogu, sauti ya injini za propeller za ndege zisizo na rubani za Irani na kisha milipuko.

Hatahivyo haijulikani ndege hizo zisizo na rubani zilikuwa na malengo gani na iwapo zilifanikiwa .

**UKRAINE YASONGA MBELE**

Vikosi vya Ukraine vimevikomboa vijiji muhimu katika eneo la kusini la Kherson, na kuwafurusha wanajeshi wa Russia.

Wizara ya Ulinzi ya Ukraine, ilichapisha video inayoonyesha kikosi cha 35 cha wanamaji wakipandisha bendera ya Ukraine juu ya jengo la Davydiv Brid, huku kukiwa na ripoti za vijiji vingine kadhaa vya karibu kurudishwa mikononi mwao.

Vikosi vya Russia vimelazimika kurudi nyuma kaskazini-mashariki mwa Ukraine.

Rais Vladimir Putin alitakiwa kutia saini amri ya kutwaa maeneo manne ya Ukraine, huku vita vikiendelea katika pande zote.

Unyakuzi huo hauna uhalali chini ya sheria za kimataifa na Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky, alitangaza kuwa ni batili.

Rais Joe Biden alizungumza na Zelensky juzi na kumhakikishia Marekani kamwe haitatambua unyakuzi wa Russia.

Russia bado inadhibiti mji wa Kherson, mji mkuu wa kikanda, kusini. Lakini mtego wake unazidi kutetereka katika eneo lote la kaskazini mwa Mto Dnieper, unaojulikana kama Dnipro kwa Kiukreni.

Katika saa 48 zilizopita, vikosi vya Ukraine vilisonga kusini kando ya ukingo wa magharibi wa mto, na vitengo vya nchi hiyo vimelazimika kujiondoa kutoka kwenye makazi kadhaa kaskazini mwa mkoa wa Kherson.

***BBC***



Mtambo wa kurusha roketi aina ya BM-21 'Grad' ukifyatua makombora kwenda maeneo ya Russia katika eneo la Kharkiv juzi. **PICHA: AFP**

# Ecowas yaridhishwa na Burkina Faso

**OUAGADOUGOU, Burkina Faso**

UJUMBE wa nchi za Jumuiya ya Afrika Magharibi ambao ulikwenda kufanya tathmini nchini Burkina Faso baada ya kutokea mapinduzi, umeeleza umeridhishwa na hali ilivyo.

Rais mpya wa nchi hiyo, Kapteni Ibrahim Traoré, kiongozi wa kijeshi ambaye siku ya Ijumaa alimpindua Luteni Kanali Paul-Henri Damiba, alikutana na ujumbe huo na kufanya mazungumzo.

Damiba alipinduliwa baada ya kuingia madarakani kwa kufanya mapinduzi mwezi Januari.

Ujumbe wa kiongozi huyo mpya ulikutana katika uwanja wa ndege wa Ouagadougou ambako kulikuwa na waandamanaji waliokuwa wakitoa wito wa ushirikiano zaidi na Russia na kupinga Ufaransa.

Rais wa zamani wa Niger Mahamadou Issoufou, ambaye alikuwa sehemu ya ujumbe wa Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika Magharibi (Ecowas) kama mpatanishi, alisema watasimama pamoja na watu wa Burkinabe katika masaibu magumu wanayopitia.

***BBC***

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

Magistrates Court( Approved Forms For the Primary Court)
GN. NO 943(Contd.)

FOMU MIRATH -2

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Wilaya ya Moshi**
**Kituo cha Moshi Mjini Mkoa Kilimanjaro**
**Usimamizi wa mirathi Na 178 /2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU MONICA CORNEL SAMAGWA WA MSARANGA, MANISPA YA MOSHI MJINI KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUWA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA GOODLUCK JOSEPH MUSHI**

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote /maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 18 Mwezi 10 Mwaka 2022 Kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo,

**Zingatia :**

Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
*Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na wawea kukaguliwa.
*Marehemu hakuacha wosia
Imetolewa leo tarehe 30 Mwezi 09 Mwaka 2022

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
MOSHI - MJINI

## KUPOTEA KWA CHETI



**BARAKA MAJALI ABDUL** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1522/0052/2018** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **SCOLASTICA SECONDARY SCHOOL** mwaka **2018**. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: DAR/KIL/RB/394394/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**HAMIS MSHINDO HAMISI** anatangaza kupotea kwa cheti cha chuo chenye usajili namba **2017-04-12173** kilichotolewa na **CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM** mwaka **2020**. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA:DAR/CHU/RB/394642/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PATRICIA MORIS BURURE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Toyota Raum yenye namba za usajili **T799 DPX,** Chasis namba **NCZ200060259** na Engine namba **1NZB390576.** Kwa yeyote atakayeiona au kuiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **MAN/BAB/RB/394309/2022.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA YA MOROGORO MJINI**
**MKOA WA MOROGORO**
**SHAURI LA NDOA Na 54/....2022**
**JINA LA MDAI: EMMANUEL EDWARD KIJO**
**JINA LA MDAIWA: JUDITH GODFREY MACHIMO**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu madai katika Mahakama za Mwanzo)**

Kwa:**JUDITH GODFREY MACHIMO................MDAIWA**

Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba:Kuomba kuvunja mahusiano na kupatiwa talaka. Kwa hiyo unatakiwa Kuhuduria binafsi katika mahakama hii tarehe 15/10/2022 saa 08:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:**Kama hautohudhulia siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitishwa kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,mahakama inaweza kusikiliza shauri hili bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 29/09/2022

HAKIMU


# OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

## KWA HABARI MOTOMOTO USIKOSE GAZETI LAKO LA NIPASHE KILA SIKU

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.




# JOLIE AMFUNGULIA KESI NYINGINE PITT

**LOS ANGELES, Marekani**

MKALI wa muvi za Hollywood, Angelina Jolie, amefungua shauri lingine mahakamani akimshutumu aliyekuwa mumewe, mwigizaji Brad Pitt, kwa kumshambulia yeye na watoto wao kwa ulevi wakati wa safari ya ndege binafsi na kumfanya aombe talaka.

Jolie amesema Pitt alimsukuma kichwa na kuwashambulia watoto wao wawili huku akitukana na kuwamwagia pombe wakati wa safari ya kutoka Ufaransa kuelekea Los Angeles, mwaka 2016 na madai yamepingwa vikali na Pitt.

Wawili hao walidumu kwenye mahusiano ya mapenzi kwa miaka 10 kabla ya kuchumbiana mwaka 2012 na kufunga ndoa mwaka 2014 na hatimaye kutalikiana Septemba, 2016.

Chanzo kilicho karibu na Pitt kiliiambia BBC madai ya Jolie yalikuwa ya uongo.

"Anatakiwa kusahihisha na kufikiria upya maelezo yake ya tukio lililotokea, anaongeza taarifa zisizo za kweli kabisa kila anaposhindwa kupata anachotaka," chanzo hicho kilimnukuu Pitt.

"Kila siku madai yake yanaendelea kubadilika."

Madai ya Jolie ya tabia mbaya ya Pitt katika safari ya ndege ya Septemba 14, 2016 yamejitokeza katika shauri la awali la mahakama, ikiwa ni pamoja na suluhu ya talaka ya wenzi hao wa zamani walioshinda tuzo ya Oscar.

Shauri hilo lilifunguliwa katika kesi ya Jumanne mjini Los Angeles na timu ya wanasheria ya Jolie.

Pia kuna kesi inayoendelea kuhusu nyumba na shamba la mizabibu walilonunua wote lililoko katika eneo la Chateau Miraval SA, Kusini mwa Ufaransa.

Pitt amekuwa akibainisha wazi yeye na mke wake huyo wa zamani walikuwa wamekubaliana kutouza hisa zao katika mali zao bila idhini ya mmoja wapo, kitu ambacho Jolie anakipinga.

Lakini sasa shauri lililofunguliwa Jumanne limeongeza madai mengine ambapo Jolie amesema mume wake huyo wa zamani alikuwa akimnyanyasa kimwili na kihisia yeye na watoto wao sita – ambao walikuwa na umri kati miaka 8 hadi 15 wakati huo.

## ZUCHU ALILIA UJAUZITO

**Na Mwandishi Wetu**



NYOTA wa kike wa muziki wa Bongofleva, Zuchu ameonyeshwa kusikitishwa na kitendo cha paka wake kupata mimba wakati yeye hana.

Zuchu ambaye jina lake halisi ni Zuhura Othman, amezusha taharuki hiyo kwenye ukurasa wake wa Instagram akidai yeye hana, lakini paka wake ana mimba.

Msanii huyo ambaye tetesi zinamhusisha kutoka kimapenzi na bosi wake, Diamond Platnumz amesema kitendo hicho kimemdhalilisha kwa sababu ataonekana hajui kulea.

"Yaani paka wangu wameshampa mimba sasa hivi, mimi mama yake sina mimba, lakini yeye amepata mimba, kwa nini? Amenidhalilisha sana, ninaonekana mama gani mimi ambaye sijui kulea," aliandika Zuchu.

Baadhi ya wafuasi wake, wamemwomba ambebee ujauzito Diamond maana akichelewa sana atakuta mwana si wake.

## STAMINA AWASHUKURU MASHABIKI KWA TUZO

**Na Mwandishi Wetu**



MSANII wa Bongofleva, Stamina amewashukuru mashabiki wake kwa kumpigia kura baada ya kutangazwa mshindi wa tuzo ya PSMA katika kipengele cha Msanii Bora wa Hip Hop/Rap kwenye Ukanda wa Afrika Mashariki.

Tuzo hizo zilitolewa usiku wa kuamkia Jumamosi jijini Bujumbura, nchini Burundi na kuwashirikisha wasanii kutoka nchi mbalimbali za Afrika Mashariki.

Kupitia Instagram yake Stamina ameandika "Usiku wa Jumamosi nilitakiwa niwe Burundi katika usiku wa utoaji tuzo za PSMA, sema ratiba zikaingiliana na Fiesta ya Mwanza.

Napenda kutoa shukrani za dhati kwa mashabiki zangu wote walionipigia kura na wadau waliosapoti bila kuwasahau waandaaji wenyewe. Ushindi umerudi nyumbani Tanzania…na sasa ni Msanii Bora wa Rap/Hip Hop wa Afrika Mashariki katika tuzo za Burundi."

# SERENGETI BOYS, ETHIOPIA KUFUNGUA DIMBA CECAFA

**Na Saada Akida**

TIMU ya Soka ya Taifa ya Vijana wenye umri chini ya miaka 17 (Serengeti Boys) wanatarajia kukutana na wenyeji Ethiopia katika mchezo wa kwanza wa mashindano ya kuwania kufuzu fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON-U17) utakaochezwa leo jijini Addis Ababa, nchini humo.

Mashindano hayo yameanza kutimua vumbi juzi na ndio yatakayotoa wawakilishi wa CECAFA katika fainali za michuano hiyo zitakazofanyika Algeria, hapo mwakani.

Mechi hiyo kati ya Serengeti Boys itafanyika kwenye Uwanja wa Abebe Bikila na itatanguliwa na mchezo kati ya yosso kutoka Uganda dhidi ya wenzao wa Sudan Kusini.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Serengeti Boys, Kim Poulsen, alisema wamefanya maandalizi ya kutosha kuelekea mchezo huo na watapambana kuhakikisha wanaanza vyema mashindano hayo.

Poulsen alisema wachezaji wote wapo katika hali nzuri, kila mmoja anatambua umuhimu wa kushinda mchezo huo ambao anaamini utakuwa na ushindani mkubwa.

"Tumejiandaa vyema kuhakikisha tunafanya vizuri katika mashindano haya, tunaamini kila mchezaji atafuata kile ambacho tumekifundisha tukiwa kwenye mazoezini," alisema Poulsen.

Kocha huyo aliongeza mazoezi ya muda mrefu waliyofanya yanawapa imani ya kusonga mbele kwenye hatua inayofuata katika mashindano hayo yanayoshirikisha mataifa sita ya nchi wanachama wa CECAFA.

Nahodha wa Serengeti Boys, Omary Hassan, alisema kila mchezaji anatambua umuhimu na kushinda mchezo huo huku wakikumbushana kila wakati kupambana na hatimaye kufikia malengo waliyonayo.

Hassan alisema wanawaomba Watanzania wawaombee dua njema kwa sababu wao wanafahamu wanatakiwa kuwapa furaha na si jambo lingine.

Serengeti Boys iliyoko katika Kundi A itashuka tena dimbani Oktoba 9, mwaka huu kucheza dhidi ya Somalia. Kwa mujibu wa ratiba ya CECAFA, Kundi B linaundwa na Uganda, Burundi na Sudan Kusini.



Wachezaji wa Simba Queens ya Dar es Salaam wakifurahia jambo baada ya kumaliza mazoezi kuelekea fainali za Ligi ya Mabingwa ya Wanawake Afrika zinazotarajiwa kufanyika mwishoni mwa mwezi huu nchini Morocco. **PICHA: SIMBA SC**

# Simba Queens yawaza makubwa

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA mpya wa Timu ya Simba Queens, Charles Lukula, amesema hakuja Tanzania kufanya utalii na badala yake atajipanga kuipa mafanikio timu hiyo katika fainali za mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika , zitakazofanyika hivi karibuni nchini Morocco.

Lukula aliliambia gazeti hili malengo yake ni kuona wanafika hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo itakayofanyika kuanzia Oktoba 30, mwaka huu. Kocha huyo raia wa Uganda alisema kazi yake haitokuwa ngumu sana kwa sababu anafahamu ubora wa wachezaji wa Simba Queens, hivyo akiungana na benchi la ufundi alilolikuta atahakikisha wataifikisha mbali timu hiyo.

"Nina furaha sana kuwa hapa, lakini sikuja hapa kutalii bali kufanya kazi, tunakwenda kufanya kazi pamoja na benchi la ufundi nililolikuta. Mimi siyo malaika, ila nina uzoefu, ninakwenda kuiongoza timu ili ifike nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, lengo letu ni hilo," alisema Lukula.

Lukula alikuwa akiwafundisha mabingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Uganda, She Corporates ambapo katika mechi ya fainali ya CECAFA alifungwa bao 1-0 na wenyeji Simba Queens.

# Wizara ya Viwanda yaichapa RAS Tanga

**Na Cheji Bakari, TANGA**

TIMU ya Soka ya Wanaume ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji imeanza vyema michezo ya Shirikisho la Michezo ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI) kwa kuifunga RAS Tanga mabao 2-1 katika iliyochezwa juzi kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini hapa.

Michuano hiyo inayofanyika kila mwaka ilianza kutimua vumbi tangu Oktoba Mosi, mwaka huu.

Mchezo huo ulikuwa na kivutio kikubwa baada ya Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Omari Mgumba kuwa ni miongoni mwa wachezaji walioitumikia RAS Tanga.

Akizungumza baada ya mchezo huo kumalizika, Mgumba alisema anaishukuru serikali kutoa kibali kwa Jiji la Tanga kuwa mwenyeji wa mashindano na kuongeza si tu inaleta faida za kiafya kwa wachezaji lakini itasaidia kuinua uchumi wa wakazi wa mkoa huo.

Mgumba alisema katika kipindi cha siku 15 ambazo mashindano hayo yatafanyika, wenyeji watafaidika kwa kuingiza kipato kwa kutoa huduma ya malazi, chakula na usafiri wa kuona eneo moja hadi jingine.

"Hapa kuna timu takribani 50 za SHIMIWI ambapo mbali na kuondoa msongo wa mawazo pia wamepata mtoko na kuja kujifunza mambo mbalimbali yanayofanyika mkoani hapo, pia watoa huduma ya magari, hoteli, migahawa pia watapata riziki kutokana na kuja kwa ugeni huu," alisema Mgumba.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Utawala na Rasilimali Watu kutoka Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Veronica Nchango, aliliambia gazeti hili timu za wizara hiyo zimejipanga vyema kuhakikisha wanachukua vikombe mbalimbali.

Katika mchezo mwingine uliofanyika juzi, timu ya kuvuta kamba wanaume ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ilipata pointi tatu muhimu baada ya kuwashinda wenzao wa Bunge wakati timu ya Wanawake ya NEC pia ilipata ushindi wa mezani baada ya RAS Ruvuma kutotokea uwanjani.

Katika michezo mingine ya kuvuta kamba Mahakama Sports wanaume na wanawake wameibuka kidedea dhidi ya Haki ya RAS Singida.

Timu ya Wizara ya Maji ilibuka na ushindi dhidi ya RAS Mara kwa jumla ya magoli 4-1 wakati Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari wameifunga RAS Lindi mabao 2-0 na Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa (TAKUKURU) waliwaadhibu Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara magoli 2-0.

## ZISIKUPITE

### TUCHEL AIKATAA LEVERKUSEN

KOCHA wa zamani wa Chelsea, Thomas Tuchel, amekataa nafasi ya kuinoa klabu ya Bayer Leverkusen iliyozorota nyumbani kwao katika Ligi Kuu Ujerumani. ***(Sport1)***

### ALONSO ANUKIA LEVERKUSEN

KLABU ya Bayer Leverkusen inataka kumteua kiungo wa zamani wa Liverpool, Bayern Munich na Real Madrid, Xabi Alonso kuchukua nafasi ya kocha wa sasa, Gerardo Seoane. ***(ESPN)***

### COOPER MAMBO MAGUMU

MMILIKI wa Nottingham Forest, Evangelos Marinakis, anafikiria kumfukuza kocha, Steve Cooper na baadhi ya wafanyakazi wa klabu hiyo baada ya kufungwa mara tano mfululizo katika Ligi Kuu England. ***(Mail)***

### BENITEZ ANUKIA FOREST

KLABU ya Nottingham Forest inamfikiria kocha wa zamani wa Liverpool, Chelsea na Newcastle United, Rafael Benitez kuwa mbadala wa Steve Cooper, wakati kocha wa zamani wa Burnley, Sean Dyche pia akitajwa. ***(Guardian)***

### UNITED YAMBANA RONALDO

KLABU ya Manchester United inasitasita kumruhusu fowadi wa Ureno, Cristiano Ronaldo kuondoka katika dirisha la usajili la Januari na huenda mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 37 atalazimika kusubiri hadi mkataba wake uishe msimu ujao kabla ya kuondoka Old Trafford. ***(Mirror)***

### LEAO KUTUA CHELSEA

CHELSEA wanaongoza katika mbio za kumsajili, mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ureno mwenye umri wa miaka 23, Rafael Leao. ***(Star)***

### PULISIC ATAJWA MILAN

KLABU ya AC Milan inawaweza kutumia mechi yao dhidi ya Chelsea kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kuzungumza na The Blues kuhusu kumsajili beki wa England, Trevoh Chalobah mwenye umri wa miaka 23 na mshambuliaji wa Marekani, Christian Pulisic (24). ***(Calciomercato)***

### INTER YAMTAKA DE BEEK

INTER Milan wanaweza kujaribu kumsajili kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Uholanzi, Donny van de Beek mwenye umri wa miaka 25 kutoka Manchester United ifikapo Januari. ***(Fichajes)***

### LIVERPOOL KUMWAGA FEDHA

WAMILIKI wa Liverpool wako tayari kufadhili uhamisho wa fedha nyingi Januari ikiwa kocha wa Wekundu hao, Jurgen Klopp atapata mchezaji mzuri. ***(Football Insider)***

### KLOPP ALIMHITAJI ODEGAARD

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amesema alitaka kumsajili, Martin Odegaard wa Arsenal mwenye umri wa miaka 23 kwa klabu yake ya awali ya Borussia Dortmund, lakini kiungo huyo wa Norway alichagua kujiunga na Real Madrid. ***(Goal)***

### TROSSARD NJIA MOJA

LEANDRO Trossard mwenye umri wa miaka 27, amekataa kutupilia mbali uvumi unaomhusisha na kutaka kuondoka Brighton, huku Arsenal na Chelsea wakimtaka winga huyo wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji. ***(Mail)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# KLOPP AFURAHIA USHINDI WA ULAYA

●●●Aeleza wamepata walichotaka huku akiipongeza safu yake ya...

**LIVERPOOL, England**

JURGEN Klopp, amesema ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Rangers "ndio kile ambacho Liverpool walikihitaji" baada ya kuanzisha timu yake katika mfumo mpya kwenye mchezo huo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, Jumanne.

Liverpool wamekuwa na tatizo la kutawala mechi hadi sasa msimu huu huku wakipata ugumu usio wa kawaida katika kujilinda dhidi ya mashambulizi ya kushtukiza.

Hilo lilisababisha mabadiliko ya fikra kutoka kwa Klopp katika mchezo huo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Rangers, na wachezaji wake walimzawadia ushindi kwa mabao ya Trent Alexander-Arnold na Mohamed Salah.

Wakati Klopp alifurahishwa na safu yake ya ulinzi, jambo ambalo alifurahishwa zaidi ni namna Liverpool walivyomiliki mpira kwa asilimia kubwa tofauti na mechi zilizopita.

"Ilikuwa kile tulichohitaji usiku wa leo (juzi)," alisema akiiambia BT Sport.

"Kiwango kipya, tulilazimika kubadili mambo. Tulikuwa na nafasi nyingi na mchezo ulikuwa mzuri sana.

"Mabao mawili yalikuwa safi kabisa bila kuhitaji VAR."

Klopp pia, alimmwagia sifa pekee, Alexander-Arnold, ambaye uchezaji wake umekuwa ukiimarika kila siku licha ya kushtumiwa na kocha wa timu ya taifa ya England, Gareth Southgate kuwa hachezi kwa kujituma.

"Hakuna shida katika kulinda, katika wakati mzuri kila kitu kiko sawa,ikiwa hakuna ulinzi inaonekana kama hauna kitu," alisema.

"Tulitarajia afanye vyema zaidi - na tunaamini ataendelea kucheza kwa kiwango bora zaidi."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,037,3
MECHI KALI
OMANIA NICOSIA
VERSUS
MANCHESTER UTD
1 | 10.07
X | 5.49
2 | 1.27
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# CHRISTENSEN AUNGANA NA NYOTA 5 MAJERUHI BARCA

**MILAN, Italia**

HALI ya majeruhi katika kikosi cha Barcelona imezidi kuwa mbaya baada ya beki, Andreas Christensen kuumia kifundo cha mguu katika mechi ya Jumanne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ambayo ilimalizika kwa kufungwa bao 1-0 na Inter Milan.

Christensen, alitolewa nje ya mchezo dakika ya 58 baada ya kuhangaika kwa dakika chache na Barcelona wamethibitisha beki huyo ameumia kifundo cha mguu wa kushoto.

Klabu hiyo ilisema vipimo zaidi vilitarajiwa kufanywa jana ili kujua kiwango kamili cha jeraha hilo.

Jeraha la Christensen linakuja kabla ya mechi ngumu, kwani watamenyana na Celta Vigo kwenye Ligi Kuu Hispania, LaLiga, wikendi hii kabla ya mechi ya marudiano na Inter Milan, Oktoba 12 na Clasico dhidi ya Real Madrid itakayochezwa Oktoba 16, mwaka huu.

Pia Blaugrana, hao watacheza na Villarreal na Athletic Bilbao kwenye LaLiga baada ya hapo.

Beki huyo wa zamani wa Chelsea alibadilishwa na mkongwe Gerard Pique, ambaye huenda sasa akaanza badala yake kwenye mechi zijazo.



# De Beek ruksa kuondoka United

**MANCHESTER, England**

DONNY van de Beek amepewa ruhusa ya kuondoka Manchester United katika dirisha la usajili la Januari mwakani, kwa mujibu wa 90min.

Mholanzi huyo alijiunga na Mashetani Wekundu hao mwaka 2020, wakati timu hiyo ilipokuwa kwenye uhitaji mkubwa wa viungo.

Lakini, maisha ya Van de Beek pale United hayajaenda kabisa kama mipango ilivyotarajiwa.

Alianza mara nne pekee kwenye mechi za Ligi Kuu England katika msimu wake wa kwanza, na baada ya kushindwa kumfurahisha bosi wa muda, Ralf Rangnick mwaka jana, alipelekwa kwa mkopo Everton.

Kuwasili kwa Erik ten Hag, ambaye alimfundisha Van de Beek kule Ajax, kulileta imani mpya kwa kiungo huyo hatimaye angeingia kwenye kikosi cha kwanza cha United, lakini mambo yamekwenda tofauti.

Na sasa 90min imeelezwa wawakilishi wa Van de Beek wamearifiwa na United hawatamzuia kama anataka kuondoka Januari, ingawa pia anaweza kubaki na kupigania nafasi yake.

Klabu yake ya zamani ya Ajax, pamoja na wapinzani wao PSV Eindhoven wote wanavutiwa nae.



HABARI MICHEZO

361,877/-

# AZAM FC YAENDA LIBYA IKITAMBA KUFANYA KWELI

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha wachezaji 25 wa Azam FC kiliondoka nchini leo alfajiri kuelekea Benghazi, Libya kuwafuata wenyeji Al Khadar kwa ajili ya mechi ya kwanza ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika itakayochezwa keshokutwa kuanzia saa 2:00 usiku (saa za Tanzania), kwenye Uwanja wa Martyrs of February.

Ofisa Habari wa Azam FC, Thabit Zacharia 'Zaka Zakazi' alisema wanakwenda nchini humo kwa lengo moja tu la kuitendea haki nafasi ya timu nne ambazo Tanzania imepewa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF) kwa kufanya vizuri.

Zacharia alisema, wamejiandaa vyema kuwakabili wapinzani wao na wanatarajia kupata matokeo mazuri ili kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kusonga mbele.

"Tunakwenda na wachezaji 25, hatuwezi kwenda na wachezaji wote kwa sababu tutacheza mechi moja tu, kwa hiyo wengine ni lazima wabaki, mfano sisi tuna makipa wanne, hawawezi kwenda wote kwa ajili ya mechi moja tu. Lakini tunakwenda huko tukiwa tumejipanga, kila kitu tumekifanya sawa sawa, tuna imani kabisa tutafanya vizuri, tunataka tuonyeshe kwa nini ni sisi tu ndiyo tumeanzia raundi hiyo na CAF hawakupendelea," alisema kiongozi huyo.

Baada ya mechi hiyo, Azam itarudiana na Al Khadar Oktoba 16, mwaka huu kuanzia saa 1:00 usiku kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Endapo Azam itapata matokeo bora katika mechi zote mbili itasubiri kukutana na timu iliyotolewa katika hatua ya raundi ya kwanza ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa kucheza mechi za mchujo.

Wawakilishi wengine wa Tanzania waliobakia katika mashindano ya CAF ni Simba ambayo itaelekea Angola kuwafuata De Agosto wakati Yanga itawakaribisha Al Hilal kutoka Sudan hapo keshokutwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.



Wachezaji wa karate kutoka nchi 35 wakishiriki semina ya mchezo huo inayofanyika kwa siku saba chini ya mkufunzi wa kimataifa kutoka Japan, Shihan Naka kwa pamoja na Shihan Okuma kwenye viwanja vya Starlight Arena, Masaki, Dar es salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Yanga hatulali, Al Hilal

INATOKA UK. 32

"Tumemaliza mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Ruvu Shooting, sasa kazi iliyobaki ni kuona mwaka huu tunatinga hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya muda mrefu kutofika hatua hiyo, hili litafanikiwa endapo wachezaji watajituma na kujitoa kwa dakika 90 za mwanzo.

Nimeona baadhi ya mechi za Al Hilal, wako vizuri kuanzia kwa wachezaji hadi na benchi la ufundi, maandalizi yanaendelea vizuri kwa ajili ya kujipanga kuelekea mchezo huo, tunayafanyia kazi mapungufu yetu ikiwamo kuzidisha umakini wa kutumia nafasi tunazotengeneza hasa katika kipindi cha kwanza ili kujiwekea mazingira bora na si vinginevyo," Nabi alisema.

Alisema pia anaendelea kuwasisitiza wachezaji wake kila mmoja kuwajibika kutokana na majukumu waliyopewa kwa sababu kwa kufanya hivyo watafikia malengo yao ya kupata ushindi hapa nyumbani na kwenda ugenini kumalizia dakika 90 zilizobakia.

Naye Aziz Ki alisema amerejea nchini salama na anawashukuru viongozi wa Yanga kwa kumpa ushirikiano wakati wote tangu alipopata changamoto ya ugonjwa wa Uviko-19.

"Nina matumaini makubwa tutafanya vizuri (dhidi ya Al Hilal), tunachohitaji mashabiki ni kutuunga mkono kwa kufika uwanjani, uwepo wao utakuwa chachu kubwa kwetu kuongeza bidii," alisema Aziz Ki.

Aliongeza kurejea kikosini kwa Morrison kutaongeza nguvu katika timu yao na kila mchezaji yuko tayari kuonyesha uwezo wake.

"Tunashukuru changamoto tuliyoipata dhidi ya Ruvu Shooting, ni kama ilikuwa kipimo kizuri kwenye benchi letu la ufundi kwa ajili ya mechi inayokuja, ilibidi tuonyeshe sanaa yetu ya kushambulia na wao kuonyesha sanaa yao ya kuzuia, sasa akili na mawazo nguvu zote zipo kwenye mechi ya Jumamosi dhidi ya Al Hilal, tunataka tuvunje rekodi mbaya tuliyonayo ya Yanga kutocheza hatua ya makundi barani Afrika, wengi wanatubeza wakitutolea maneno ya hapa na pale, lakini ndiyo ukweli, " Ofisa Habari wa Yanga, Ally Kamwe alisema.

Kamwe alisema pia kikosi cha Al Hilal kinatarajiwa kutua nchini leo tayari kwa mchezo huo ambao maandalizi yake yamekamilika.

## Simba yafunguka

INATOKA UK. 32

Banda na Jimmyson Mwanuke ambao ni majeruhi.

Kabla ya kurudiana na Waangola hao, Simba ambao ni vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara itawafuata Singida Big Stars katika mchezo wa ligi hiyo utakaochezwa Oktoba 12, mwaka huu kwenye Uwanja wa CCM Liti ulioko mkoani Singida.

Simba inatarajia kuelekea Luanda, Angola na baada ya mechi itaondoka siku hiyo hiyo kwa ndege ya kukodi kurejea nyumbani kuwasubiri Waangola hao.


SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 08/10/22 | 17:00 | Millwall vs Middlesbrough | 2.63 | 3.13 | 2.73 |
| 02. 08/10/22 | 17:00 | Swansea vs Sunderland | 2.33 | 3.28 | 3.03 |
| 03. 08/10/22 | 17:00 | Wigan vs Cardiff | 2.35 | 3.18 | 3.08 |
| 04. 08/10/22 | 17:00 | Birmingham vs Bristol City | 2.59 | 3.24 | 2.69 |
| 05. 08/10/22 | 19:30 | Brighton vs Tottenham | 2.90 | 3.35 | 2.37 |
| 06. 08/10/22 | 19:30 | Sevilla FC vs Athletic Bilbao | 2.69 | 3.19 | 2.64 |
| 07. 08/10/22 | 22:30 | Pacos Ferreira vs Vitoria Guimaraes | 3.00 | 3.10 | 2.48 |
| 08. 09/10/22 | 14:00 | Huddersfield vs Hull City | 2.36 | 3.33 | 2.93 |
| 09. 09/10/22 | 15:00 | Valladolid vs Betis | 3.03 | 3.33 | 2.30 |
| 10. 09/10/22 | 16:00 | Salernitana vs Verona | 2.53 | 3.37 | 2.68 |
| 11. 09/10/22 | 16:00 | Udinese vs Atalanta | 2.63 | 3.37 | 2.58 |
| 12. 09/10/22 | 16:00 | Angers vs Strasbourg | 2.44 | 3.33 | 2.78 |
| 13. 09/10/22 | 17:15 | Cadiz CF vs Espanyol | 2.88 | 3.18 | 2.48 |
| 14. 09/10/22 | 18:30 | Arsenal vs Liverpool | 2.64 | 3.45 | 2.53 |
| 15. 09/10/22 | 18:30 | Hertha BSC vs SC Freiburg | 3.02 | 3.41 | 2.25 |
| 16. 09/10/22 | 19:30 | Real Sociedad vs Villarreal | 2.53 | 3.23 | 2.78 |
| 17. 09/10/22 | 20:30 | Stuttgart vs Union Berlin | 2.61 | 3.15 | 2.71 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 06/10/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 2908 | Nassaji Mazandaran vs Zob Ahan | 2.50 | 2.55 | 3.55 |
| 15:30 | 5953 | Peykan FC vs Aluminium Arak | 2.80 | 2.70 | 2.90 |
| 16:45 | 1690 | Al Hala Muharraq vs Muharraq SC | 4.58 | 3.51 | 1.68 |
| 16:45 | 3439 | Shams Azar Qazvin vs Shahrdari Astara | 1.71 | 2.87 | 6.02 |
| 17:00 | 1394 | Esteghlal Khuzestan vs Saipa Karadj | 2.31 | 2.62 | 3.50 |
| 17:00 | 3508 | Khalijfars Mahshahr vs Pars Jonoubi Jam | 3.55 | 2.95 | 2.23 |
| 17:45 | 4013 | Honka vs Inter Turku | 1.48 | 4.01 | 5.73 |
| 18:00 | 5070 | Shabab Al Ordun vs Moghayer AL Sarhan | 1.84 | 3.20 | 4.08 |
| 18:30 | 1469 | Al Taawon vs Al Wehda | 1.71 | 3.99 | 4.29 |
| 18:30 | 2659 | AL Tai vs Al Khaleej Club | 1.96 | 3.70 | 3.45 |
| 19:00 | 2002 | Valerenga IF 2 vs Baerum | 2.48 | 3.99 | 2.24 |
| 19:15 | 1521 | AL Sahel vs AL Arabi | 3.11 | 3.40 | 2.06 |
| 19:45 | 1441 | Sivasspor vs KF Ballkani | 1.46 | 4.49 | 6.54 |
| 19:45 | 1542 | Sheriff Tiraspol vs Real Sociedad | 5.69 | 4.06 | 1.54 |
| 19:45 | 1771 | FC Zurich vs PSV Eindhoven | 5.02 | 4.22 | 1.58 |
| 19:45 | 2056 | HJK Helsinki vs Ludogorets Razgrad | 3.40 | 3.35 | 2.09 |
| 19:45 | 2482 | Pyunik Yerevan vs Zalgiris | 2.40 | 3.22 | 2.92 |
| 19:45 | 2515 | Red Star Belgrade vs Ferencvaros TC | 1.91 | 3.54 | 3.79 |
| 19:45 | 3162 | Slovacko vs Nice | 3.68 | 3.48 | 1.96 |
| 19:45 | 3467 | Anderlecht vs West Ham | 3.54 | 3.49 | 2.00 |
| 19:45 | 4394 | Molde vs Shamrock Rovers | 1.29 | 5.22 | 9.43 |
| 19:45 | 4486 | Lech Poznan vs Hapoel Beer Sheva | 1.95 | 3.51 | 3.66 |
| 19:45 | 4977 | Silkeborg vs Steaua Bucuresti | 1.69 | 3.71 | 4.82 |
| 19:45 | 4989 | SC Dnipro 1 vs FC Vaduz | 1.68 | 3.74 | 4.79 |
| 19:45 | 5402 | Sturm Graz vs Lazio | 4.58 | 3.88 | 1.68 |
| 19:45 | 5841 | Malmo vs Union Berlin | 3.65 | 3.40 | 1.99 |
| 19:45 | 5855 | Monaco vs Trabzonspor | 1.54 | 4.24 | 5.46 |
| 19:45 | 5878 | Omonia Nicosia vs Manchester Utd | 10.07 | 5.49 | 1.27 |
| 21:00 | 3969 | AL Baten vs Dhamk | 15.96 | 6.98 | 1.16 |
| 21:00 | 4630 | Al Shabab Riyadh vs Al Raed Club | 1.39 | 4.75 | 7.07 |
| 21:00 | 5494 | Al-Ettifaq vs Al Hilal Riyadh | 4.89 | 3.99 | 1.63 |
| 21:45 | 2289 | GKS Piast Gliwice vs Rakow Czestochowa | 4.19 | 3.32 | 1.79 |
| 22:00 | 1472 | SC Freiburg vs Nantes | 1.56 | 4.12 | 5.42 |
| 22:00 | 1580 | FC Koln vs Partizan | 1.38 | 4.85 | 7.07 |
| 22:00 | 1667 | Rigas Futbola Skola vs Basaksehir | 5.61 | 4.11 | 1.54 |
| 22:00 | 2046 | KAA Gent vs Djurgardens IF | 1.69 | 3.79 | 4.69 |
| 22:00 | 2211 | Fenerbahce vs AEK Larnaca | 1.36 | 4.88 | 7.57 |
| 22:00 | 2769 | Villarreal vs Austria Vienna | 1.16 | 7.01 | 15.02 |
| 22:00 | 3238 | Slavia Prague vs CFR Cluj | 1.50 | 4.28 | 6.32 |
| 22:00 | 3731 | Roma vs Betis | 1.78 | 3.70 | 4.20 |
| 22:00 | 4355 | Sporting Braga vs Union Saint Gilloise | 1.83 | 3.48 | 4.24 |
| 22:00 | 4388 | Rennes vs Dynamo Kiev | 1.44 | 4.40 | 6.79 |
| 22:00 | 4968 | Midtjylland vs Feyenoord | 2.95 | 3.65 | 2.19 |
| 22:00 | 5143 | AZ Alkmaar vs Apollon Limassol | 1.39 | 4.78 | 7.18 |
| 22:00 | 5145 | Arsenal vs Bodo Glimt | 1.25 | 5.95 | 9.92 |
| 22:00 | 5500 | FC Basel vs Slovan Bratislava | 1.59 | 4.11 | 5.01 |
| 22:00 | 5558 | Olympiakos vs Karabakh | 1.87 | 3.64 | 3.84 |
| 22:00 | 5637 | Hearts vs Fiorentina | 5.20 | 3.85 | 1.62 |
| 23:30 | 3380 | Resistencia FC vs Libertad Asuncion | 5.06 | 3.90 | 1.55 |
| 23:30 | 4039 | SOL De America vs Nacional Asuncion | 3.12 | 3.22 | 2.13 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Alhamisi Oktoba 6, 2022

Nipashe




Klopp afurahia ushindi wa Ulaya

# Simba yafunguka inachokitaka CAF

●●●Pia yaeleza wamejipanga kutowadharau wapinzani wao kwa sababu wanahitaji...

**Na Adam Fungamwango**

KATIKA kuhakikisha inajiweka katika nafasi nzuri ya kusonga mbele katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, mabosi wa Simba wamesema kamwe hawatawadharau wapinzani wao, Primeiro de Agosto ya Angola, imefahamika.

Primeiro de Agosto inatarajia kuikaribisha Simba katika mechi ya kwanza ya hatua ya kwanza itakayochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Estadio 11 de Novembro mjini Luanda.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema jana wamejipanga kucheza kwa tahadhari kwa sababu wanafahamu ubora wa wapinzani wao na rekodi nzuri waliyonayo walipokutana mara ya mwisho.

Ahmed alisema wanafahamu mechi hiyo haitakuwa rahisi kama baadhi ya watu wanavyodhani kutokana na wapinzani wao kuwa na kikosi bora, ambacho kinatarajiwa kuwapa ushindi.

Alisema Simba haitabweteka katika mechi hiyo ya kwanza na ile ya marudiano itakayochezwa Oktoba 16, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

"Tumeshapeleka mtu Angola kwa ajili ya maandalizi ya awali, ameshafanya kila kitu, tunajua wapi tutafikia, wapi tutafanya mazoezi, hii ni kuonyesha ni namna gani tuko makini na tuna dhamira ya kutinga hatua ya makundi.

Hatuichukulii poa hata kidogo timu hiyo kwa sababu tunafahamu ubora wao, msidhani kama tunawadharau wapinzani wetu, wao pia kama sisi wana dhamira ya kutaka kutinga hatua ya makundi," alisema Ahmed.

Ofisa huyo aliongeza malengo ya Simba msimu huu ni kufika robo fainali au kwenda mbele zaidi kwa sababu uwezo wa kufika hatua hiyo wanao.

"Tukifika robo fainali tutakuwa hatujafeli ila tutakuwa tumeishi pale tu ambapo tumeishia msimu uliopita. Tukitolewa hatua hii, au tukaingia makundi na kushindwa kuvuka, tutakuwa tumeshindwa, tena kwa kiasi kikubwa, kitu ambacho hatutaki kukipa nafasi kwenye klabu yetu kwa sasa," alisema Ahmed.

Aliongeza kwa sasa Kaimu Kocha wa timu hiyo, Juma Mgunda, yuko katika harakati za kukiimarisha kikosi chao kwa ajili ya mechi hiyo na ile ya marudiano ili kufikia malengo.

"Mpira wa kisasa ni mbinu, morali, na kujiamini ukiwa na kitu hicho kwenye timu yako unaweza kupata ushindi sehemu yoyote ile, tunamshukuru kocha Mgunda kwa sababu amekuwa ni zaidi ya kocha, ni kocha, mlezi na mwanasaikolojia, anaweza kulea wachezaji, hata akikata tamaa ana namna ya kuzungumza nao kama baba, pia anaweza kucheza na saikolojia ya wachezaji, amewabadilisha wachezaji kwa sababu wamekuwa wakipambana uwanjani, wana morali na kujiamini kumeongezeka chini yake," Ahmed alisema.

Naye Mgunda aliliambia gazeti hili hana hofu na wachezaji wake kwa sababu wanafahamu wanachotakiwa kukifanya katika mechi zote mbili.

Mgunda alisema licha ya timu yake kupata ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Dodoma Jiji, bado analazimika kurekebisha makosa yaliyojitokeza na hilo ni jambo la kawaida katika mchezo wa soka.

"Tunakabiliwa na dakika 180 ngumu za ugenini na nyumbani, katika soka hakuna mechi rahisi, sisi tunajipanga na wenzetu pia wanajipanga, ili kuona tunapata matokeo chanya, tunaendelea kujiimarisha kwa kufanyia kazi mapungufu yetu," alisema Mgunda.

Katika mchezo huo wa Jumapili, Simba itaendelea kukosa huduma ya beki wake, Shomari Kapombe, Peter

INAENDELEA UK. 31



Wachezaji wa Azam FC wakifanya mazoezi kabla ya leo kuanza safari ya kuelekea Libya kwa ajili ya kuwafuata wenyeji, Al Khadar katika mechi ya mashindano ya kimataifa Kombe la Shirikisho Afrika itakayochezwa keshokutwa mjini Benghazi. **PICHA: MTANDAO**

## Yanga hatulali, Al Hilal ikiwasili

**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

WAKATI kiungo wa Yanga, Stephanie Aziz Ki, ameshajiunga na kikosi cha timu hiyo, Kocha Mkuu, Nesreddine Nabi amesema anaendelea na mkakati wa kuiimarisha safu yake ya kiungo, winga na ushambuliaji baada ya kuona ubora wa wapinzani wao katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Al Hilal ya Sudan.

Nyota wanaotajwa kupewa majukumu ya kuhakikisha Yanga inavuna matokeo chanya ni pamoja na Tuisila Kisinda, Bernard Morrison, Jesus Moloko, Yannick Bangala, Fiston Mayele na Aziz Ki ambaye yuko tayari kwa mchezo huo wa kwanza utakaochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Hata hivyo Aziz Ki anaonekana bado hajaimarika vizuri kutokana na changamoto ya kiafya iliyokuwa inamkabili na kusababisha kuchelewa kurejea nchini baada ya kukwama Morocco alipokuwa na Timu ya Taifa ya Burkina Faso mechi za kimataifa zinazotambuliwa na Kalenda ya Shirikisho la Soka Duniani (FIFA).

Nabi aliliambia gazeti hili jana ameona ubora na udhaifu wa wapinzani wao na ameanza kuyafanyia kazi haraka kwa ajili ya kujiweka imara na tayari kwa mchezo huo.

"Tumeongeza mazoezi na kupata mbinu wachezaji wa nafasi ya kiungo na washambuliaji, hawa ndio roho ya timu, wakifanya vizuri, tutarajie matokeo chanya, hatututulia kwa sababu tunakutana na timu yenye uzoefu pia," Nabi alisema.

Aliongeza kikubwa wanatakiwa kuongeza umakini hasa kwenye safu ya ushambuliaji ambayo inatakiwa kutumia vyema nafasi wanazotengeneza kuanzia kipindi cha kwanza.

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >